# Nipashe

Jumatano Oktoba 26, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581110

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710

LIKE & FOLLOW US



SUPA JACKPOT

TZS.1,044,303,118

KWA TZS. 1000 TU!

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SportPesa.CO.TZ

PIGA *150*87#




**Sugu:** Bado nipo, tukutane Mbeya Mjini mwaka 2025

UKURASA 3



Congo na imani kwa Tanzania ndiyo baba wa uchumi wa DRC

Bilionea Rishi Sunak anapoahidi uadilifu mkubwa kwa Waingereza

siasa

HABARI BORA NA KAMILIFU

Nipashe

TOM JOSEPH MBOYA

Shujaa wa uhuru, maendeleo ya Kenya aliyezawadiwa kifo

TAKUKURU, ZAECA NJIA PANDA

Ni kuchunguza watuhumiwa wanapoelekezwa si 'kulianzisha'

UKURASA 13



Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Aldof Mkenda akizungumza na mtahiniwa wa darasa la saba aliyebadilishiwa namba ya mtihani katika Shule ya Chalinze Modern Islamic, Iptisum Slim, kabla ya kuzungumza na waandishi wa habari mkoani Dar es Salaam jana. **PICHA: ROMANA MALLYA**

# Sasa shule aliyoishtaki mwanafunzi kufungiwa

• **Ni** yule aliyedai kubadilishiwa namba ya mtihani, uchunguzi waibua... *Ukurasa 2*

## YALIYOMO

**UKURASA WA 4**

**WATUMIAJI MTANDAO INTANETI WAONGEZEKA**

MAMLAKA ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), imetoa takwimu za robo ya...

## Tanzania yapata soko la uhakika korosho Marekani

UKURASA 3



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akipata maelezo kwa Rais na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya Sung Shin Rolling Stock ya Korea, Gye Shul Park (wa pili kulia), kuhusu mabehewa ya reli ya kisasa (SGR) alipotembelea kujionea maendeleo ya utengenezaji wake ikiwa ni ziara ya kikazi nchini humo, jana. **PICHA: OWM**

# Mgawo wa maji rasmi Dar, Pwani

UK. 2

**MICHEZO** **NABI NJIAPANDA YANGA IKIIVAA KMC** UK.32 **KABWELA** UK.7




Mkurugenzi wa Rasilimali Watu na Utawala wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), Francis Sangunaa, akifungua mkutano mkuu wa 54 wa mwaka 2022 wa Chama cha Ushirika cha Akiba na Mikopo cha Wafanyakazi wa Shirika hilo (TANESCO SACCOS), jijini Dar es Salaam. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Shule iliyoshtakiwa na mwanafunzi kufungiwa

**Na Romana Mallya**

WAZIRI wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Profesa Adolf Mkenda, ameagiza kufungwa kwa Shule ya Msingi na Sekondari ya Chalinze Modern Islamic, baada ya kubainika kuwapo kwa uzembe uliosababisha wanafunzi saba kubadilishiwa namba za mitihani.

Sambamba na hatua hiyo, ameagiza walimu na wasimamizi waliohusika na udanganyifu huo, wachukuliwe hatua kali ikiwamo kufukuzwa kazi.

Mkenda alitoa maagizo hayo jana mkoani Dar es Salaam wakati akitoa ripoti ya uchunguzi kuhusiana na madai yaliyotolewa awali na mwanafunzi wa shule hiyo, Iptisum Slim.

Oktoba 13, mwaka huu, mwanafunzi huyo kupitia mitandao ya kijamii alisikika akidai kuwa wakati wa mtihani wa taifa wa kumaliza darasa la saba alibadilishiwa namba ya mtihani.

Kutokana na tuhuma hizo ililazimu Baraza la Mitihani la Taifa (NECTA) kufanya uchunguzi wa kina kufahamu undani wa tukio hilo.

Akitoa ripoti ya uchunguzi ya tukio hilo, Waziri Mkenda alisema wamebaini ni kweli mtahiniwa Iptisum Slim na wengine sita shuleni hapo walibadilishiwa namba zao za mitihani.

Dosari hiyo, alisema ilisababishwa na uzembe wa watumishi wanne ambao ni msimamizi wa mkondo, Muddy Mndeme; msimamizi mkuu, Vitalisa Kindole, Mwalimu Mkuu, Amran Ramadhani na Mwalimu wa Takwimu, Rajab Kijangwa ambao wamekiri makosa yao.

Waziri Mkenda alisema baada ya taarifa hiyo, serikali kupitia NECTA ilichukua hatua kwa kuwasiliana na Kamati ya Uendeshaji Mitihani ya Mkoa wa Pwani kwa kuielekeza kufanya uchunguzi na kuwasilisha taarifa baraza la mitihani.

Pia alisema walitaka wafanye uchunguzi wa miandiko ya watahiniwa kwenye karatasi zao kwa kutumia wataalamu wa maandishi kutoka Jeshi la Polisi.

"Uchunguzi uliofanywa umebaini mtahiniwa Iptisum alifanya masomo matano kwa kutumia namba PS.1408009/0040 na somo la mwisho la sita alifanya kwa kutumia namba PS.1408009/0039 kama alivyodai. Alichosema ni kweli," alisema.

Alisema watahiniwa wengine wanne nao walibadilishiwa namba katika somo la sita ambao ni Jasmin Mzee aliyefanya mitihani mitano kwa kutumia namba PS1408009/0041 na somo la sita (mwisho) kwa kutumia namba PS1408009/0040.

Wengine aliwataja kuwa ni Jokha Nassor alifanya mitihani mitano kwa kutumia namba PS1408009/0042 na somo la sita kwa kutumia namba PS1408009/0041.

Waziri Mkenda alisema mtahiniwa mwingine Khailat Mohamed alifanya mitihani mitano kwa kutumia namba PS1408009/0043 na somo la sita kwa kutumia namba PS1408009/0042 na Khaula Mruma alifanya mitihani mitano kwa kutumia namba PS1408009/0039 na somo la sita kwa kutumia namba PS1408009/0043.

Pia alisema uchunguzi ulibaini mwandiko wa mtahiniwa PS1408009/0033 katika masomo matano unafanana na mwandiko wa mtahiniwa PS1408009/0034 katika somo la sita.

"Mwandiko wa mtahiniwa PS1408009/0034 katika masomo matano unafanana na mwandiko wa mtahiniwa PS1408009/0033 katika somo la sita.

Mwandiko wa mtahiniwa PS1408009/0040 katika masomo matano unafanana na mwandiko wa mtahiniwa PS1408009/0039 katika somo la sita," alisema.

Kadhalika, alisema mwandiko wa mtahiniwa PS1408009/0039 katika masomo matano unafanana na mwandiko wa mtahiniwa PS1408009/0043 katika somo la sita, kadhalika mwandiko wa mtahiniwa PS1408009/0041 katika masomo matano unafanana na mwandiko wa mtahiniwa PS1408009/0040 katika somo la sita.

Alisema mwandiko wa mtahiniwa PS1408009/0042 katika masomo matano unafanana na mwandiko wa mtahiniwa PS1408009/0041 katika somo la sita. Pia alisema mwandiko wa mtahiniwa PS1408009/0043 katika masomo matano unafanana na mwandiko wa mtahiniwa PS1408009/0042 katika somo la sita.

Prof. Mkenda alisema uchunguzi ulibaini kuwa mwanafunzi huyo (Iptisum) pamoja na wenzake sita shuleni hapo walibadilishiwa namba ya mtihani.

Alieleza kuwa kutokana na uzembe huo NECTA imefanya marekebisho ya namba za mitihani za watahiniwa hao ili kila mmoja aweze kupewa matokeo yake halali.

**ATOA MAAGIZO**

Prof. Mkenda alisema kwa mujibu wa kifungu cha 4(8) cha kanuni za mitihani 2016, Shule ya Awali na Msingi Chalinze Modern Islamic inafungiwa kuwa kituo cha mitihani kwa muda usiojulikana.

Alisema pia watumishi wa serikali waliohusika wataandikiwa barua na kufukuzwa kazi na kuagiza mmiliki wa shule kuwafukuza kazi walimu waliohusika na kwamba endapo hawatachukua uamuzi huo ofisa elimu aifute shule hiyo.

Kuhusu mashtaka dhidi ya waliosababisha uzembe huo, Prof. Mkenda alisema watazungumza na mwanasheria ili kuona kama kuna jinai ili hatua zaidi dhidi yao zichukuliwe.

Alisema shule yoyote itakayobainika kufanya vitendo vya udanganyifu wa mitihani itafungiwa au kufutwa kuendesha shughuli za elimu.

Baba mzazi wa mtoto huyo, Suleiman Said na mama mzazi, Atwiya Mohamed ambao walikuwapo jana wakati waziri akitoa ripoti hiyo, walipongeza hatua iliyochukuliwa na serikali kwa kuhakikisha watoto hao wanapata haki zao.

# Mgawo wa maji rasmi Dar, Pwani

**Na Frank Monyo**

KAMATI ya Ulinzi na Usalama Mkoa wa Dar es Salaam na Pwani imetangaza mgawo wa maji katika mikoa hiyo kutokana na kupungua kwa kina katika Chanzo cha Ruvu Juu na Chini vinavyohudumiwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira (DAWASA).

Vyanzo hivyo kwa pamoja vilikuwa vinazalisha maji lita milioni 466 kwa saa, sasa vinazalisha milioni 300 sawa na asilimia 64 kwa saa.

Akitoa tamko hilo jana mkoani Pwani, Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makalla, ambaye pia ni Mwenyekiti wa kamati hiyo, alisema wamefanya ziara hiyo kwa niaba ya wakuu wa mikoa ya Pwani na Morogoro kwa lengo la kukagua na kufanya tathmini hali ya vyanzo vya maji chanzo cha Ruvu Juu na Chini.

"Hali ya maji imeshuka kwenye vyanzo vya maji (Ruvu Juu na Chini) kwa kiasi kikubwa na kwa taarifa zilizopo ni kwamba vyanzo vyote viwili kwa pamoja vinazalisha lita milioni 466 na hali iliyopo sasa vinazalisha lita milioni 300, kwa maana hiyo kitakuwa na upungufu wa maji kwa Mkoa wa Dar es salaam na sehemu ya Mkoa wa Pwani," alisema.

"Tulitarajia ikifika mwezi wa 10 (Oktoba) mvua za vuli ambazo zinakuja kusaidia kuongeza maji katika vyanzo viwili, lakini kwa taarifa za TMA, safari hii kutakuwa na kiangazi cha muda mrefu na ndio chanzo cha kina kushuka katika vyanzo vya maji."

Vile vile, Makalla alisema serikali na Bodi ya DAWASA imefanya jitihada kubwa maji yaliyopo yatumike vizuri na Kamati za Ulinzi na Usalama Dar es Salaam na Pwani kwa kutimiza majukumu kwa kuhakikisha wote wanaochepusha maji hawafanyi hivyo.

"Serikali inafanya kila jitihada kuhakikisha hiki kidogo (maji) kilichopo kinawafikia wananchi. Asijee mtu akafikiri hata mvua inaletwa na serikali au sera za Chama cha Mapindizi, suala la mvua ni kudra za Mwenyezi Mungu na ukiona upungufu wa maji suala ni mvua," alisema Makalla.

Aliwaomba wakazi wa Mkoa wa Dar es Salaam na Pwani, kutumia maji vizuri huku serikali ikifanya jitihada za kupunguza makali ya uhaba wa huduma hiyo.

Aliiagiza DAWASA kuhakikisha chanzo cha maji cha visima vilivyopo Kigamboni vinavyotoa lita milioni 70 vianze kutumika ifikapo mwishoni mwa mwezi Oktoba, mwaka huu.

"Ukifanya kazi mradi wa Kigamboni utakuwa na uwezo wa kuzalisha lita milioni 70 ambazo zitasaidia wakazi wa Kigamboni na maeneo ya katikati ya jiji.

"Ninazo taarifa kutoka kwa wananchi wa Kigamboni na Dar es Salaam wananitumia sms (ujumbe mfupi) kwamba kuna mgawo wa maji, mimi nimekuja kuthibitisha kwamba ni kweli kina cha maji kimepungua kwa asilimia 64 kwa vyovyote vile kutakuwa na mgawo wa maji," alisema.

Alisistiza kuwa viongozi wa mikoa mitatu (Dar es Salaam, Pwani na Morogoro) wataendelea kutoa elimu na kuhakikisha maji yanayopatikana asitokee mtu mwengine akayaharibu na kuomba Mungu mvua ziendelee kunyesha.

# Tanzania yapata soko la uhakika korosho Marekani

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WAZIRI wa Kilimo, Hussein Bashe, amesema Tanzania imepata soko la uhakika la kuuza korosho nchini Marekani tani saba.

Alisema serikali imetenga Shilingi trilioni nne kwa ajili ya kilimo cha bustani ili kuwainua wakulima kiuchumi, pamoja na kupanua soko la mazao hayo.

Alibainisha hayo jana mkoani hapa wakati akizungumza na waandishi wa habari wakati wa uzinduzi wa mkakati wa taifa wa mazao ya bustani.

Alisema serikali inatekeleza hayo ili kuboresha mpango wa kusindika mazao hayo badala ya kuuza ghafi ili kuyaongezea thamani ikiwamo wakulima kuwa na tija zaidi.

Alisema kilimo cha bustani ni muhimu kwa kuwa kinaongeza pato kwa mkulima na serikali ikiwamo kuzalisha ajira kwa vijana na wanawake na kuongeza lishe kwenye jamii.

"Serikali imejipanga kuhakikisha kilimo hicho kinazidi kusonga mbele na katika bajeti ya mwakani fedha lazima zitengwe," alisema Bashe.

Akizungumzia kilimo cha korosho, Bashe alisema serikali imepata soko la kupeleka tani saba za zao hilo nchini Marekani.

Alisema soko hilo wamelitafuta kwa muda wa miaka mitatu na zaidi na kwamba wataendelea kulinda soko hilo ili kuwainua wakulima lengo ni kuona wanaendesha kilimo chenye tija.

Naye Katibu Mkuu Kilimo, Andrew Massawe, alisema uamuzi wa kuandaa mkakati umetokana na maombi ya wadau mbalimbali na vikao vilivyofanyika wizarani.

Bashe alisema mkakati unalenga kutoa msukumo katika kuongeza tija, malighafi za viwanda masoko ya ndani na nje ya mazao ya bustani.

Alisema uandaaji wake umeshirikisha wataalamu wa Wizara ya Kilimo na sekta binafsi

Mwakilishi wa Umoja wa Ulaya (EU), Collins Scott, alisema EU inaunga mkono mipango ya serikali ya kuongeza uzalishaji kwenye kilimo cha bustani. Alisema lengo ni kuboresha uzalishaji wa kilimo hicho, uwezeshaji wa masoko na uwekezaji.

Mkurugenzi wa World Vegetable Center, Gabriel Rugalema alisema utekelezaji wa mkakati unahitaji uwe wa haraka na tija.

Alisema mchango wao kwenye mkakati huo ni ushiriki katika uwezeshaji pamoja na utoaji wa mbegu na utaalamu.

Alisema pia watasaidia katika upatikanaji wa mazao mapya na kuongeza mnyororo wa thamani wa mazao ya bustani ili yasaidie lishe bora, kipato na ajira.

## Kamati kuchunguza Bodi Mikopo yadaiwa kuhujumiwa

**Na Romana Mallya**

WAZIRI wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Aldof Mkenda, amesema amebaini kuna baadhi ya watu wanashawishi kamati aliyoiunda kuchunguza utolewaji wa mikopo katika Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB), isiendelee na kazi hiyo.

Julai, mwaka huu, Waziri Mkenda alitangaza kuunda kamati ya watu watatu ikiongozwa na Prof. Allan Mushi wa Chuo Kikuu Mzumbe kuchunguza malalamiko dhidi ya HESLB kwamba kuna upendeleo katika utoaji wa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu nchini.

Wengine wanaounda kamati hiyo ni Idd Makame kutoka Zanzibar na Dk. Martin Chegeni ambao wote kwa pamoja ni wataalamu wa mifumo katika sayansi ya kompyuta na takwimu.

Akizungumza na waandishi wa habari jana mkoani Dar es Salaam kuhusiana na kamati hiyo, Waziri Mkenda alisema aliiunda ili kufanya uchunguzi wa malalamiko ya mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu.

"Kumekuwa na kusuasua kwenye HESLB mara wapite huku mara huku, uchunguzi nilisema ufanyike kwa miaka mitano lengo lake ni kwa sababu tungependa kidogo tulichonacho kitolewe kwa haki kisaidie wale wenye uhitaji mkubwa zaidi. "Ile kamati inashawishi huku inapita huku, kamati ya waziri haisimamishwi kufanya kazi, wasishawishi na HESLB pengine tutawachukulia hatua kama watashawishi kwa maana wanataka kutuambia pengine wanataka kuficha mambo," alisema.

Prof. Mkenda alibainisha kuwa taarifa ya kamati hiyo itafanyiwa kazi ndani na haina lengo la kuweka hadharani mtoto wa nani amepata mkopo.




Askari wa Kikosi cha Usalama Barabarani, wakikagua ajali baada ya basi la kampuni ya Lim kugongana na gari dogo, Bunju mkoani Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Sugu: Bado nipo kwenye siasa tukutane 2025

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

JOTO la kisiasa limeanza kupanda jijini Mbeya baada ya aliyekuwa Mbunge wa Mbeya Mjini kwa tiketi ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Joseph Mbilinyi, maarufu Sugu, kutangaza nia yake ya kumvaa Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2025.

Akizungumza katika mahojiano maalum na Nipashe jana, Sugu alisema amefikia uamuzi huo baada ya makundi mbalimbali ya wananchi kumwomba arejee kwenye nafasi hiyo.

Sugu alisema wananchi hao wamekuwa wakimweleza kuwa alikuwa na mchango mkubwa kwenye maendeleo ya jiji hilo kuliko mbunge aliyepo sasa hivi madarakani.

Alisema wananchi wa Jiji la Mbeya wanamhitaji kwa ajili ya kuyasemea mahitaji na vikwazo vinavyowakabili kwenye sekta mbalimbali ikiwamo miundombinu ya barabara na kwamba amewasikia na muda ukifika atagombea tena.

"Bado naendelea kuishi mioyoni mwa wananchi wa Jimbo la Mbeya Mjini kutokana na mazuri niliyoyafanya kabla na wakati wa ubunge wangu. Nilifanya mengi kama vile ujenzi wa barabara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali," alisema.

"Nilifanya kazi kubwa pia kwenye maboresho ya sekta ya afya na kuwasaidia wajasiriamali. Nimeendelea kuwasaidia wananchi wenye matatizo mbalimbali ambao hufika nyumbani kwangu. Nadhani ndiyo sababu wananchi hawa bado wananihitaji," aliongeza.

Pia alisema akipita mitaani watu wanamkimbilia kwa lengo la kumlaki na kumsalimia huku wakisema 'wamenimiss' (wamemkumbuka) arudi tena ulingoni.

Sugu alisisitiza kuwa anafarijika kuona bado wananchi wa jimbo hilo wanampenda na kwamba watu hao asilimia kubwa ndio wapigakura, hivyo akasema ameshakubaliana na matakwa ya wananchi hao.

Alisema kwa miaka miwili aliyokaa nje ya bunge kitu kilichopungua ni mshahara wa ubunge lakini maisha mengine yanaendelea zikiwamo biashara zake mbalimbali kama vile hoteli ya Desderia ambayo ni ya kitalii.

Sambamba na hilo, alisema anaendelea na shughuli yake ya sanaa ya muziki na mara kadhaa amekuwa akitoa nyimbo mbalimbali ambazo zimelenga kuelimisha na kuburudisha jamii.

"Katika maisha haya nimejifunza kwamba kama ipo ipo tu. Wana Mbeya nawaomba waendelee kuwa na subira licha ya kwamba nimejaribu kukaa kimya lakini bado wananchi wanafuata wanaleta mambo yao mbalimbali," alisema Sugu.

Alisema katika baadhi ya maeneo ya jiji hilo amekuwa akitoa zawadi za mipira na jezi kwa vilabu mbalimbali vya mpira wa miguu ili kuwasaidia vijana kuonyesha vipaji vyao.

Hivi karibuni, Sugu amekuwa akipita katika maeneo mbalimbali ya jiji la Mbeya yakiwamo ya sokoni na kwenye vituo vya daladala kwa lengo la kuwasalimia wananchi na kupiga nao 'stori'.

Pia Sugu amekuwa akiishi maisha ya kawaida na wananchi hao ambapo amekuwa akiingia sokoni kwa ajili ya kununua bidhaa mbalimbali za wananchi zikiwamo nyanya na mboga za majani.

# TCRA: Watumiaji mtandao intaneti wameongezeka nchini

**Na Halfani Chusi**

MAMLAKA ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), imetoa takwimu za robo ya kwanza zinazoonyesha watumiaji wa intaneti nchini kwa kipindi cha Juni hadi Septemba, mwaka huu wameongezeka kutoka milioni 29.9 hadi 31.1 likiwa ni ongezeko la asilimia 6.7.

Pia huduma za kifedha kupitia simu za mkononi zimeongezeka kutoka Sh. milioni 38 hadi Sh. milioni 39.6, huku idadi ya miamala ikiongezeka kutoka Sh. bilioni 349.9 hadi Sh. bilioni 366.1.

Mkurugenzi Mkuu wa TCRA, Dk. Jabir Bakari, aliyasema hayo jana mkoani Dar es Salaam wakati akitoa mukhtasari kuhusu maendeleo ya sekta ya mawasiliano kwa robo ya kwanza ya mwaka 2022/23.

Dk. Bakari alisema mwelekeo wa ongezeko la watumiaji wa intaneti unaonyesha kulikuwa na ukuaji wa takribani asilimia 17 kila mwaka katika kipindi cha miaka mitano.

Alisema kwa mwaka 2017 kulikuwa na watumiaji milioni 16.1 na mwisho wa mwaka 2021 waliongezeka kufikia milioni 29.1.

Kuhusu idadi ya watumiaji wa mitandao ya kijamii, Dk. Bakari alisema mtandao wa Facebook uliongoza kwa kurekodi GB bilioni 2.59 ukifuatiwa na You Tube wenye GB bilioni 1.91, Whatsapp GB bilioni 1.58, TikTok GB milioni 999.

Kuhusu huduma za simu, Dk. Bakari alisema kuna ongezeko la asilimia 3.4 kwa laini za simu zinazotumika, hadi Septemba mwaka huu kulikuwa na laini milioni 58.1 ikilinganishwa na laini milioni 56.2 zilizokuwapo Juni.

Dk. Bakari alisema takwimu zinaonyesha mikoa mitano inayoongoza kwa kuwa na idadi kubwa ya laini za simu zinazotumika ni Dar es Salaam, milioni 9.7, Mwanza (milioni 3.7), Arusha (milioni 3.4), Mbeya (milioni 3.08) na Tabora (milioni 3.06).

Kuhusu gharama za vifurushi vya simu na data Dk. Bakari alisema wastani wa gharama za vifurushi vya simu zilikuwa ni Sh. 7.8 kwa kupiga simu ndani ya mtandao kwa kipindi cha Septemba kutoka Sh. 7.7 iliyokuwapo kwa Juni.

Dk. Bakari alisema: "Pamoja na ongezeko hili dogo, gharama bado ni chini kulinganisha na vifurushi vya simu kwenda mitandao mingine. Wastani wa vifurushi vya simu kwenda mitandao mingine ulikuwa Sh. 8.1 kwa Septemba ikiwa ni ongezeko kutoka Sh. 7.6 kwa Juni".




Mkuu wa Wilaya ya Mtwara, Dunstan Kyobya (wa pili kulia), akipokea moja ya meza kwa Meneja wa Benki ya NMB Kanda ya Kusini, Janeth Shango (wa pili kushoto), katika hafla ya kukabidhi msaada kwa shule tano katika wilaya hiyo juzi. Benki hiyo, imetoa madawati 120 kwa shule tatu za msingi na meza 100 pamoja na viti 100 kwa shule mbili za sekondari vyote vikiwa na thamani ya Sh. milioni 22. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Waziri Mkuu Majaliwa atembelea kampuni ya mabehewa SGR

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa, amesema ameridhishwa na maendeleo na kasi ya ujenzi wa mabehewa mapya kwa ajili Reli ya Kisasa (SGR) ya Shirika la Reli Tanzania yanayotengenezwa na kampuni ya Sung Shin Rolling Stock (SSRT), nchini Korea Kusini.

"Kati ya mabehewa 81 ambayo Tanzania inatengeneza kutoka kwenu, tayari 36 yamekamilika na yameshapelekwa nchini Tanzania na 45 yaliyobaki yanategemewa kukamilika Machi 2023. Mabehewa haya ni ya daraja la tatu na yatatoa huduma zote muhimu."

Waziri Mkuu aliyasema hayo jana alipotembelea kampuni ya SSRST inayotengeneza mabehewa na injini za treni nchini Korea Kusini.

Kadhalika, Waziri Mkuu amemkaribisha nchini Tanzania Rais wa kampuni hiyo, Gye Shul Park, kuwekeza kutokana na fursa mbalimbali zilizopo ikiwamo mpango wa serikali wa kuendelea kuiboresha sekta ya usafiri wa reli.

"Mna kiwanda kikubwa, teknolojia ya hali ya juu pamoja na utaalamu na watalaam kwenye eneo hili. Kwa sasa tuna mipango mikubwa ya kuendelea kuiboresha sekta hii ya usafiri wa reli, yapo maeneo tofauti kwenye mpango wa kuunganishwa na reli ya kisasa (SGR), nakukaribisha kuja kuwekeza kitu kama hiki Tanzania."

Aidha, alitembelea kituo cha Seamul Undong, ambacho ni taswira ya maendeleo ya Korea kupitia mpango wa kuviwezesha vijiji ambao unatekelezwa nchini Tanzania katika mkoa wa Morogoro (Pangawe) na Zanzibar.

Majaliwa alimshukuru Rais wa kituo hicho na kumuomba kuendelea kutoa ushirikiano ili kukuza zaidi mpango huo na kufikia maeneo mengi zaidi.

"Mfumo huu kwa sasa umekuwa wa kitaifa, ushirikishwaji wa wananchi ni mkubwa, sasa tunataka tuikuze zaidi, haya maeneo ya Morogoro na Zanzibar tunataka yawe mifano, kwenye utekelezaji wa eneo hili,"

Pia, Majaliwa alitembelea kituo cha ubunifu cha CEIC kilichopo katika mji wa Pangyo 2.

# Samia kuongoza mjadala nishati

**Na Pilly Kigome**

RAIS Samia Suluhu Hassan (pichani chini) anatarajiwa kuongoza mjadala wa kitaifa kuhusu matumizi ya nishati safi kwa ajili ya matumizi ya kupikia ili kuwa na mkakati wa kitaifa kuachana na nishati chafu ambayo ni hatari kwa afya za watu na mazingira.

Mkutano huo shirikishi unatarajiwa kufanyika Novemba mosi hadi 2, mwaka huu jijini Dar es Salaam.

Akihojiwa katika kipindi cha Breakfast cha EATV, Waziri wa Nishati, January Makamba, alisema mjadala huo utajumuisha wadau na jopo la wataalamu wa nishati mbadala na kutakuwa na mijadala mbalimbali ya sera, sheria, kanuni na maazimio ya kuhusiana na nishati.

Makamba alisema wapo katika mpango wa kuteketeza nishati chafu na kuhakikisha kila Mtanzania anatumia nishati safi mbadala kwa matumizi ya nyumbani.

Alisema watakuja na mpango wa ubunifu wa kununua nishati kwa kujipimia kadri uwezavyo kama inavyonunuliwa umeme wa LUKU, ili kila Mtanzania aweze kutumia nishati hiyo.

January alisema kuwa mpango huo utawezesha kila Mtanzania atamudu kutumia nishati hiyo kwa kuwa Watanzania wengi wana mazoea ya kununua kitu kidogo kidogo kulingana na hali za uchumi.

Alibainisha kuwa biashara ndogo ndogo za Sh.500 ndizo zinazopendwa na zinatoka kwa wingi katika maeneo mengi kwasababu ya kumudu gharama.

Alisema watu wengi majumbani wananunua nishati ya mkaa kuchemshia na kupikia maharagwe kuanzia Sh. 500 na kwamba nishati safi itaweza kununuliwa kadri ya uwezo wa mtu.

Kadhalika, Waziri Makamba alifafanua kuwa asilimia 72 ya nishati zote zinatumika majumbani kwa matumizi ya kupikia kutokana na umuhimu wake kwa ustawi wa jamii.

Tayari wameshapitisha mabomba katika mikoa ya Mtwara, Lindi na Pwani na hadi mwakani watatoa matokeo ya walipofikia.

Aliwatoa hofu Watanzania kuwa matumizi ya nishati gesi ni salama kwa kuwa teknolojia inawekwa kemikali maalum kwa ajili ya kuondoa mlipuko wakati wa matumizi.



HABARI KITAIFA

## RC awafunga kitanzi ma-DC, ma-DED

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

MKUU wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, ameingia mkataba wa utendaji kazi na wakuu wa wilaya wa kushughulikia suala la lishe bora huku akionya mkurugenzi wa halmashauri ambaye hatatenga Sh.1,000 katika bajeti kwa ajili ya kutekeleza mpango huo, atakuwa anatafuta ugomvi na serikali.

Alitoa agizo hilo jana wakati akitiliana saini mkataba na wakuu wa wilaya na wakurugenzi wa halmashauri ikiwa ni agizo la Rais Samia Suluhu Hassan alipokutana na wakuu wa mikoa jijini Dodoma. Rais aliwaagiza kujipanga na kuongeza jitihada za kuhamasisha utekelezaji wa shughuli za lishe bora.

"Jambo la lishe na afua za lishe tulipe kipaumbele cha kwanza. Tukifanikiwa kuifanya jamii yetu iwe na lishe bora hasa kwa watoto kuanzia umri wa mwaka mmoja hadi mitano, tutakuwa tumeweka jiwe la msingi kwenye kizazi kijacho," alisema.

Serukamba alisema madhara ya watoto kukua bila lishe ni makubwa zaidi kwa jamii ni vile tu hayaonekani haraka hivyo ni jukumu kwa waganga wakuu wa wilaya na wataalamu wanaohusika na lishe kuongeza juhudi kutoa elimu kwa wananchi wafahamu mpangilio wa vyakula.

"Tunaweza tukawa tunajiuliza kwa nini mitihani watu wanafeli sana tukadhani walimu hawafundishi. Lakini inaweza kuwa sababu mojawapo ni madhara ya kutopata lishe bora tena hasa kutoka kwa mama anapopata mimba," alisema.

Mkuu huyo wa mkoa alisema Rais Samia ndiye 'champion' wa jambo hilo, hivyo njia bora ya kumshukuru ni kumaliza tatizo la lishe ili kuzuia vifo vya wajawazito na watoto.

"Unaweza kukuta mtu nyumbani kwake ana kila kitu lakini anajua matunda ni kwa ajili ya kuuza tu si kula. Akikamua maziwa ni kuuza tu siyo kunywa. Viongozi wa lishe wa wilaya tusiishie kwenye makaratasi tu tuelimishe wananchi wajue mpangilio wa vyakula," alisema.

# Vijiji vitano na vitongoji 41 kuondolewa eneo la hifadhi

**Na Munir Shemweta,** MBARALI

SERIKALI imeamuru vijiji vitano na vitongoji 41 katika vijiji 14 pamoja na sehemu ndogo ya kitongoji cha Magwalisi kilichoko katika Mamlaka ya Mji mdogo wa Rujewa Wilaya ya mbarali, kuhamishwa ili kupisha hifadhi.

Pia vitongoji vitatu katika kijiji cha Lualaje wilayani Chunya, navyo vinatakiwa kuondoka kupisha hifadhi hiyo.

Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, alitoa kauli hiyo jana katika mkutano wa hadhara na wananchi wa eneo la Ubaruku, Mbarali wakati Kamati ya Mawaziri Wanane wa Wizara za Kisekta walipofanya ziara kwenye eneo la Mto Ruaha na Mnazi katika kijiji cha Mwanavala.

Uamuzi huo wa serikali unalenga kutunza na kulinda ardhioevu pamoja na vyanzo vya kupokea na kutunza maji yanayotiririka kutoka mito mbalimbali kuingia katika Mto Ruaha.

Alivitaja vijiji vitakavyoondoka kwa asilimia mia moja kuwa ni Luhanga, Madundasi, Msanga, Iyala na Kalambo vyenye idadi ya watu 21,252 na kusisitiza wa watu wa maeneo hayo wanatakiwa wasiwapo na usajili wa vijiji hivyo kufutwa.

"Katika zoezi hili wenye kulipwa fidia watalipwa na wale wasiostahili wataondoka kama walivyokuja. Lengo la serikali ni kuwa na urithi wa watu wote," alisema Dk. Mabula.

Pia Dk. Mabula alisema serikali imeridhia vijiji 15 vyenye ukubwa wa hekta 74,24.12 na ranchi ya Usangu ya Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO) kuendelea kubaki huku vijiji vyote vinavyopakana na hifadhi ya Ruaha kufanyiwa mpango wa matumizi ya ardhi.

Katika mapendekezo yake timu ya wataalamu ilipendekeza eneo la ranchi ya Usangu linalopendekezwa kuondolewa ndani ya hifadhi litumiwe na wafugaji watakaohamishwa kutoka kwenye vijiji na vitongoji vinavyopisha hifadhi.

Aidha, Tume ya Taifa ya Matumizi ya Ardhi kwa kushirikiana na halmashauri za wilaya za Mbarali na Chunya na wadau wengine wametakiwa kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi katika vijiji vyote vinavyopatikana na Hifadhi ya Taifa ya Ruaha.

Pia Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) imetakuwa kushirikiana na wadau wote muhimu katika suala la usajili wa vijiji na vitongoji ili kuepusha migogoro ya ardhi inayoweza kujitokeza.

Miongoni mwa wadau ni wizara zenye dhamana ya ardhi, maji, maliasili na utalii na Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira.

Uhifadhi wa Bonde la Usangu ulianza mwaka 1953 wakati eneo likijulikana kama pori tengefu la Utengule likiwa na ukubwa wa kilomita za mraba 500 kwa lengo la kuhifadhi bioanuwai katika ardhi oevu ya Ihefu.

Kutokana na uharibifu mkubwa wa mazingira na vyanzo vya maji uliofanyika miaka ya 1990 serikali iliamua kupandisha hadhi pori tengefu la utengule na kuwa Pori la Akiba la Usangu likiwa na ukubwa wa kilomita za mraba 4,148 kwa tangazo la serikali namba 436A la Julai 24, 1998.

Uharibifu ulisababisha serikali kuja na mkakati wa kitaifa wa hifadhi na mazingira ya ardhi oevu na vyanzo vya maji mwaka 2006 na kutaka bonde la Usangu kuwa kati ya maeneo ambayo wafugaji waliovamia mabonde na maeneo ya vyanzo vya maji wanaondolewa.



Mzee Bakari Muya (wa pili kulia) wa Kijiji cha Songe, Kata ya Songe, wilayani Kilindi, mkoani Tanga, akionyesha eneo ambalo uharibifu mkubwa wa mazingira umefanyika kutokana na ukataji miti kwenye Mlima wa Bokwa, wakati wajumbe wa kamati ya mila ya kata hiyo, walipotembelea kijijini hapo juzi. **PICHA: DEGE MASOLI**

# Bodi yatangaza mkakati kumaliza uhaba wa sukari

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI imeanza mikakati ya kuongeza uzalishaji wa sukari nchini ili kukabili uhaba wa bidhaa hiyo kwa kufanya upanuzi wa viwanda, kuhamasisha wakulima kulima kilimo cha miwa chenye tija na kuvutia wawekezaji.

Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Sukari Tanzania (SBT), Prof. Kenneth Bengesi, alibainisha hayo jana jijini hapo alipokuwa akitoa taarifa ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali za bodi hiyo kwa waandishi wa haabari.

Alisema kutokana na mikakati mbalimbali inayofanywa na bodi hiyo, wanatarajia ifikapo mwaka 2025/26 uzalishaji wa sukari utaongeza hadi kufikia tani 756,0000.

Prof. Bengesi alisema kutokana na hali nchi itakuwa na sukari ya kutosha, hivyo kutosheleza mahitaji ya ndani na kuuza nje ya nchi.

"Hivi sasa uzalishaji wa sukari nchini ni tani 380,000 na mahitaji ni tani 440,000 hivyo pengo ni tani 60,000. Ilani ya Chama Cha Mapinduzi inatutaka hadi ifikapo 2025 kuwa na uwezo wa kuzalisha tani 700,000 za sukari hivyo sisi tutakua tumevuka lengo hilo kwa kuzalisha tani 756,000," alisema Prof. Bengesi.

Alisema, hivi sasa viwanda vyote vinavyozalisha sukari nchini wanafanya upanuzi ili kuongeza uzalishaji kutoka kiasi ambacho kinazalishwa sasa.

"Viwanda vyetu vyote hivi sasa tunavifanyia upanuzi ili kuongeza uzalishaji lakini kuna kiwanda kipya cha Bagamoyo ambacho tayari kimeanza uzalishaji mwaka huu.

"Mwakani pia tutaongeza uzalishaji kwa kiwanda kipya cha Mkulazi mkoani Morogoro na kuzifanyia kazi changamoto zilizoko hivi sasa kwenye mashamba ya miwa makubwa na madogo ili kuzalisha miwa mingi na yenye ubora," alisema.

Pia alisema serikali ipo katika mipango ya kuanza uzalishaji wa sukari kwa ajili ya matumizi ya viwanda ambayo hivi sasa inayotumika nchini inaagizwa kutoka nje.

"Hatujawahi kuzalisha sukari kwa ajili ya matumizi ya viwanda hivyo inayotumika hivi sasa kiasi cha tani 205,000 yote inatoka nje, hivyo kufanya serikali kutumia Dola milioni 150 sawa na zaidi ya Sh. bilioni 300 kuagiza sukari ya matumizi ya nyumbani na hii kwa ajili ya viwanda.

"Kitendo hiki cha kutumia fedha nyingi kwa ajili ya kuagiza sukari nje ya nchi ni sawa na kuimarisha viwanda vya wenzako na ni aibu kuagiza sukari nje ya nchi," alisema.

Vilevile, alisema kama fedha hizo zinazotumika kuagiza sukari nje ya nchi zitatumika kuwekeza kwenye kuimarisha viwanda vya ndani kutasaidia kuondoa uhaba wa bidhaa hiyo, kuongeza ajira na kuimarisha uchumi wa nchi.

"Tunaishukuru serikali kwa kuweka mazingira rafiki kwa ajili ya wawekezaji wa ndani ambao wanaifanya nchi yetu tunapata wawekezaji wapya katika sekta ya sukari," alisisitiza.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Ni aibu walimu kufukuzwa kazi kwa utoro, ulevi

**TAARIFA** kutoka Wilaya ya Bagamoyo, mkoani Pwani kuwa kuna walimu 13 wamefukuzwa kazi kutokana na tuhuma za utoro, zinasikitisha na kutia aibu.

Taarifa zinaeleza kuwa kuna mashauri mengine matano yakiendelea kufanyiwa kazi kwa sababu hizo hizo.

Kati ya mashauri hayo manne yanadaiwa kutoka katika Halmashauri ya Chalinze na moja Bagamoyo ambayo yanahusisha tuhuma mbalimbali zikiwamo za kujihusisha na mapenzi na wanafunzi pamoja na ulevi uliokithiri.

Walimu ni tegemeo kubwa la kulea watoto na kuwafundisha tabia njema, baada ya wazazi walimu hao huwa ni walezi wa pili wanaotegemewa kuwalea watoto hao katika maadili mema.

Lakini kutokana na taarifa zilizotolewa na walimu waliopatwa na mkasa huo wanahusishwa na utoro, ulevi na kujihusisha kimapenzi na wanafunzi.

Kama shuleni ndiko wazazi wanaamini ni mahala salama pa watoto wao kufundishwa masomo na tabia njema, halafu watu wanaoaminiwa ndio wanao waharibu, sasa wapelekwe wapi?

Imeelezwa kuwa walimu hao wanadaiwa kufukuzwa katika kipindi cha miaka miwili kuanzia 2020 hadi Septemba 2022. Taarifa hizo za kufukuzwa kwa walimu hao zilitolewa mjini Bagamoyo na Katibu wa Tume ya Utumishi wilayani humo, Fedinand Ndomba, alipokuwa akizungumza kwenye mkutano wa wa Chama Cha Walimu.

Alisema, tabia hiyo ya utoro kwa baadhi ya walimu inachangia kushuka kwa kiwango cha ufaulu kwa wanafunzi Uamuzi wa kuwafuta kazi walimu hao umefanyika ili iwe fundisho kwa watumishi wengine wenye tabia kama hizo ambao wanasababisha kushuka kwa elimu.

Haishangazi kuona watoto wanasoma kutoka darasa la kwanza mpaka wanapomaliza darasa la saba baadhi yao hawajui kusoma wala kuandika.

Hiyo inatokana na watoto hao kushindwa kufuatiliwa na walimu wao na hata wazazi pia ni wa kulaumiwa kwa kushindwa kufuatilia nyendo za watoto wao na badala yake kuwaachia jukumu hilo walimu peke yao.

Katibu huyo alisema, kuna baadhi ya walimu pia hususani wa kiume wamekuwa wakijihusisha na mahusiano ya kimapenzi na wanafunzi, watoto ambao wamepewa dhamana ya kuwalea, kuwatunza, lakini wamebadilika na kuwaharibia maisha na ndoto zao.

Licha ya Mwenyekiti wa Chama cha Walimu Wilaya ya Bagamoyo, Hamis Kimeze, kuelezea vikwazo vinavyowakabili walimu ikiwamo kucheleweshwa kwa fedha za uhamisho pamoja na malipo kwa wastaafu, lakini kisiwe kigezo cha wao kufanya mambo yasiyofaa katika jamii na kuonyesha mifano mibaya.

Hata hivyo, Katibu Tawala Wilaya ya Bagamoyo Kasilda Mgeni, aliyemwakilisha Mkuu wa wilaya alikemea vitendo viovu vinavyofanywa na walimu na kusema kamwe hatovifumbia macho.


Akizungumzia tuhuma za baadhi ya walimu kujiingiza kwenye mapenzi na wanafunzi, alisema zitafanyiwa kazi na hatua zitachukuliwa kukomesha tabia hiyo.

Kauli aliyoitoa Katibu Tawala inatia matumaini ili kudhibiti vitendo viovu vinavyofanywa na baadhi ya walimu wasio na maadili ya kazi zao.

Vitendo vya udhalilishaji na ukatili dhidi ya watoto vinapigwa vita kila siku na walimu wanatakiwa kuwa mfano bora kwa watoto waliokabidhwa kuwalea badala ya kuwafundisha vitendo vibaya.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji:** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253 676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Figisu hizi zitakwamisha kupata viongozi mahiri

Na Sabato Kasika

**VYAMA** vya siasa ni nguzo muhimu katika ujenzi wa demokrasia ya uwakilishi. Tena vina majukumu mengi ikiwamo kuelimisha, kushawishi watu kushiriki michakato ya kisiasa, kutafuta wanachama pia kuandaa viongozi wa kila wakati.

Kwa mantiki hiyo, ili viweze kufanikiwa katika shughuli hizo, havina budi kujipanga kama taasisi, hasa kuanzia ngazi za msingi, kwani huko ndiko kwenye ushawishi mkubwa wa wanachama lakini kuwa na safu imara inayoviongoza.

Kwa Tanzania vyama viko katika muundo wa kuanzia ngazi ya mashina hadi taifa, ambapo tangu mfumo wa vyama vingi uliporejeshwa mwaka 1992, baadhi yake vimeendelea kuimarika na kusonga mbele.

Vyama ambavyo viko imara vimekuwa vikifanya uchaguzi wa viongozi wake kila muhula wa uchaguzi unapowadiwa ambapo uchaguzi huo huanzia ngazi ya chini hadi taifa ukihusisha pia jumuiya za vyama husika.

CCM ni miongoni mwa vyama hivyo, ambapo kwa sasa kinaendelea na uchaguzi wa viongozi wake kikiwa kinaelekea kwenye ngazi ya mkoa, huku kukidaiwa kuwa na 'figisu', katika baadhi ya uchaguzi.

'Figisu' hizo zinathibitishwa na Katibu Mkuu CCM, Daniel Changolo, akisema kwamba moja ya shida zinazowakabili ni kuwapo baadhi ya wanachama ndani ya chama hicho wanaotengeneza anachokiita miundombinu haramu ya kuwadhibiti watu wazuri kupata nafasi za uongozi.

Akiwa wilayani Kigamboni, anasema chama kina watu wazuri na bora wenye nia njema, ila wanatengenezewa mazingira ya kuwakosesha dhamana na kwamba kutokana na hilo, anatoa angalizo wanachama kuacha mara moja vitendo hivyo, na kwamba kwa idadi ya mikoa 32 iliyopo ni michache, ambayo chama kitapitia kila jina katika orodha ya walioomba kuchaguliwa.

Lengo la kufanya hivyo kwa mujibu wa maelezo yake ni kutazama maelezo binafsi na mengine na kujiridhisha kwa kila mtu, ili kupata viongozi ambao wanafanana na mazingira na wana dhamira ya kweli ya kuendeleza utumishi na uhai wa chama hicho.

Kiongozi huyo anafunguka kwamba, chama hicho kinataka viongozi bora na siyo bora viongozi, na kubainisha kuwa mwaka 2025 makada hawatachaguliwa kwa sababu wana sare nzuri ya chama.

Badala yake watachaguliwa kutokana na jinsi watakavyofanya kazi kwa kiwango chenye tija na kutatua shida za wananchi, na kwamba kila mtu achaguliwe kwa kuomba ridhaa mwenyewe na hakuna mtu anayefuatwa nyumbani achukue fomu ya kugombea.

Ingekuwa vyema kama makada wa CCM wangechukua hatua tangu zilipotokea figisu katika uchaguzi wa ngazi ya chini ambao kiongozi huyo aliamuru fomu zigawiwe upya kwenye baadhi ya maeneo.

Hatua hizo zilichukuliwa baada ya kubainika kuwapo kwa fitina na mazingira ya kuwanyima fomu za kuwania uongozi baadhi ya makada waliojitokeza kusaka uongozi na kusababisha malalamiko.

Mambo hayo yasingekuwa sehemu ya chama, kwani yanasababisha makada wenye uwezo wa kuongoza wakate tama, hali inayochangia kuchaguliwa wale wasio na sifa za kuongoza chama, badala yake wanakuwa na malengo binafsi.

Chongolo pia, analia na rushwa ndani ya chama hicho, na kwamba katika ngazi ya wilaya, walibaini baadhi ya watu kufanya rafu na kukiuka taratibu katika uchaguzi na kusababisha kufutwa kwa uchaguzi kwenye wilaya 21.

Kutokana na mazingira hayo, anabainisha kuwa macho yao yanatazama mchakato kwa karibu na hawatasita kuchukua hatua popote watakapoona kuna jambo lisilokuwa na heri kwenye chama hicho.

Ni jukumu la makada kuzingatia maelekezo ya viongozi wa chama, kwani uongozi unatumia muda mwingi kuimarisha chama, lakini wanajitokeza watu wanaotaka nafasi za uongozi kwa njia zisizo halali na kukwamisha jukumu hilo.

## HABARI KITAIFA




Meneja wa Bidhaa za Intaneti wa Tigo, Imelda Edward, akionyesha simu aina ya Redmi A1 Plus kutoka Xiaomi Tanzania, baada ya kuizindua jijini Dar es Salaam jana. Kulia ni Meneja Masoko Xiaomi, Alex Katagira. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TPA yachangia mil. 20/- ujenzi soko la Fumba

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

SHIRIKA la Bandari Tanzania (TPA), limechangia Sh. milioni 20 kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa soko la samaki Fumba uliokuwa unasuasua baada ya waliokuwa wameahidi kuchangia mwaka jana kutotimiza ahadi zao.

Akizungumza na vyombo vya habari jana mjini Unguja, Mwenyekiti wa Kamati ya Maandalizi ya Mashindano ya Zanzibar Blue Economy Club Championship 2022, Abdallah Majura, alisema msaada huo wameutumia kununua mabati, mbao, misumari, matofali, kulipa mafundi na vifaa vingine vyote vinavyohitajika.

Alisema TPA imetoa msaada huo kama mrejesho wa shukrani kwa Wazanzibari ambao wanaotumia bandari zao ama kwa kusafiria au kusafirisha mizigo kutoka Tanzania Bara kwenda Zanzibar.

"Nachukua nafasi hii kuishukuru TPA na Mkurugenzi Mkuu, Plasduce Mbossa, kwa msaada huu mkubwa kwani tulikuwa tumekwama kuendeleza ujenzi ule na ninaamini kama soko la samaki Fumba halitokamilika kabisa basi yatabakia mambo machache sana ambayo tutayakamilisha sisi wenyewe," alisema.

Majura ameeleza kusikitishwa na waliohidi kuchangia ujenzi huo na kutotimiza ahadi hiyo hali iliyofanya ujenzi wa soko hilo kusuasua na kumweka katika wakati mgumu kutokana na ahadi hizo kuzitangaza mbele ya Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, wakati wa maadhimisho ya mwaka mmoja Uwanja wa Amaan.

"Kuna hoteli moja kubwa ya Tanzania Bara na pia ina tawi hapa Zanzibar kupitia kwa msemaji wao waliahidi nao kutuchangia vifaa vya ujenzi wa soko la Fumba," alisema.

Alisema anasikitishwa na watu walitoa ahadi bila kuzitimiza mbele ya Rais Mwinyi na wengi waliamini imetolewa huku ujenzi ukiwa haukamiliki.

"Nitumie fursa hii kuwaambia wote wenye mashaka kuwa misaada ile tuliyoahidiwa haikutolewa," alisema Majura ambaye hata hivyo, hakuwataja kutokana na ahadi hiyo kutolewa kwa maneno na si kimaandishi.

"Kama ahadi zile zingetolewa kwa maandishi wallahi ningewaanika hapa," alisema.

Pia aliishukuru kampuni ya Bakhresa kupitia kampuni yake ya Fumba up Living Town ambayo imewahi kuwasaidia magari mawili ya kokoto na vifusi.

# Serikali kutekeleza miradi athari mabadiliko tabianchi

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Khamis Hamza Khamis, amesema serikali imechukua hatua mbalimbali ikiwamo kutekeleza miradi kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

Alisema hayo akizungumza kwa nyakati tofauti mkoani Songwe wakati wa ziara ya kamati ya mawaziri wanane wa wizara za kisekta inayoshughulikia migogoro ya matumizi ya ardhi katika vijiji.

Akizungumza na uongozi wa Mkoa wa Songwe, Khamis alisema serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais inatekeleza miradi hiyo ikiwamo uchimbaji visima katika maeneo yenye ukame ili wananchi waweze kupata maji kwa ajili ya matumizi.

Alisema pia serikali inatekeleza miradi ya kuwezesha upatikanaji wa majiko banifu ambayo yanasaidia kupunguza au kuondoa kabisa vitendo vya ukataji miti kwa ajili ya kuni na mkaa na kuhamasisha matumizi ya mkaa mbadala.


"Serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais imeanzisha na inasimamia Kampeni Kabambe ya Hifadhi na Usafi wa Mazingira, Kampeni ya Soma na Mti ambayo inahusisha wanafunzi wa shule na vyuo kupanda miti kwa lengo la kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi," alisema Khamis.

Akizungumza na wananchi wa kitongoji cha Ikanka kijiji cha Itumba wilayani Ileje alisisitiza wananchi kuendelea kupanda miti katika maeneo waliyoachiwa ili kutunza mazingira.

Naibu Waziri Chilo alisema kuwa miti mingi inaonekana imekatwa hali inayosababisha ukosefu wa mvua katika maeneo mbalimbali nchini.

Tayari kamati ya mawaziri wanane wa wizara za kisekta imeshatembelea mikoa 19 kati 26, kamati imeshapeleka mrejesho wa maamuzi ya baraza la mawaziri na inaendelea na ziara yake kwenye mikoa ya Mbeya, Iringa, Njombe na Ruvuma.

## KABWELA



# TANGAZO

**Tanzania Commercial Bank**
Growing stronger together

www.tcbbank.co.tz

## UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA(HESABU AMBAZO HAZIJAKAGULIWA)

Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014

### TANZANIA COMMERCIAL BANK

### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 30 SEPTEMBA, 2022

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Robo Mwaka /Mwaka wa sasa | Robo Mwaka/Mwaka uliopita |
|---|---|---|---|
| | | 30.09.2022 | 30.06.2022 |
| A. | MALI | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 56,072 | 62,114 |
| 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 33,436 | 48,661 |
| 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 105,901 | 105,096 |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 78,791 | 84,817 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | 499 | 253 |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | 0 | 0 |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | 0 | 0 |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | 0 | 0 |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 129,413 | 145,384 |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | 0 | 0 |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 821,878 | 770,613 |
| 12 | Mali Nyingine | 43,904 | 46,371 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | 0 | 0 |
| 14 | Akaunti za udhamini | 0 | 0 |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 21,075 | 20,999 |
| **16** | **JUMLA YA MALI** | **1,290,968** | **1,284,309** |
| | **DHIMA** | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 0 | 0 |
| 18 | Amana za Wateja | 834,456 | 835,519 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | 0 | 0 |
| 20 | Amana Maalumu | 147,846 | 172,704 |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | 6,238 | 3,618 |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | -0 | -0 |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 20,855 | 20,896 |
| 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | 0 | 0 |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | 0 | 0 |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | 2,723 | 2,504 |
| 27 | Dhima Nyingine | 25,644 | 25,438 |
| 28 | Madeni | 134,672 | 106,945 |
| **29** | **JUMLA YA DHIMA** | **1,172,434** | **1,167,625** |
| **30** | **MALI/(DHIMA) HALISI** ***(16 kutoa 29)*** | **118,534** | **116,684** |
| C. | **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 31,372 | 28,072 |
| 32 | Akiba ya Mtaji | 0 | 0 |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | 71,792 | 73,955 |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 5,677 | 3,719 |
| 35 | Akaunti Nyingine za Mtaji | 9,694 | 10,939 |
| 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | 0 | 0 |
| **37** | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **118,534** | **116,684** |
| 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | 108,694 | 207,546 |
| 39 | Mikopo Chechefu | 70,393 | 72,052 |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 13,790 | 11,275 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | 1,761 | 945 |
| D. | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 9.18% | 9.09% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 8.36% | 9.15% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 85.76% | 78.12% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 63.66% | 60.00% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 81.89% | 79.51% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | -2.57% | 7.47% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | 0.52% | 6.00% |

## TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA ROBO /MWAKA ULIOISHIA TAREHE 30 SEPTEMBA, 2022

(Kiasi kwa shilingi milioni}

| | Robo Mwaka ya sasa | Robo Mwaka iliyopita | Limbikizo la Mwaka wa sasa | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) |
|---|---|---|---|---|
| | 30-Sep-22 | 30-Jun-22 | 30-Sep-22 | 30-Sep-21 |
| **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za** | | | | |
| Mapato/(Hasara) Halisi | 3,479 | 3,360 | 10,691 | 15,093 |
| Marekebisho kwa Ajili ya: | | | | |
| - Hasara Katika Mali | 6,878 | 5,964 | 18,814 | 17,496 |
| - Badiliko Halisi Katika Mikopo | (51,265) | (41,898) | (103,278) | (64,175) |
| - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | - | - | - | - |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana | (25,921) | 70,112 | 74,187 | 119,591 |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi | - | - | - | - |
| - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | 3,004 | (2,102) | 4,648 | (9,313) |
| -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | 2,468 | 2,669 | (4,997) | (4,812) |
| - Kodi Iliyolipwa | (1,521) | (1,521) | (5,014) | (6,690) |
| - Mengineyo (bainisha) | 5,261 | (21,901) | (47,956) | (95,484) |
| ***Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji*** | **(57,617)** | **14,684** | **(52,906)** | **(28,294)** |
| **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za** | | | | |
| Gawio Lililopokewa | - | - | - | - |
| Ununuzi wa Mali za Kudumu | (279) | (933) | (2,193) | (4,824) |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | - | - | - |
| Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa | - | - | - | - |
| Mengineyo (bainisha) | - | - | - | - |
| *Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji* | **(279)** | **(933)** | **(2,193)** | **(4,824)** |
| **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | | | | |
| Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - | - | - |
| Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | - | - | - |
| Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | - | - | - | - |
| Mengineyo (bainisha) | (2,366) | (1,000) | (5,164) | (5,432) |
| **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha** | ***(2,366)*** | ***(1,000)*** | ***(5,164)*** | ***(5,432)*** |
| **Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | | | | |
| Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | (60,263) | 12,750 | (60,263) | (38,550) |
| Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | **157,687** | **144,937** | **157,687** | **173,727** |
| Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 97,424 | 157,687 | 97,424 | 135,177 |

## TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA TAREHE 30 SEPTEMBA, 2022

(Kiasi kwa shilingi milioni}

| | Robo ya Mwaka sasa | Robo ya mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) | Limbikizo la Mwaka wa sasa | Limbikizo la Mwaka Linganishi (Mwaka Uliopita) |
|---|---|---|---|---|
| | 30-Sep-22 | 30-Sep-21 | 30-Sep-22 | 30-Sep-21 |
| 1 Mapato ya Riba | 34,319 | 33,720 | 103,672 | 99,075 |
| 2 Gharama za Riba | (12,988) | (9,762) | (35,563) | (29,008) |
| 3 Mapato Halisi ya Riba (1kutoa 2) | **21,331** | **23,957** | **68,109** | **70,067** |
| 4 Madeni Viza Yaliyofutwa | (548) | (72) | (604) | (157) |
| 5 Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | (3,435) | (3,398) | (10,349) | (10,339) |
| 6 **Mapato Yasiyo ya Riba**: | **10,632** | **6,559** | **26,846** | **25,071** |
| 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 1,344 | 1,338 | 3,965 | 3,925 |
| 6.2 Ada na Kamisheni | 4,903 | 4,615 | 13,774 | 13,329 |
| 6.3 Gawio | - | - | - | - |
| 6.4 Mapato Mengine | 4,384 | 606 | 9,107 | 7,817 |
| 7 **Gharama Zisizo za Riba:** | **(24,500)** | **(23,989)** | **(73,312)** | **(69,549)** |
| 7.1 Mishahara na Mafao | 11,804 | 11,958 | 36,296 | 34,417 |
| 7.2 Ada na Kamisheni | 2,125 | 933 | 5,497 | 3,355 |
| 7.3 Gharama Nyingine | 10,572 | 11,098 | 31,518 | 31,778 |
| 8 **Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **3,479** | **3,057** | **10,691** | **15,093** |
| 9 Tengo la Kodi ya Mapato | 1,521 | 2,189 | 5,014 | 6,690 |
| 10 **Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **1,958** | **869** | **5,677** | **8,402** |
| 11 **Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha)** | - | - | - | - |
| 12 **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **1,958** | **869** | **5,677** | **8,402** |
| 13 Idadi ya Waajiriwa | 1,089 | 1,103 | 1,089 | 1,103 |
| 14 Mapato kwa Hisa | 62 | 31 | 181 | 299 |
| 15 **Idadi ya Matawi** | 48 | 47 | 48 | 47 |
| **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | | | |
| (i) Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | 0.15% | 0.08% | 0.46% | 0.77% |
| (ii) Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | 1.66% | 0.77% | 4.88% | 7.71% |
| (iii) Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 54.51% | 59.56% | 56.17% | 56.02% |
| (iv) Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 2.04% | 2.64% | 6.74% | 8.12% |

**Tarakimu za wastani zitakokotolewa kwa kujumlisha salio la mwisho kwa miezi inayohusika katika kipindi na kugawanya kwa idadi ya miezi katika kipindi hicho.**

## TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA TAREHE 30 SEPTEMBA, 2022

(Kiasi kwa shilingi milioni}

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | Mengineyo | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **28,072** | - | **75,447** | **(0)** | **0** | **9,694** | **113,213** |
| Mabadiliko ya mpito ya IFRS 9 | - | - | - | | | | - |
| Hamisho kwenda hifadhi ya kisheria | - | - | **11** | - | - | | **11** |
| Faida ya mwaka | - | - | - | - | - | 5,677 | **5,677** |
| Mapato mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| Hifadhi ya jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Hamisho kwenda/kutoka mapato yaliyohifadhiwa | **3,667** | - | (3,667) | - | - | - | **(0)** |
| Mengineyo | **(367)** | - | - | - | | - | **(367)** |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **31,372** | - | **71,791** | **(0)** | **0** | **15,371** | **118,534** |
| **Mwaka uliopita** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **28,072** | - | **66,533** | **(0)** | **0** | **9,694** | **104,299** |
| Hamisho kutoka hifadhi ya udhibiti | - | - | - | - | - | - | - |
| Faida ya mwaka | - | - | 9,167 | - | - | - | **9,167** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | (253) | - | - | - | **(253)** |
| Hisa za ziada | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la ziada ya jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Hasara ya sasa ya manufaa yaliyofafanuliwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Kurudishiwa Gawio lililosimamishwa | | | - | | | | - |
| Mengeineyo | | | | | | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **28,072** | - | **75,447** | **(0)** | **0** | **9,694** | **113,213** |

**BAADHI YA MAELEZO KWA ROBO MWAKA INAYOISHIA 30 SEPTEMBA, 2022**

Benki ililipa faini ya shilingi 98,000.00 katika kipindi cha robo mwaka kwa kushindwa kuzingatia miongozo ya COU

Katika kuandaa taarifa hizi za fedha, sera za uandaaji ni zilezile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita (kama kulikua na mabadiliko katika sera za uandaaji taarifa za fedha katika kipindi cha robo mwaka ya/mwaka wa sasa, mabadiliko yaelezwe kwa mujibu wa IAS 34 na IAS 8)

| *Jina na Cheo* | *Saini* | *Tarehe* |
|---|---|---|
| **SABASABA K. MOSHINGI** (Ofisa Mtendaji Mkuu) | Imesainiwa | **21.10.2022** |
| **REGINA E. SEMAKAFU** (Mkuu wa Fedha) | Imesainiwa | **21.10.2022** |
| **SOSTHENES F. NYENYEMBE** (Mkaguzi Mkuu wa Ndani) | Imesainiwa | **21.10.2022** |

Sisi tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi,tunathibitisha usahihi wa Taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathimini taarifa hizi,na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na viwango vya kimataifa vya uwasilishaji wa Taarifa za fedha na matakwa ya sheria ya Benki na Taasisi za fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi

| | | |
|---|---|---|
| **DR. EDMUND B. MNDOLWA** Mwenyekiti wa Bodi | Imesainiwa | **21.10.2022** |
| **MS. ANNE C. MBUGHUNI** Mjumbe wa Bodi | Imesainiwa | **21.10.2022** |

tcbbank

Head Office, Millenium Tower II, 10th Floor, Kijitonyama Opp. Makumbusho Village,
P.O. Box 9300, Dar Es Salaam | Telephone; +255 22 216 2940
E-mail: info@tcbbank.co.tz | www.tcbbank.co.tz | Customer Care: +255 787 669977 | +255 788 767 683 | +255 658 767 683

217113802

TANGAZO

Tanzania Commercial Bank
Growing stronger together

# MINIMUM DISCLOSURE OF RATES AND CHARGES 2022

*All charges are VAT exclusive.

| PRODUCT | MINIMUM OPENING BALANCE | | MONTHLY MAINTANCE FEES | | MINIMUM OPERATING BALANCE | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | TZS | USD | TZS | USD | TZS | USD |
| Call account | 100,000.00 | 100.00 | 10,000.00 | 5.00 | 100,000.00 | 100.00 |
| Business Current Account | 100,000.00 | 100.00 | 20,000.00 | 20.00 | 100,000.00 | 100.00 |
| Personal current Account | 100,000.00 | 100.00 | 7,000.00 | 5.00 | 50,000.00 | 100.00 |
| Vikundi Current Account | 100,000.00 | N/A | FREE | N/A | 50,000.00 | N/A |
| Quick Account | 20,000.00 | 10.00 | 1,800.00 | 0.86 | 20,000.00 | 10.00 |
| Salary Account | FREE | N/A | 1,800.00 | N/A | 0 | N/A |
| Tabasamu Individual | 10,000.00 | N/A | FREE | N/A | 10,000.00 | N/A |
| Tabasamu Group Account | 50,000.00 | N/A | FREE | FREE | 50,000.00 | N/A |
| Platinum Account | 15,000.00 | N/A | FREE | N/A | 5,000 | N/A |
| Minor Account | 20,000.00 | N/A | FREE | N/A | 20,000 | N/A |
| Group Account | FREE | N/A | FREE | N/A | 0 | N/A |
| Scout Minor Account | 10,000.00 | N/A | FREE | N/A | 10,000 | N/A |
| Scout Account | 30,000.00 | N/A | FREE | N/A | 30,000 | N/A |
| Wavuvi Account | 10,000.00 | N/A | 1,800.00 | N/A | 10,000 | N/A |
| Wadu Account | 20,000.00 | N/A | FREE | FREE | 20,000 | N/A |
| Kivulini Account | FREE | N/A | 700.00 | N/A | 1,500.00 | N/A |

## CASH SERVICES

| DESCRIPTION | BANDS | CHARGES |
|---|---|---|
| Cash deposit | | FREE |
| | Withdrawal below 400,000 | 1,800.00 |
| | Withdrawal 400,001 - 800,000 | 3,000.00 |
| | Withdrawal from 800,001 - 1,200,000 | 4,400.00 |
| | Withdrawal from 1,200,001 - 10,000,000 | 5,000.00 |
| | Withdrawal from 10,000,001 - 50,000,000 | 6,000.00 |
| | Withdrawal from 50,000,001 -100,000,000 | 14,000.00 |
| Cash withdrawal TZS | Withdrawal from above 100,000,000 | 0.12% max 170,000 |
| | Withdrawal below 50 | 1.00 |
| | Withdrawal from 51-1,000 | 2.50 |
| | Withdrawal from 1,000 -2,250 | 5.00 |
| | Withdrawal from 2,251-5,000 | 15.00 |
| Cash withdrawal USD | Withdrawal Above 5,000 | 0.25% |
| **BANK STATEMENT** | **TZS** | **USD** |
| Balance enquiry over the counter | 1000.00 | USD equivalent |
| Statement per page | 2,000.00 | USD equivalent |
| **CHEQUE SERVICE** | **TZS** | **USD** |
| Cheque book per leaf | 500.00 | USD equivalent |
| Cheque clearing | FREE | FREE |
| Unpaid cheque/insufficient fund | 150,000.00 | USD equivalent |
| Stop Payment order | 30,000.00per leaf Max 300,000.00 | USD equivalent |

## DORMANT ACCOUNT

| | | |
|---|---|---|
| Dormant account fee | FREE | |
| Re-activation | FREE | |

| ACCOUNT CLOSURE | TZS | USD |
|---|---|---|
| Closing account fee | 13,000.00 | USD equivalent |

| OTHER SERVICES | TZS | USD |
|---|---|---|
| Government Securities transaction Handling fees | 50,000.00 | N/A |
| Confirmation to Auditors | 45,000.00 | USD equivalent |
| Introduction letter/Confirmation to Embassies | 45,000.00 | USD equivalent |

| FUND TRANSFER SERVICE | TZS | USD |
|---|---|---|
| TISS-Outward | 10,000.00 | USD Equivalent |
| TISS-Inward | FREE | FREE |
| EFT-Outward | 2,000.00 | N/A |
| EFT-Inhouse | 1,500.00 | N/A |
| TT-Outward | N/A | 55 |
| TT-Inward | N/A | 5 |
| Internal Transfer | FREE | FREE |
| Standing Order - Within the Bank | FREE | FREE |
| Standing Order - To other Bank | 13,000.00 | USD Equivalent |
| Salary Handling-Cheque list | 1,000.00 | USD Equivalent |

## AGENT BANKING SERVICE

| DESCRIPTION | BANDS | CHARGES |
|---|---|---|
| Deposit | PER TRANSACTION | FREE |
| Withdrawal | 0.01 - 10,000.00 | 800.00 |
| | 10,000.01 - 20,000.00 | 1,250.00 |
| | 20,000.01 - 50,000.00 | 1,500.00 |
| | 50,000.01 - 100,000.00 | 2,250.00 |
| | 100,000.01 - 200,000.00 | 2,750.00 |
| | 200,000.01 - 300,000.00 | 4,200.00 |
| | 300,000.01 - 400,000.00 | 5,500.00 |
| | 400,000.01 - 500,000.00 | 6,000.00 |
| | 500,000.01 - 700,000.00 | 6,500.00 |
| | 700,000.01 - 1,000,000.00 | 7,500.00 |
| | 1,000,000.01 - 1,500,000.00 | 8,500.00 |
| | 1,500,000.01 - 2,000,000.00 | 9,000.00 |
| | 2,000,000.01 - 3,000, 000.00 | 10,000.00 |
| Balance Enquiry | | 100.00 |
| Mini Bank Statement | | 200.00 |

## POPOTE ATM SERVICE

| ACTIVITY | BAND[TZS] | New Charge (TZS) |
|---|---|---|
| 1. ATM Cash Withdraw | 1,000 – 99,000 | 1,500 |
| | 100,000 – 400,000 | 1,700 |
| 2. Interbank transfer on ATM | 1 – 99,999 | 1,300 |
| | 100,000 - 199,999 | 1,700 |
| | 200,000 - 299,999 | 1,700 |
| | 300,000 - 399,999 | 1,700 |
| | 400,000 - 499,999 | 2,500 |
| | 500,000 - 599,999 | 3,000 |
| | 600,000 - 699,999 | 3,500 |
| | 700,000 - 999,999 | 4,000 |
| | 1,000,000 - 1,999,999 | 5,000 |
| | 2,000,000 - 2,999,999 | 6,000 |
| | 3,000,000 - 3,999,999 | 7,000 |
| | 4,000,000 - 4,000,000 | 8,000 |
| 3. Intra-Bank Transfer on ATM | Any Amount | 1,000 |
| 4. Balance Inquiry | NA | 400 |
| 5. Mini Statement | NA | 400 |
| 6. Popote ATM card issuance /Replacement | N/A | 15,000 |
| 7. PIN Re-issue | N/A | 1,000 |
| 8. Collection of ATM card at non-domicileBranch | N/A | 6,500 |
| 9. Uncollected and Destroyed ATM Card | N/A | |
| 10. Card Maintainance | N/A | 5,000 |
| 11. Failed Transaction Due to insufficient fund | | 9,00 |

## POPOTE MOBILE BANKING / INTERNET BANKING

| DESCRIPTION | BANDS | CHARGES |
|---|---|---|
| Registration | | FREE |
| | 500 -10,000.00 | 850.00 |
| | 10,000.01 - 50,000.00 | 1,200.00 |
| | 50,000.01 - 100,000.00 | 1,500.00 |
| | 100,000.01 - 250,000.00 | 2,800.00 |
| | 250,000.01 - 500,000.00 | 4,600.00 |
| | 500,000.01 - 750,000.00 | 7,500.00 |
| Transfer Bank to MNO | 750,000.01 - 1,000,000.00 | 10,000.00 |
| From MNO to Bank (Deposit) | | FREE |

## LENDING INTEREST RATES AND OTHER CHARGES

| LOANS | CATEGORY | RATE |
|---|---|---|
| Consumer loans | Consumer loan Admnistartion fee | 1.5% of the Approved Loan Minimum TZS 20,000.00 |
| Wastaafu Loans | Loan Application fee | TZS 20,000.00 |
| | Loan Administration fee | 1.5% Minimum TZS 20,000.00 Maximum TZS 150,000.00 |
| Other Charges On individual Micro Credit | MIC loan Application fee | TZS 150,000.00 |
| | MIC loan processing/Administration fee | 1.5% Minimum TZS 150,000.00 |
| Charges on Business Loan | Loan Applicationfee for Business Loans | TZS 200,000.00 |
| | Loan Administration fee- Business and Personal loans | 2% of the Approved Amount |

| LETTER OF CREDIT ISSUED (IMPORT LCS) | CHARGES |
|---|---|
| Charges on Draft LC | USD 60 |
| LC commission per quarter | 1% per quarter or part thereof. Min USD 150 or foreign eqv |
| LC commission per quarter with cash cover | 1% per quarter or part thereof. Min USD 150 or foreign eqv |
| Amendment fee per quarter on the tenor extended or amount increased | 1% perquarter Min USD 150 or foreign eqv |
| Other amendments | USD equiv 60 or foreign eqv |
| Discrepancy fee per pack | USD equiv 60 or foreign eqv |
| Documen examination Fee per pack | 0 |
| Cancellation charges | USD 60 or foreign eqv. |
| Swift charges | USD 60 or foreign eqv. |
| Non-Payment of Bills Due Date | 0 |
| Expire unutlised Letters of Credit | 0 |

| LETTER OF CREDIT ISSUED BY OTHER BANKS (EXPORT LCS) | CHARGES |
|---|---|
| Advising Fee or commission | USD 200 or foreign eqv |
| Bank client for LC available with us | USD 150 or foreign eqv |
| Client for LC available with other Bnaks | N/A |
| Non Bank Customer | USD 250 or foreign eqv |
| Confirmation Fee(per quarter)USD eqv | 1% per quarter and part thereof,Min USD 250 or foreign eqv |
| Amendment advising Fee | USD 120 or foreign eqv |
| Cancellation Fee | USD 60 or foreign eqv |
| Transfer Fee (per quarter) | 0.75% per quarter, Min USD 250 or foreign eqv |
| Courier services | Actual costs plus USD 10 or foreign eqv |
| Swift charges | USD 60 or foreign eqv |
| Document Handling commission | N/A |
| Discrepancy Fee per document | N/A |

| LETTER OF CREDIT ISSUED BY OTHER BANKS (EXPORT LCS) | CHARGES |
|---|---|
| Commission on LC discounting/Negotiation | 0.75% Min USD 200 Max 600 or foreign eqv |
| Negotiation Bills under an Export Letter of Credit (Discounting Bills) | N/A |
| Extension - Commission for unconfirmed LC | 0.5% per quarter and part thereof, Min of USD 200 or foreign eqv |
| Extension - Commission for confirmed LC | 1% per quarter and part thereof Min. of USD 100 or foreign eqv |

| COLLECTION (DOCUMENTARY CREDIT) | CHARGES |
|---|---|
| Documents processing | 1% Min USD 15 Max 200 |
| Courier services | Actual cost plus USD 10 |
| **Outward Documentary bills for collection (OFBC)** | |
| Document handling commission | 0.5% Min USD 150 Max USD 350 or foreign eqv |
| Courier services | Actual cost plus USD 10 or foreign eqv |
| Chaser/Tracer | USD 60 or foreign eqv. |
| **Inward Documentary bills for collection** | |
| Bill discounted handling commission | 0.5% Min USD 150 Max USD 600 or foreign eqv |
| Document returned unpaid or unaccepted | 0 |
| For each amendment of previous instructions | 0 |
| Every presentation or reminder protest fee | 0 |
| Delivery of documents for non - customers | USD 250 or foreign eqv |
| Swift charges | USD 60 or foreign eqv. |
| Payment commission for documents value greater than USD 50,000 | 0 |
| Payment commission for documents value less than USD 50,000 | 0 |
| Avalisation commission per quarter or part thereof | 1.20% |
| Risk margin on acceptance (per quarter) | 1.20% |

## GUARANTEE

| COLLECTION (DOCUMENTARY CREDIT) | CHARGES |
|---|---|
| Issuance or confirmation of foreign Currency guarantee Commission(per quarter) | 1.0% per quarter or part thereof Min TZS 250,000 or USD 110, foreign eqv |
| Issuance of guarantee commission (per quarter) for Bid bond | 1.0% Bid bond Issuance part thereof Min TZS 150,000 of USD 64 foreign eqv |
| Issuance of guarantee commission (per quarter) for Perfomance,Advance Payment and any other bank guarantees | 1.0% per quarter or part thereof Min TZS 350,000 or USD 150, foreign eqv |
| Amendment fee per quarter on the tenor extended or amount increased | 1.0% per quarter or part thereof Min TZS 250,000 or USD 110, foreign eqv |
| Text amendment fee | TZS 150,000 or USD 64 or foreign eqv. |
| Other amendments | USD 60 or foreign eqv |
| Guarantee advisisng fee (from other Banks) | USD 200 or foreign eqv |
| Courier services (Direct delivery to Beneficiary) | 0 |
| Open ended guarantees(charged per annum) | 3%p.a |
| Cancellation | TZS 150,000 or USD 64 or foreign eqv. |

## POPOTE VISA CARD

| DESCRIPTION | CHARGES |
|---|---|
| Popote VISA issuance/Replacement | 20,000.00 |
| ATM Withdrawal - Domestic | 3,350.00 |
| Balance Inquiry - Domestic | 1,000.00 |
| ATM Withdrawal - International | 5,500.00 |
| Balance Inquiry - International | 2,000.00 |


TCB BANK POPOTE VISA CARD

Accepted at all Visa outlets Point of Sales (POS) and Online platforms worldwide




Apply for your Popote card at your nearest TCB Branch/ Online!

Tanzania Commercial Bank
Growing stronger together

VISA

Huduma kwa Wateja: +255 22 787 669977, +255 788767683, +255 658 767683, Namba bila Malipo: 0800110160 Website: www.tcbbank.co.tz


Makao Makuu, PSSSF, Millenium Towers II, Barabara ya Bagamoyo, S.L.P. 9300, Dar es Salaam, Tanzania. Simu +255 22 2162940, Faksi +255 22 2114814

Huduma kwa Wateja: +255 22 787 669977, +255 788767683, +255 658 767683 Namba bila Malipo: 0800110160

# Waziri ataka usimamizi wa miradi ya umma

**Na Mwandishi Wetu, MUFINDI**

NAIBU Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Deogratius Ndejembi, amewataka watumishi wa umma kuwajibikaji kikamilifu katika kusimamia miradi ya maendeleo inayotekelezwa ikiwamo ujenzi wa madarasa, zahanati, vituo vya afya na miundombinu ya barabara na reli.

Ndejembi alitoa wito huo jana alipokuwa akizungumza na watumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi, akiwa katika ziara ya kikazi yenye lengo la kutatua changamoto zinazowakabili na kuhimiza uwajibikaji.

"Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan amekuwa akitoa fedha nyingi kutekeleza miradi ya maendeleo kwenye halmashauri zote nchini, hivyo ni lazima tuwajibike kikamilifu katika kuisimamia miradi yote ili ikamilike kwa wakati na kuwanufaisha wananchi," alisema.

Pia aliwataka kuwajibika kwa wananchi kwa kutoa huduma bora ili kuondoa dhana potofu iliyojengeka katika jamii kuwa watumishi wa umma hawawajibiki ipasavyo kama ilivyo katika sekta binafsi.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi, Kenny Shilumba, alimshukuru Ndejembi kwa kuhimiza uwajibikaji, kutoa ufafanuzi wa masuala mbalimbali ya kiutumishi na kutatua kero mbalimbali zilizokuwa zikiwakabili watumishi katika halmashauri hiyo.

Mtumishi wa halmashauri hiyo, Tunu Kombo, kwa niaba ya watumishi wenzake, alimshukuru Naibu Waziri kwa kuwapatia elimu kuhusiana na masuala mbalimbali ya kiutumishi ikiwa ni pamoja na kutatua kero zilizokuwa zikiwakabili kwa muda mrefu.

Sambamba na hilo, Komba alimshukuru Rais Samia kwa kuteua viongozi mahiri wenye kujituma katika kusikiliza na kutatua changamoto zinazowakabili watumishi wa umma nchini.

Naibu Waziri Ndejembi ameanza ziara ya kikazi mkoani Iringa kwa kuhimiza uwajibikaji kwa watumishi wa umma walioko katika Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi.



Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, akizungumza na wananchi wa Kitongoji cha Ikanka, Kijiji cha Itumba, wilayani Ileje jana wakati Kamati ya Mawaziri Nane wa Wizara za Kisekta inayoshughulikia migogoro ya matumizi ya ardhi katika vijiji 975 ilipotembelea kitongoji hicho. **PICHA: WANMM**

# Waruhusiwa kuishi ndani hifadhi ya msitu

**Na Munir Shemweta, ILEJE**

RAIS Samia Suluhu Hassan ameridhia wananchi wa Kitongoji cha Ikanka katika Kijiji cha Itumba, Ileje mkoani Songwe, kuendelea kuishi sehemu ya eneo la Hifadhi ya Msitu wa Ileje Range.

Uamuzi huo unakifanya Kitongoji cha Nkanka sasa kutambuliwe ndani ya hifadhi ya msitu huo kutokana na kaya 105 zenye makazi kwenye eneo hilo.

Aidha, uamuzi huo pia umegusia mgogoro wa matumizi ya ardhi katika Hifadhi za Msitu wa Mugombezi ulioko Kijiji cha Nyimbili katika kata ya Mlowo, Ilengo Mbozi mkoani Songwe.

Akitangaza juzi uamuzi huo, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, alisema sehemu ya eneo la hifadhi ekari 278 zitamegwa na kubaki kwa wananchi kutoka ekari 414 kwa kuwa eneo hilo limeendelezwa kwa shughuli za kilimo, makazi na kuwekwa huduma za kijamii kama uwanja wa mpira na pampu ya maji.

Waziri Mabula amewatahadharisha wananchi walioruhusiwa kuendelea eneo hilo kutojaribu kuongeza maeneo wanayoishi huku akisema baada ya utatuzi wa migogoro ya matumizi ya ardhi kukamilika, maeneo yote ya hifadhi yanatakiwa kulindwa.

Dk. Mabula wakati akizungumza na wananchi wa Kijiji cha Ikanka akiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Mawaziri Wanane wa Wizara za Kisekta, aliagiza shughuli za kilimo pembezoni mwa vyanzo vya maji nazo zisitishwe ili kunusuru vyanzo hivyo ndani ya hifadhi.

Mawaziri walioambatana na Dk. Mabula walisisitiza umuhimu wa kutunzwa mazingira pamoja na kuandaliwa mipango ya matumizi ya ardhi kwa maeneo yote yalivomegwa.

Naibu Waziri wa Maji, Maryprisca Mahundi, aliwaambia wananchi wa Kitongoji cha Ikanka kuwa baada ya kuruhusiwa kuendelea kuishi eneo hilo, wahakikishe wanatunza na kuhifadhi vyanzo vya maji na kuepuka shughuli zozote zitakazosababisha uharibifu wa vyanzo hivyo.

Khamis Hamza Chilo, Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira, alisisitiza suala la wananchi kupanda miti katika maeneo waliyoachiwa ili kutunza mazingira.

Naye Naibu Waziri wa Kilimo, Anthony Mavunde, na Naibu Waziri Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, walieleza umuhimu wa maeneo yaliyomegwa kupangiwa matumizi ya ardhi na kupimwa sambamba na kuainishwa maeneo ya kilimo, mifugo na uvuvi ili kuepuka kutengeneza migogoro mingine.

Katika hatua nyingine, Waziri Mabula aliwataka viongozi wa mikoa na wilaya kuhakikisha wanatekeleza uamuzi wa Baraza la Mawaziri kuhusiana na migogoro ya matumizi ya ardhi katika vijiji 975 kwa kuweka mpango wa utekelezaji hasa kwa yale maeneo ambayo hayana tathmini ya kina.

Katika uamuzi wake, Baraza la Mawaziri liliamua vijiji 920 kati ya 975 vyenye migogoro katika ranchi, mapori ya akiba, mashamba na vyanzo vya maji kubaki ingawa baadhi ya vijiji vitahusisha marekebisho ya mipaka kwa njia shirikishi.

Hata hivyo, vijiji 55 kati ya 975 vinaendelea kufanyiwa tathmini na kamati na wataalamu wake kutoa mapendekezo kwa ajili ya maamuzi.

# Jela miaka miwili kuua bila kukusudia

**Na Grace Gurisha**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, imemhukumu Mkazi wa Dar es Salaam, Jacob Masaka (57), kifungo cha miaka miwili jela, baada ya kupatikana na hatia ya kumuua Baraka Thomas bila kukusudia.

Hukumu hiyo ilitolewa juzi na Hakimu Mkazi Mkuu Franco Kiswaga, baada ya mshtakiwa kukiri kosa la kuua bila kukusudia na mahakama kumtia hatiani. Kabla ya hukumu hiyo, mshtakiwa alikuwa amekaa mahabusu miaka minne na miezi tisa.

Hakimu Kiswaga alisema amepitia shufaa ya mshtakiwa kwamba haina ubishi kuwa Masaka ni mkosaji wa mara ya kwanza na pia amekaa mahabusu muda mrefu na kwamba anastahili nafuu ya mahakama.

Alisema mshtakiwa atatumikia kifungo cha miaka miwili jela, lakini akiwa gerezani anaweza kuomba adhabu mbadala.

Kabla ya adhabu hiyo kutolewa, Wakili wa Serikali Sabina Nduguru aliiomba mahakama itoe kauli kwa mshtakiwa ili iwe fundisho kwake na kwa wengine na pia ili ajue kwamba hasira hasara.

Baada ya kudai hivyo, Wakili wa Utetezi, Gerald Noah, aliiomba mahakama kumpunguzia adhabu mshtakiwa kwa sababu amekaa mahabusu kwa muda mrefu kwamba kwa muda huo atakuwa amejifunza na amejutia kosa lake.

Alidai mshtakiwa ni kosa lake la mara kwanza, ana umri wa miaka 57 na ana wazazi wazee sana ambao wanamtegemea yeye, kwa hiyo anaomba mahakama impunguzie adhabu.

Hakimu aliridhia kumpunguzia adhabu mshtakiwa kutokana na shufaa iliyotolewa na pia hakuisumbua Mahakama kwa sababu alikiri kosa la kuua bila kukusudia.

Ilidaiwa Januari 26, 2018, mshtakiwa aliimuua Baraka Thomas bila kukusudia, maeneo ya Temeke, Dar es Salaam.

Mshtakiwa alikuwa akiishi na wenzake wawili katika chumba kimoja akiwamo Thomas na chanzo cha mauaji hayo ni ugomvi wake na mtu mwingine aliyefahamika kwa jina la Hussein.

Mshtakiwa alikuwa katika ugomvi na Hussein lakini waliamuliwa na baadaye Hussein kukimbilia pembeni ndipo mshtakiwa akaamua kufuata uelekeo aliokwenda Hussein kwa nia ya kumpiga.

Baada ya muda mshtakiwa alimkanyaga tumboni akidhani ni Hussein kumbe alikuwa Thomas. Shuhuda wa tukio hilo, George Charles, alimtoa mtuhumiwa na kumwambia kuwa huyo anayempiga si Hussein.

## Shughuli za binadamu zachangia uharibifu chanzo maji

Na Mwandishi Wetu, HAI

KUKITHIRI kwa shughuli za binadamu na ongezeko la ujenzi wa makazi pembezoni mwa chanzo cha maji cha Magadini, Wilaya ya Hai, mkoani Kilimanjaro, kimewaamsha usingizini wadau wa mazingira kuanza kupiga kelele ili mamlaka husika zichukue hatua za kukinusuru kukauka.

Chanzo hicho kilikuwa kikitumika pia kama bwawa la ufugaji wa samaki katika Kata ya Bondeni.

Akizungumzia tishio hilo jana, wakati wa upandaji miti katika chanzo cha maji cha Salehe kilichoko Rundugai, Aziz Simbano, alisema eneo hilo walikuwa wanafuga samaki na kujipatia kipato, lakini sasa chanzo hicho kimeanza kukauka.

"Tunaomba sana mamlaka zinazohusika, hasa Bonde la Pangani na Halmashauri ya Wilaya ya Hai, kutafuta mwarobaini wa kukinusuru chanzo hiki kisife na kuathiri uchumi wa wananchi wa Bondeni na wilaya yetu kwa ujumla," alisema.

"Ni ajabu chanzo hicho kimevamiwa na watu wanajenga nyumba na wengine kulima, na hivyo kufanya chanzo kuanza kukauka na kuwa katika hatari ya kupotea kabisa."

Simbano ambaye ni Diwani wa Kata ya Rundugai, aliwasihi viongozi na wanaharakati wa masuala ya mazingira, kufanya tathmini ya kujua idadi ya vyanzo vya maji ambavyo vimevamiwa na kuwa katika hatari ya kutoweka.

Katibu wa Kikundi cha Kutunza Mazingira Rungugai (TUMAYA), Haji Msuya, akizungumzia suala la mazingira, alisema kikundi hicho licha ya kujitahidi kutunza na kusimamia mazingira, kinakabiliwa na tatizo la uhaba wa vitalu vya miti na kurudisha nyuma jitihada zao.

Kwa mujibu wa Msuya, kikundi hicho kinasimamia vyanzo 36 vya maji vilivyoko ukanda wa tambarare.

# Uchakavu madarasa watishia maisha walimu, wanafunzi

**Na Mwandishi Wetu, HAI**

SHULE ya Sekondari ya Ng'uni Wilaya ya Hai, mkoani Kilimanjaro, inadaiwa kutishia usalama wa wanafunzi na walimu kutokana na uchakavu wa vyumba vya madarasa na miundombinu.

Inadaiwa pia kuwa shule hiyo inakosa ushawishi wa kuwavutia wanafunzi wengi kusoma masomo ya Sayansi kutokana na kukosa maabara za Kemia na Bailojia.

Taarifa kuhusu hali inayoikabili shule hiyo kwa sasa iliwasilishwa jana kwa Mkuu wa Wilaya hiyo, Juma Irando, wakati wa mahafali ya kidato cha nne. Irando aliwakilishwa na Ofisa Tarafa ya Masama Mashariki, Nsajigwa Ndagile.

Akisoma taarifa hiyo, Neema Massawe, alisema madarasa chakavu yanayotumika sasa hayana madirisha na kuathiri utayari na usikivu wa wanafunzi kutokana na baridi kali na mvua kupenya madarasani wakati wa mvua za msimu wa masika na vuli.

"Mambo haya kwa ujumla wake yanaathiri sana ufaulu wa wanafunzi, hasa ukizingatia kwamba jiografia ya ukanda huu ni ya baridi kali na mvua kwa vipindi virefu.

Matatizo mengine yanayoikabili shule ya kata ni pamoja na kukosa mashine ya kudurufu mitihani ya majaribio na hivyo kuwalazimu walimu kuandika ubao na ukosefu wa bwalo.

Akijibu malalamiko kuhusu miundombinu ya shue hiyo, Nsajigwa Ndagile ambaye ni Ofisa tarafa hiyo, alisema amesikia kilio cha wanafunzi na wakazi wa Ng'uni, atalipeleka jambo hilo kwa Mkuu wa Wilaya ili lipate ufumbuzi wa kudumu.

"Nalibeba kama lilivyofika kwangu na nitazifikisha kwa wahusika ambao ni Mkuu wa wilaya aliyenituma kuja hapa pamoja na Halmashauri ya Wilaya ya Hai, ambayo ndio wenye shule hii," alisema Ndagile.




Ofisa wa Kitengo cha Mawasiliano na Masoko wa Taasisi ya Uhandisi na Usanifu Mitambo Tanzania (TEMDO), Dk. Sigisbert Mmasi (katikati), akifafanua jambo kwa baadhi ya wananchi waliotembelea katika maonyesho ya 17 ya Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO) Kanda ya Kaskazini, kwenye viwanja vya Makumbusho jijini Arusha juzi. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

# Wadau waomba mpango urasimishaji ardhi uendelee

**Na Cynthia Mwilolezi, ARUSHA**

WADAU wa sheria nchini, wameiomba serikali kuendelea na mpango wa urasimishaji ardhi ili wananchi wawe na maeneo yanayotambulika kisheria na kuondoka na migogoro inayowasumbua.

Akizungumza jana katika soko la Mbauda na Kilombero, jijini hapo, wakati wa utoaji wa msaada wa kisheria katika Wiki ya Azaki, Mratibu wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Hamisi Mayombo, alisema katika utoaji wao msaada wa kisheria kwa Kanda ya Kaskazini wamebaini kesi nyingi ni za migogoro ya ardhi na masuala ya ajira.

"Kutokana na utitiri wa kesi hizi za ardhi sisi wadau wa sheria tunaomba serikali iendelee na zoezi la urasimishaji maeneo kwani yakipimwa itasaidia kupunguza migogoro hii," alisema.

Pia alishauri kuwe na mabaraza ya ardhi zaidi ya moja kwa wilaya zenye watu wengi kama Arusha na kwingine kuwapo moja kwa kila wilaya ili kuharakisha mashauri ya kesi hizo.

Alisema kwa sasa changamoto katika kusuluhisha kesi hizo ni kurundikana kutokana na kuwa na baraza moja kwa Wilaya ya Arusha ambalo linahudumia Wilaya ya Longido, Monduli na kwingine.

Alishauri serikali kuitazama upya sheria na sera za ardhi na urasimishaji ardhi na itungwe kulingana na matatizo yaliopo.

Kayombo alisema kwa upande wa ajira kesi nyingi zimetokana na janga la Uviko-19 kutokana na waajiri wengi kushindwa kulipa watumishi wao mishahara na kukatiza mikataba bila kufuata sheria.

Ofisa Sheria kutoka LHRC, Amani Mkwama, alisema katika msaada wa kisheria wanaoutoa wamebaini uwapo wa watu wenye mahitaji mbalimbali wakiwamo wanaohitaji msaada wa mawakili mahakamani na baadhi kuandikishwa nyaraka za kisheria.

"Kila mmoja tunamsaidia kulingana na hitaji lake, hivyo tunawaomba wananchi kujitokeza kuja kupata msada huu bure hata wenye migogoro ya kifamilia pia tunapokea na kuwapatia huduma stahiki," alisema.

Mmoja wa wananchi waliopatiwa msada huo, Rashidi Msangi alishukuru LHRC na wadau wote wa sheria walionao kwa kuwa umesaidia tatizo lake na sasa atafuta hatua alizoshauriwa.

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) katika utoaji msaada huo wanasaidiana na Chama cha Wanasheria Wanawake (TAWLA), Chama cha Mawakili Tanganyika (TLS) na Mfuko unaotoa msaada wa huduma za kisheria (LSF).

## Serikali kuendeleza ushirikiano wawekezaji wa nje

**Na Cynthia Mwilolezi, ARUSHA**

MKUU wa Wilaya ya Arumeru, Richard Ruyango, amesema serikali itaendelea kutoa ushirikiano kwa wawekezaji toka nje, kutokana na kuonekana matunda kwenye sekta mbalimbali ikiwamo elimu.

Aliitaja Shule ya Kimataifa ya Turkish Maarif inayomilikiwa na serikali ya Uturuki inavyofanya vizuri kwa kutoa elimu bora.

Aidha, amepongeza hatua ya shule hiyo kuweka msisitizo kuendeleza vipaji vya watoto kwa kuwawezesha kutimiza ndoto zao kwa yale wanayoyajua nje ya masomo na mmoja wa wanafunzi hao alionyesha ndege aliyoitengeneza kwa kutumia kemikali rafiki na mazingira kuirusha.

Aliyasema hayo jana wakati wa mahafali ya wanafunzi 87 wa chekechea, msingi na sekondari wa shule hiyo Ngaramtoni wilayani Arumeru, mkoani Arusha.

"Serikali inavyofanya kazi na wawekezaji shule hii inaendeshwa na serikali ya Uturuki na inatoa elimu bora kwa vijana wetu. Rais Samia Suluhu Hassan mara zote anatuhimiza tuhakikishe kila wakati tunawapa ushirikiano wawekezaji na hii ndiyo faida," alisema Mhandisi Ruyango na kuongeza:

Tumeona ni jinsi gani vijana wetu wana vipaji mbalimbali wanaweza kuongea lugha nne kwa wakati mmoja, (Kiswahili, Kiingereza, Kirafansa na Kituruki) vijana wa chekechea wameweza kuimba nyimbo za asili za Tanzania, vijana wa sekondari wameimba Kituruki."

"Niwapongeze shule hii kwa mazingira mazuri, majengo mazuri na walimu wanavyowafundisha watoto vizuri na hii inadhihirishwa na yale watoto waliyotuonyesha hapa.

Wazazi mtakubaliana na mimi watoto wenu wanaohitimu hapa wana mabadiliko makubwa kimakuzi na kielimu," alisema.

Hata hivyo, aliwakumbusha wazazi suala la malezi ya watoto ni la walimu na wazazi na kwamba ni vyema wakatimiza wajibu wao badala ya kuacha jukumu hilo kwa walimu pekee.

"Watoto wameniambia wametumia Sh 100,000 kwa ajili ya kuandaa 'jet' (ndege) nawarudishia ili waendelee na utafiti wao lengo langu ni kuwafanya vijana hawa wasikate tamaa waendelee kuwa wabunifu," alisema.

Mkurugenzi wa shule hiyo, Halil Server, alisema wanaendelea kuboresha miundombinu ya shule hiyo ikiwamo kupanua bwalo la kulia chakula na chumba cha Tehama ili viweze kutumiwa na wanafunzi wengi zaidi kwa wakati mmoja.

Kwa upande wake, Mkuu wa Shule ya Msingi, Turkish Maarif, Rafael Sabaya, aliwasihi wazazi kubadili mtazamo wa kutaka watoto wao kusoma ili wafanye kazi za kuajiriwa badala yake wawaache watumie vipaji walivyonavyo kujitengenezea ajira.

Awali, akisoma risala kwa niaba ya wahitimu, Ethan alisema shule hiyo imewapa elimu bora itakayowawezesha kukabiliana na mazingira yao na kuweza kuishi na jamii.

# Bodi ya Maji, Tume Umwagiliaji kukutana na wakulima mabadiliko ya tabianchi

**Na Mary Mosha, MOSHI**

KUTOKANA na mabadiliko ya hali ya hewa, Bodi ya Maji Bonde la Pangani (PBWB), kwa kushirikiana na Tume ya Umwagiliaji wamelazimika kukutana na wakulima wa skimu ya Umwagiliaji Lower Moshi ili kuona namna ya kutumia maji yaliyopo.

Hali hiyo imeibuka baada ya maji katika baadhi ya mifereji hiyo kupungua na baadhi ya wakulima kuhofia mazao yao kukauka.

Mkurugenzi wa Bodi hiyo, Segule Segule, aliwataka wakulima kuacha kuongeza mashamba yao na badala yake kutumia maji hayo kwa uangalifu.

"Sheria ya Maji namba 11 inatutaka kunapotokea tatizo la maji, kupitia upya vibali na wakati mwingine kusitisha baadhi, lakini kwa hapa tumekubaliana wakulima wapate maji kidogo waliopo milimani waache na wenzao kupata maji hasa wa ukanda wa chini."

Mmoja wa wakulima akiwamo Abbas Mrutu, alisema maji yamepungua na kusababisha baadhi ya mazao kuanza kukauka.

"Leo tumekutana hapa, tumeeleweshwa nini kimetokea, sisi tutaanza kufanya usafi kwenye vyanzo vya maji na kuotesha miti ili kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi," alisema Safina Mshana.

Mhandisi wa Tume ya Umwagiliaji, Said Ibrahim alisema lengo la kukaa pamoja ni pamoja na kujua hali halisi na mahitaji yaliyopo ili kuomba fedha kwa ajili ya uchimbaji wa visima kuwasaidia wakulima.

Alisema ni vigumu serikali kutoa fedha kwa ajili ya uchimbaji wa visima ikiwa hawajui hali halisi.

"Leo tumekuja kwenu kuwasikiliza pamoja na kujua ukubwa wa tatizo ulivyo, hakuna haja ya kuombana tunatakiwa kushirikiana ili kila mtu aweze kuvuna kupitia maji kidogo yanayopatikana kwa sasa licha ya kuwapo kwa ukame," alisema Mhandisi Said.



Ofisa Rasilimali Watu Mwandamizi wa Barrick, Renatus Malawa, akichangia mada katika warsha ya wataalamu wa fani ya rasilimali watu Kanda ya Afrika Mashariki, jijini Arusha jana, iliyodhaminiwa na kampuni hiyo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mwekezaji kiwanda cha maziwa amlilia Samia amsaidie

**Na Woinde Shizza ARUSHA**

MWEKEZAJI mzawa wa kiwanda cha maziwa jijini hapa, John Kyenkungu (68), Mkazi wa jijini Dar es Salaam amemwangukia Rais Samia Suluhu Hassan, kumwomba arejeshewe kiwanda chake alichokuwa ameuziwa na serikali na baadaye kupokonywa kimabavu katika mazingira ya utata.

Akiongea kwa uchungu baada ya kufika kiwandani hapo, alisema kiwanda hicho kinachojulikana cha New Northern Creameries Ltd kilichopo eneo la Unga Ltd, plot 4213, alikinunua kihalali mwaka 1998 baada ya kufilisika.

Alisema kiwanda hicho kilitangazwa mufilisi na shirika la serikali la Tanzania Industrial Studies and Consulting Organisation, kupitia gazeti la serikali la tarehe 6/11/ 1996.

"Mwaka huo 1996 kupitia kampuni yangu ya Jamaa Fast Food, nilinunua Tender Document na kuanza mchakato kuomba kuuziwa kiwanda hicho tukiwa na wengine ambao pia wali -Tender. "

Alisema, mwaka 1998 alijulishwa kwamba kampuni yake ya Jamaa fast food imeshinda zabuni ya kununua kiwanda hicho kwa gharama ya Sh. milioni 440.

Kyenkungu ambaye ni Mkurugenzi wa kampuni ya Jamaa Fast Food alisema mwaka 1999 walifanikiwa kulipa kiasi hicho cha fedha na kununua hisa zote za serikali kwa asilimia 100.

"Moja ya vigezo vilivyopo kwenye zabuni ni kwamba serikali ikishauza hisa zake zote asilimia 100 itabadilisha jina na hati ya umiliki kwenda kwa kampuni itakayonunua."

Alisema baada ya kukidhi masharti yote ya zabuni ikiwamo kulipa fedha zote alitia saini hati ya mauziano na kukabidhiwa hati ya kiwanda hicho inayosoma kampuni yake mpya ya maziwa ya New Northern Creameries Ltd.

Alisema baada ya kukabidhiwa alichukua mkopo wa Sh. milioni 600 kutoka taasisi za fedha ili kukifufua baada ya kusimamisha uzalishaji kwa muda wa miaka mitano.

"Mwaka 1999 tulifanikiwa kuanza uzalishaji wa maziwa yaliyojulikana kwa jina la Jamii Milk." Alisema katika kipindi chote cha uzalishani walikumbana na changamoto mbalimbali ikiwamo uhaba wa upatikanaji wa maziwa na masoko, na pia kushindwa kutimiza malengo ya uzalishaji na kulipa mkopo waliochukua kuendesha kiwanda hicho.

"Mwaka 2002 taasisi ya fedha ilitupeleka mahakama ya biashara kwa kushindwa kulipa mkopo na mahakama hiyo ilitoa hukumu ya kusudio la kuuza kiwanda hicho ili kufidia deni lililokuwa limefikia kiasi cha Sh. milioni 825 kutoka Sh. milioni 600 tulizokopa."

Kyenkungu alisema kampuni yake iliingia makubaliano na taasisi hiyo ya fedha kulipa deni hilo katika kipindi cha miaka kumi hadi mwaka 2017 walipofanikiwa kulipa deni lote. Alisema mwaka 2019 wakiwa kwenye mpango kazi wa kuendelea na uzalishaji, ghafla askari polisi wapatao 20 wakiwa na silaha za moto waliwavamia na kuwaondoa kwa nguvu bila maelezo yoyote wala barua za maelezo.

Kyenkungu amemwomba Rais Samia kumsaidia kurejeshewa kiwanda anachoamini ni mali yake akidai kwamba juzi Oktoba 23, 2022 alienda kiwandani hapo na walinzi wake ili kuangalia hali baada ya kusimama kwa muda mrefu, lakini aliondolewa na walinzi wa Suma JKT waliowekwa na serikali na kutakiwa kutoa maelezo polisi jambo ambalo alisema ni uonevu mtupu.

Mwekezaji huyo alilalamika kukuta kiwanda kikiwa kimeoza na kuwa katika mazingira mabovu huku miundombinu ikiwa imeharibika na kumwomba Rais Samia kumsadia kuchunguza mazingira ya kumwondoa.

Alisema aliwekeza rasilimali zake nyingi kuendesha kiwanda hicho na sasa amezeeka hataki kukimbilia mahakamani kuishtaki serikali kwa sababu nyaraka zake zinajieleza na anaamini hajawahi kuvunja masharti ya ununuzi.



Ukurasa 16

## Congo na imani kwa Tanzania ndiyo baba wa uchumi wa DRC



Ukurasa 18

Bilionea Rishi Sunak anapoahidi uadilifu mkubwa kwa Waingereza



Ukurasa 19

**TOM JOSEPH MBOYA**

## Shujaa wa uhuru, maendeleo ya Kenya aliyezawadiwa kifo

siasa

JUMATANO OKTOBA 26, 2022

HABARI BORA NA KAMILIFU

Nipashe

TAKUKURU, ZAECA NJIA PANDA

# Ni kuchunguza watuhumiwa wanapoelekezwa si 'kulianzisha'

**Na Ani Jozeni**

KUNA dalili kwamba mshikamano wa kiserikali unaweza kuzuia utendaji kazi wa mamlaka za Taasisi za Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Bara na Mamlaka ya ZAECA kwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

Ni hali ambayo imejitokeza katika matamshi na hatua za viongozi wakuu wawili wa serikali Rais Samia Suluhu Hassan hivi karibuni na Rais Hussein Ali Mwinyi.

Kwa upande wa Zanzibar, mkuu wa taasisi hiyo alijiuzulu wakati Bara, Rais Samia akiwaambia 'wajisafishe kwanza.'

Katika hotuba ya hivi karibuni, Rais Samia anaikemea TAKUKURU kuacha kuchukua hatua kuzuia rushwa na ubadhirifu, ikingoja taarifa kwa mfano ripoti ya mwaka ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali (CAG) aelekeze wapi kuna hitilafu, ili waanze uchunguzi. Wakati Rais Mwinyi akisema ripoti za kila mwaka za CAG wa Zanzibar zinatoka na hakuna hatua inayochukuliwa, Rais Samia anawaelezea kuhusu kutokujituma na kungoja ripoti kama hiyo ya CAG ili waanze kufanya kazi.

Sheria ya kuunda TAKUKURU inalenga 'kuzuia na kupambana na rushwa,' si 'kuja baadaye,' kama ambavyo sasa wameshitukiwa.

Rais Samia anasema hayo akizungumza baada ya kupokea taarifa ya Mbio za Mwenge wa Uhuru 2022, inayoeleza kuzindua miradi 65 na kukataa mingine kadhaa.

Taarifa ya Mwenge inatuhumu gharama kubwa zaidi ya uwekezaji kuliko kinachoonekana katika miradi hiyo, ikitaka hatua zichukuliwe kwa kuiichunguza.



Rais Samia Suluhu Hassan, akihitimisha mbio za Mwenge mwaka huu mjini Bukoba. **PICHA MTANDAO**

Mwenge wa Uhuru ulizimwa kwenye Uwanja wa Kaitaba mjini Bukoba Oktoba 14 siku ya kumbukumbu ya kifo cha Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere.

Baada ya timu ya Mwenge kukataa miradi kadhaa Rais Samia akashangaa kama hapakuwa na dalili zozote za hali hiyo hadi Mwenge ulipowasili.

Ingekuwa imeonekana, TAKUKURU wangechukua hatua mapema, lakini huenda hakuna aliyefuatilia.

Rais Samia anasisitiza kuwa TAKUKURU imeundwa ili kuzuia na kupambana na rushwa, akitilia mkazo ulazima wa kuendana na malengo hayo katika utendaji wake.

### KUJISAHAU AU?

Suala hapa ni kama TAKUKURU na ZAECA wanajisahau kiutendaji au kuna siri katika utekelezaji inayotawala shughuli zao, na sasa hitaji la ufanisi serikalini likileta ukinzani kati ya utendaji halisi na 'siri' hiyo.

Ni kama kuziumbua taasisi hizo kiutendaji wakati walioko madarakani pande zote ni kama wanavunja mwiko, kwa uelewa wa taasisi hizo, nini hasa kinatokea au kifanyike.

Suala hapa ni kama TAKUKURU na ZAECA wanakiuka maelekezo ya sheria ya kuunda taasisi

INAENDELEA UK. 20

MIAKA 14 KUPIGA KURA

# HakiElimu yaulizwa yawezekana umri huo kuwa mbunge, diwani?

• Wadau wapata kigugumizi wataka utafiti, mjadala, si kukurupuka



Wanafunzi wa miaka 14 ambao baadhi wanakuwa bado shule za msingi wanaweza kupiga kura na kuchaguliwa kuwa viongozi, ni pendekezo la taasisi ya HakiElimu. **PICHA: MTANDAO**

**Na Sabato Kasika**

UMRI wa kupiga kura ambao upo kikatiba, ni kuanzia miaka 18 Mtanzania anapotimiza anaruhusiwa kushiriki katika michakato ya kisiasa, iwe kuchagua au kuchaguliwa kuwa kiongozi na kushika nafasi mbalimbali, japo sio kuwa rais , ili kuongoza serikali unatakiwa kutimiza miaka 40.

Hata hivyo, Asasi ya Haki Elimu ambayo hivi karibuni ilifanya utafiti, inakuja na mapendekezo mapya ya kutaka umri huo ushuke na kuanzia miaka 14, lengo likiwa ni kumuandaa mtoto ambaye hajatimiza miaka 18 atakapokuwa kijana kushiriki katika michakato ya demokrasia na masuala ya kisiasa kikamilifu.

Kutokana na mapendekezo hayo, Nipashe inazungumza na wadau mbalimbali ili kupata mtazamo na maoni yao kuhusu umri huo unaopendekezwa na asasi hiyo kama unatosha au uendelee ule wa miaka 18.

Mayasa Kalinga ni Mkurugenzi na mtaalam wa saikolojia wa taasisi ya Tanzania Suicide Prevention Coalition (TSPC), ya jijini Dar es Salaam, inayojishughulisha na kuzuia na kupambana na kujiua, anakubaliana na mapendekezo ya HakiElimu, kwa maelezo kwamba dunia ya sasa si kama ya zamani, na kufafanua kuwa watoto wadogo wana akili kubwa.

"Ninaungana nao kama wamemuangalia mtoto kiakili, kiafya, kwani watoto wa sasa, wanajifunza vitu vingi wanaelewa, wana upeo mkubwa wa mambo, hivyo kwa hali hiyo si vibaya wakaruhusiwa kupiga kura,"anasema Mayasa.

Anafafanua kuwa uelewa wa watoto wa zama hizi si kama wa watoto wa zamani ambao walikuwa wazito, na kwamba kwa muktadha huo, haoni tatizo wakiruhusiwa kupiga kura wakiwa na umri huo wa miaka 14.

> Lakini pia ingekuwa ni vyema masomo ya masuala ya siasa na demokrasia yangefundishwa shuleni, ili watoto waanze kuelewa umuhimu wa kushiriki uchaguzi, kama miongoni mwa haki zao za kidemokrasia.



Mtaalam huyo wa saikolojia, anasema ikiwezekana, umri wa kuanza elimu ya msingi nao ungebadilishwa hadi kuanzia miaka mitano ili watoto wa umri huo nao waweze kufanya vizuri darasani.

"Lakini pia ingekuwa ni vyema masomo ya masuala ya siasa na demokrasia yangefundishwa shuleni, ili watoto waanze kuelewa umuhimu wa kushiriki uchaguzi, kama miongoni mwa haki zao za kidemokrasia," anasema.

Anaeleza kwamba si vibaya kwenda kulingana na mabadiliko, akifafanua kuwa uelewa wa watoto wa umri wa miaka 14 wa sasa, uko sawa na ufahamu wa watoto wa miaka 18 wa zamani na kuongeza kuwa dunia inakwenda kwa kasi.

### NI SAWA, LAKINI

Mchambuzi wa siasa na Mkurugenzi Mtendaji wa Jukwaa la Katiba Tanzania (JUKATA), Bob Wangwe, anasema suala la kupiga kura linahitaji mjadala mpana, majaribio, utafiti wa kutosha ili wadau wengine waweze kufanya utafiti wao ili kuona kama umri huo unafaa au vinginevyo, lakini kwa mtazamo wake kama mdau na mchambuzi wa masuala ya siasa na elimu, miaka 18 inafaa zaidi kama ambavyo Ibara ya 5 (1) ya Katiba ya Tanzania ilivyompa haki kila raia aliyetimiza miaka 18 kupiga kura.

Anautaja kuwa ni wakati ambao kimsingi mtu anaitwa mtu mzima, lakini zaidi labda wangeshauri uanzie miaka 16, badala ya miaka14 kwa kuwa miaka 14 bado ni watoto wadogo ambao hawajakomaa.

"Hivyo ushauri wangu ni wadau wengine zaidi wajitokeze kufanya utafiti ili kuja na majibu ambayo yatalinganishwa na hatimaye kujibu kwa usahihi wakati ambao mtu anatakiwa kupiga kura. Ila jambo la muhimu ni kwamba unahitajika mjadala mpana zaidi ukishirikisha wadau wengi kama wanasaikolojia, wanasiasa, walezi, wazazi walimu na wanafunzi ili kuchambua faida na hasara za umri huo kushiriki katika uchaguzi, kwani ninaamini katiba kuweka umri wa miaka 18, kuna utafiti wa kina ulifanyika."

### UTAFITI UPANULIWE

Abdulkarim Atiki ni mchambuzi wa siasa na kada wa CCM, anaungana na Wangwe akishauri utafiti ufanyike kwanza ili kuja na jibu akisema: "Kwenye suala la umri, watu wa saikolojia ni wa muhimu na hata walimu wao kwani hao ni wadau muhimu wanaowajua watoto vizuri na wanaweza kusaidia kupata umri sahihi wa mtu kushiriki katika uchaguzi," anasema Atiki.

Mchambuzi huyo anafafanua kuwa wadau hao wanaojua kuwa mtoto wa miaka 14 anaweza kushiriki uchaguzi au la, kwa kuwa suala la kuchagua haliisadii kuchagua tu bali pia kuchaguliwa.

"Je, mtoto wa miaka 14 naye achaguliwe kuwa mbunge, diwani, mwenyekiti wa serikali za mitaa? Kama nilivyoeleza, suala la kuwapo kwa utafiti zaidi ni la msingi ingawa ukweli ni kwamba utafiti huwa unapingwa kwa utafiti,"anasema Atiki.

### WALICHOBAINI HAKI ELIMU

Kwa mujibu Kaimu Mkurugenzi Mkuu HakiElimu, Godfrey Bonventure, asilimia 44.4 ya wanafunzi wa sekondari hawaelewi maana ya demokrasia, huku asilimia 85.5 hawajawahi kushiriki, kushirikishwa katika vikao rasmi vya shule vinavyofanya uamuzi.

Anasema hayo hivi karibuni, katika hafla ya uzinduzi wa ripoti ya utafiti wa Mchango wa Elimu ya Uraia Shule za Sekondari na ushiriki wa vijana katika michakato ya kidemokrasia.

Anasema utafiti huo umebaini kuwa asilimia 68.9 ya wanafunzi hawajawahi kugombea au kuonyesha nia ya kugombea nafasi yoyote ya uongozi ngazi ya shule, huku asilimia 44 hawashiriki katika uchaguzi za uongozi wa wanafunzi.

Lakini pia asilimia 26 hawajawahi kushiriki katika midahalo na mijadala ya hoja kama sehemu ya kuwajengea uwezo wa ushawishi na demokrasia, na kwamba utafiti uliofanyika katika wilaya za Mkuranga, Tabora, Ukerewe, Kilwa, Sumbawanga na Arusha, huku ukionyesha ushiriki hafifu wa vijana katika mifumo ya kidemokrasia ndani na nje ya shule unachangiwa na upungufu katika mtaala wa elimu ya uraia itolewayo shule za sekondari.

"Utafiti pia umebaini kuwapo kwa changamoto kubwa katika mtaala wa somo la uraia shule za sekondari, ambao kwa kiwango kikubwa haumpi mafunzo stahiki mwanafunzi yatakayomfanya aelewe vyema na kushiriki shughuli za kidemokrasia katika ngazi mbalimbali kwa nafasi yake," anasema.

Hata hivyo iwapo watoto hawafahamu masuala ya siasa na wana zaidi ya miaka 14 inawezekana waingizwe kwenye michakato ya kidemokrasia katika umri mdogo bila hatua kuchukuliwa na kuboresha na kubadilisha mitaala, ni swali ambalo HakiElimu wanatakiwa kulifanyia tena kazi.

SEIF SHARIFF HAMAD

# Anapoibuliwa tena akitajwa mhubiri wa kipekee wa amani, mshikamano

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

NI miaka miwili sasa Tanzania na Zanzibar bila Seif Shariff Hamad. Inafanyika kumbukizi ya miaka miwili ya kumuezi mwanasiasa nguli Maalim Seif, zinazomtaja kuwa mwanazuoni mwenye kuhubiri amani na mshikamano pamoja na kuwa alama ya mchango mkubwa wa kukuza demokrasia na haki za binaadamu Bara na Visiwani.

Tafakuri ya maisha ya Hamad inaibua hisia za wanasiasa,vijana na washiriki wa mkutano na kuueleza mchango mkubwa uliofanywa na mwanasiasa huyo wakimtaja kuwa amefanikisha kuiumba na kuisuka demokrasia madhubuti inayoonekana leo.

Ukitayarishwa na Maalimu Seif Foundation, mkutano huo umewakutanisha wananasiasa, wataalamu, wanadiplomasia na wananchi kujadili mada kadhaa ikiwa ni hatua ya kuenzi fikra za Maalim Seif kutokana na mchango wake mkubwa katika kuweka Wazanzibari na Watanzania pamoja, kuhubiri amani na mshikamano na kuchangia ukuaji wa demokrasia na haki za binaadamu nchini.

Akizungumza katika kumbukizi hiyo Makamu Mwenyekiti wa CCM Abrahman Kinana, anamwelezea kuwa kiongozi mwenye maono ,msimamo na mwenye ushawishi mkubwa kwa watu wengi wakiwemo wafuasi wake na wanaomwamini.

Anasema mwanasiasa huyo aliyefariki Machi 17 mwaka 2020, alipenda kuona vijana wanapata elimu bora inayolingana na mahitaji ya wakati na yenye kuwajenga kudadisi,kujituma, kujitegemea na kuwa wazalendo kwa jamii na ndio maana elimu yake alipata kwa kujituma na bila kukata tamaa.

"Bila shaka viongozi wa wakati huo waliona na kuthamini kiu aliyokuwa nayo Maalim Seif na hivyo kumpa nafasi ya kuongoza wizara ya elimu akiwa na umri mdogo jukumu hilo lilikuwa zito hasa kwa kuwa fursa za elimu zilikuwa ndogo na hafifu"anasema.

Kinana anauzungumzia ujasiri mkubwa aliokuwa nao Maalim Seif na kwa hatua za kuthubutu alijitwisha dhamana ya kufanya kazi aliyopewa kwa ustadi, hamasa na ari kubwa tena kutokana na juhudi zake hizo vijana wengi wa Zanzibar walipata nafasi za elimu ndani na nje ya nchi.

Anakumbusha kuwa aliamini sana katika elimu, nafasi yake na fursa zinazoletwa na elimu katika maisha ya binadamu na katika uhai wa taifa hilo na kukumbusha kuwa Tanzania imeanza mchakato wa kutazama upya sera na mfumo wa elimu kwa lengo la kuiboresha ili ilenge kuwajenga watoto kujitegemea na kuendana na mabadiliko na mahitaji ya ulimwengu wa sasa.

Makamu Mwenyekiti Kinana, anafurahishwa na namna vijana wengi wanavyojituma na kujielimisha kwa kutumia akili na nguvu zao pamoja na ubunifu katika kujitafutia fursa za kujitengenezea ajira, kujiongezea kipato na kuwa wabunifu wakitamani maisha bora.

"Haya tumeyaona katika nyanja za teknolojia, sanaa, biashara na katika uzalishaji wa mazao na bidhaa, hapa vijana wetu wanajituma na wanahangaika wanatafuta njia kadhaa za kujiajiri na kujiongezea kipato,"anaeleza Kinana.

Anasema Rais Samia ana lengo la kusimamia haki, kukuza, kuimarisha uhuru, kupanua wigo wa kuendesha shughuli za kisiasa na kuleta mageuzi katika uendeshaji wa serikali kwa madhumuni ya kuharakisha maendeleo ya nchi na watu wake.




Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar Othman Masoud Othman, akizungumza katika ufunguzi wa mkutano wa pili wa kumuenzi Maalim Seif. **PICHA: RAHMA SULEIMANI.**

### MARIDHIANO, UCHUMI

Makamu wa Kwanza wa Rais Othman Masoud Othman, anasema maridhiano ya kisiasa Zanzibar yaliyoasisiwa na Maalim Seif na viongozi wengine yatajenga uchumi imara wa Zanzibar na kuinua maisha ya wananchi.

Othman anasema kuwepo Zanzibar yenye uchumi imara ni muhimu katika kukabiliana na changamoto mbalimbali zinazokwamisha maendeleo ya nchi na kwamba katika kukabiliana na hali bora ya kuwatayarisha vijana kielimu ni lazima kwa serikali kutengeneza na kuwepo sera na uendeshaji bora wa sekta hiyo ya elimu unaosaidiwa na usimamizi bora na kuwepo muono sahihi katika uongozi.

Aidha, anasema kumtayarisha mtoto kuwa mwerevu kielimu kutasaidiwa na kuwepo makuzi na malezi bora kwa kuzingatia mazingira anayoishi ikiwemo usomeshaji na uwepo wa kutumika mitaala bora.

Othman ambaye ni mrithi wa Maalim Seif, anasema ni lazima kubuni mbinu tofauti zitakazosaidia sekta ya elimu kuzalisha vijana werevu watakaokwenda sambamba na mahitaji ya sasa na ya baadaye yanayoongozwa na mabadiliko ya sayansi na teknolojia kwa manufaa ya taifa.

Halikadhalika, anasema wakati nchi inaelekea katika mjadala wa mageuzi makubwa ya sekta ya elimu ni wajibu kwa Wazanzibari kuwa na tafakuri ya kina ya umuhimu wa suala hilo na namna kulifanikisha .

Anasema hatua hiyo ni muhimu katika jitihada za pamoja za kujenga hatma njema ya Zanzibar kielimu kwa kuzalisha vijana wenye maarifa na werevu wa kitaaluma hasa kwa vile taifa imara linategemea kizazi makini kilichotayarishwa kukabiliana na changamoto zilizopo na zijazo.

Anasema hali hiyo ni lazima kwenda sambamba na kuwepo maridhiano ya kweli, amani na utulivu nchini na kuwepo jitihada kubwa za kujenga uchumi imara na kuleta maendeleo ya kweli.

Mhadhiri Mstaafu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Profesa Issa Shivji, akiwasilisha mada kuhusu uhuru wa elimu msingi wa demokrasia , anasema huwezi kuwa na elimu bora bila kuwepo walimu wanaoweza kutengeneza vipaji kwa vijana.

Anasema walimu ndiyo wenye uwezo na upeo wa kuibua, kukuza na kuendeleza vipaji vya wanataaluma na kuzalisha wasomi bora wanaojiamini katika kuchangia vyema maendeleo ya taifa lao.

Professa Shevji anasema wanafunzi wa namna hiyo ndiyo wenye uwezo wa kujadili na kudadisi mawazo yaliyopo na kutoa mbadala yatakayosaidia vijana kuweza kuchangia upeo wa maendeleo ya nchi yao.

Naibu Katibu Mkuu wa ACT-Wazalendo Nassor Ahmed Mazrui, anaelezea mchango wa maalim Seif katika siasa za ujenzi wa demokrasia na kusisitiza kuwa maendeleo yatapatikana ikiwa uchumi utakuwa imara, kwa mfano katika sekta ya elimu Maalim Seif alichukua nafasi yake kuwaendeleza watu wengi na kuona wanapata elimu kwa maslahi ya taifa.

"Tutamuenzi Maalim Seif kwa mambo makubwa ambayo ameyafanya katika kipindi chake chote ikiwemo mikakati ya kukuza sekta ya elimu ambapo tunakusudia kuanzisha kigoda maalumu cha elimu ambacho kitazungumzia demokrasia"anaahidi Mazrui.

> Mfumo wa elimu wa Zanzibar unatakiwa uvunjwe moja kwa moja na tuje na mikakati ambayo itatuwezesha kuja na muundo wa elimu ambao utawezesha vijana wetu kuingia katika soko la ajira.

Mapema baadhi ya washiriki wa mkutano huo walisisitiza kuboreshwa elimu, kutumia mafunzo wanayoyapata yawafanikishe kumudu maisha yao.

Mhadhiri mwandamizi wa Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar SUZA Dk.Mariyamu Ismali Jaffar, anautaja mfumo wa elimu unahitaji kufanyiwa marekebisho hatua ambayo itawawezesha wahitimu wake kuingia katika soko la ajira kwa ajili ya kukabiliana na changamoto zilizopo.

Maryamu ambaye ni mjumbe wa kamati ya kikosi kazi kinachopitia muundo wa elimu wa Zanzibar, anaeleza kuwa wameanza kukusanya maoni na kuonana na makundi mbalimbali kujuwa mahitaji ya sekta ya elimu yanayohitajika kwa sasa.

Aidha Mkurugenzi mstaafu wa Wizara ya Elimu Hussein Ali Suleiman, alikiri kuyumba kwa sekta ya elimu ikiwemo ufaulu wake na kukitaka kikosi kazi kilichoteuliwa kufanya utafiti na kuja na mikakati ambayo itahakikisha elimu ya Zanzibar inapiga hatua kubwa na kuwawezesha wahitimu wake kujiajiri.

"Mfumo wa elimu wa Zanzibar unatakiwa uvunjwe moja kwa moja na tuje na mikakati ambayo itatuwezesha kuja na muundo wa elimu ambao utawezesha vijana wetu kuingia katika soko la ajira,"anasema.

Aidha, mhadhiri mstaafu wa Chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam, Profesa Chriss Maina Peter, anampongeza Maalim Seif Sharif Hamad ambaye alikuwa mstari wa mbele kuona vijana wengi wanajiunga na masomo ya sheria kwa ajili ya kujenga uwezo na kuingia katika soko la ajira.

"Maalim Seif Sharif Hamad alikuwa mstari wa mbele kuona vijana wanapata elimu katika ngazi mbalimbali ikiwamo ya sheria hatua ambayo ilituwezesha kuzalisha wanasheria wengi katika vyuo vikuu',anasema Maina Peter.

# Mwanahabari za uchunguzi wa Pakistan auliwa na Polisi Kenya



Balozi wa Pakistan Kenya , Saqlain Syedah, akizungumza na wanahabari kwenye hospitali ya Chiromo, ulipohifadhiwa mwili wa mwanahabari aliyeuawa Arshad Sharif.

**Na Mwandishi Wetu**

MWANDISHI wa habari mashuhuri anayeandika masuala ya uchunguzi na mkosoaji mkuu wa jeshi lenye nguvu la Pakistani, ameuawa nchini Kenya kwa kupigwa risasi ikiwa ni karibu miezi miwili baada ya kuondoka Pakistan, kunusuru maisha yake.

"Nimepoteza rafiki, mume na mwanahabari ninayempenda leo, polisi wamempiga risasi nchini Kenya," Javeria Siddique, mke wa mwanahabari huyo, anaandika katika mtandao wa tweeter kuhusu kifo cha mumewe Arshad Sharif Jumapili usiku.

Mwandishi huyo wa habari mwenye miaka 49 alitoroka Pakistani Agosti mwaka huu kukwepa kukamatwa baada ya kushitakiwa na misururu ya kesi zikiwamo za uchochezi.

Ni baada ya kufanya mahojiano na Shahbaz Gill - msaidizi wa karibu wa waziri mkuu wa zamani wa Pakistani Imran Khan .

Gill anadaiwa kutoa maoni yaliyodaiwa yameliudhi jeshi.

Akidai kunyanyaswa na taasisi za serikali pamoja na vitisho vya maisha yake kutoka kwa mamlaka za juu za Pakistani, alikimbilia Dubai Agosti mwaka huu na baadaye kuhamia Kenya, lakini akauawa.

Mwandishi huyo maarufu wa Pakistan, Arshad Sharif, aliuawa kwa kupigwa risasi usiku wa kuamkia Jumatatu maofisa wa usalama nchini Kenya wanasema.

Wanaeleza kuwa aliuawa alipokuwa akiwa ndani ya gari katika barabara ya kuelekea mji mkuu Nairobi, wakidai kuwa alipigwa risasi kimakosa kufuatia kile walichokitaja kuwa 'utambulisho uliokosewa' wakati walikuwa wakisaka gari lililofanana na alilokuwa ndani yake.

> Sharif mbobezi katika uandishi wa habari za uchunguzi alishughulikia matukio mengi ya kisiasa nchini mwake kwa mashirika ya habari ya kitaifa na kimataifa.



Mwandishi mwandamizi wa Pakstani, Arshad Sharif, enzi za uhai wake. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

Taarifa za awali zinasema Arshad Sharif aliuawa baada ya yeye na dereva wake kukaidi amri ya kusimamisha gari lao kwenye kizuizi kilichokuwa kimewekwa kukagua magari jijini Nairobi.

Kituo cha ARY ambacho Sharif alikifanyia kazi kwa miaka minane iliyopita kilifungwa na kuondoa matangazo yake hewani kwa muda mfupi Agosti kwa kupeperusha maudhui yaliyodaiwa kuwa ni "ya uwongo, chuki na uchochezi".

Kituo hicho kilitangaza mwishoni mwa Agosti kuwa kinaachana naye licha kwamba mwanahabari huyo alikuwa mmoja wa watangazaji wake wakuu na mahiri wakati wote.

Wizara ya Mambo ya Nje ya Pakistan ilieleza kuhuzunishwa na taarifa ya kifo chake ikiongeza kuwa Arshad Sharif,ataendelea kufuatilia na kuwasiliana na maofisa wa Kenya kuhusiana na suala hilo. Sharif alikuwa mkosoaji mkuu wa Jeshi la Pakistan, lakini akimuunga mkono Waziri Mkuu wa zamani wa Pakistan Imran Khan.

Kufuatia mauaji yake , uvumi umeenea katika vyombo vya habari vya Pakistan na umma kwamba Sharif ameuawa kwa kupigwa risasi jijini Nairobi Jumapili usiku katika hali isiyoeleweka.

Ripoti za awali zinaonyesha kuwa alikuwa akisafiri kurejea Nairobi kutoka Magadi akiwa na dereva wake alipokumbana na kifo kwenye kizuizi cha barabarani cha polisi.

Habari za kifo chake zilitangazwa kwa mara ya kwanza kwenye mitandao ya kijamii na mkewe Javeria Siddique, na kusababisha kizaazaa huku watumia mitandao wa Pakistan wakitaka kufahamu zaidi kuhusu hali iliyozingira kifo chake.

Waziri Mkuu wa Pakistan Shehbaz Sharif ametoa rambirambi zake kwa familia ya mwandishi huyo, huku familia yake na watu wengi wanaofutilia tukio hilo wakitaka kujua kilichotokea usiku wa Jumapili Oktoba 23, kuna maswali mengi kuliko majibu lakini haya ndiyo yanayofahamika hadi sasa kuhusu kifo cha mwanahabari huyo.

"Waliagizwa kusimamisha gari lao kwenye kizuizi katika usiku huo wa maafa, polisi wanadai kwamba mara baada ya kuingia katika barabara ya Kiserian-Magadi kutoka kwenye barabara ya vumbi, walitakiwa kusimama lakini wakakaidi." Taarifa zinasema.

Aidha, kilichofuata ni polisi kufyatua risasi ni taarifa za vyombo vya habari nchini humo vinavyodai kuiona taarifa ya polisi kuhusu tukio hilo

**POLISI KUCHUNGUZA**

Baada ya habari kuhusu kifo cha Sharif kuenea ,polisi nchini Kenya wameanza uchunguzi kuhusu mauaji yake.

Msemaji wa polisi Bruno Shioso anasema wanachunguza hali iliyosababisha kifo cha mwanahabari huyo.

Aidha, Mamlaka Huru ya Kusimamia Polisi nchini Kenya (IPOA) inasema imeanzisha uchunguzi kuhusu mauaji ya mwanahabari mashuhuri wa Pakistani Arshad Sharif.

Vyombo vya habari vya ndani viliripoti kwamba kuuawa kwa Sharif na polisi ni kisa cha utambulisho usio sahihi na kwamba IPOA, chombo cha kiraia, kiliundwa kufuatilia kazi ya polisi.

Mkuu wake, Ann Makori, amewaambia waandishi wa habari katika mji mkuu, Nairobi, kwamba timu maalum ya kutafuta majibu ya haraka imetumwa kuchunguza mauaji ya mwandishi huyo.

Kifo chake kimewashtua wengi hasa nchini Pakistan, mwanahabari huyo aliyeshinda tuzo alipinga vikali maendeleo ya kisiasa yanayoendelea nchini Pakistan.

Sharif mbobezi katika uandishi wa habari za uchunguzi alishughulikia matukio mengi ya kisiasa nchini mwake kwa mashirika ya habari ya kitaifa na kimataifa.

Sharif, mkosoaji mkali wa serikali ya Pakistan, aliondoka nchini humo mapema mwaka huu baada ya msururu wa kesi za uchochezi kuwasilishwa dhidi yake.

Chama cha waandishi wa habari nchini Pakistan kinataka uchunguzi kuhusu kifo chake ufanyike na watu wengi nchini humo kupitia mitandao ya kijamii wameelezea kushangazwa na hali iliyosababisha kifo chake na kutaka uchunguzi kufanyika. **MITANDAO**

ZIARA YA TSHISEKEDI

# Congo na imani kwa Tanzania ndiyo baba wa uchumi wa DRC

• Kitovu bandari ya DSM ikiitumia kwa hali zote

**NA GAUDENSIA MNGUMI**



Rais Samia Suluhu Hassan akiagana na mgeni wake Rais wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo Félix Tshisekedi , kwenye uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere Jijini Dar es Salaam baada ya kukamilisha ziara yake. **PICHA: IKULU**

JUNI 2019, ilikuwa ziara ya kwanza ya kiserikali kwa Rais Felix Tshisekedi tangu achaguliwe kuwa Rais wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, kuitembelea Tanzania.

Wakati huo anatinga nchini na kukutana na Rais John Magufuli, katika kipindi ambacho DRC ilihitaji Tanzania kuiunga mkono na kushirikiana na raia wake mpya.

Felix Tshisekedi aliyeapishwa Januari, 2019 baada ya kushinda kwenye uchaguzi wa kidemokrasia akikabidhiwa kijiti na mstaafu Joseph Kabila, ni dhahiri kiongozi huyo anaelekea kumaliza kipindi cha muhula wa kwanza na DRC inatarajiwa kufanya uchaguzi mkuu mwaka 2023, wakati huu anapoitembelea Tanzania.

Katika ziara yake ya kwanza ya kiserikali tangu achaguliwe kuwa Rais wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo mwaka 2019, anakutana na Rais John Magufuli, na tangu wakati huo ziara zake zinabaki kuwa muendelezo wa ukweli kuwa DRC na Tanzania zina historia ndefu katika ushirikiano.

Aidha, mikutano ya viongozi wa mataifa hayo inalenga kujadili shughuli za kiuchumi kati ya nchi hizo mbili ikiwamo kutumia Bandari ya Dar es Salaam na kuinua biashara za mipakani.

DRC ni miongoni mwa nchi zinazotumia bandari ya Dar es Salaam kwa hali zote ikiwa ni pamoja na kuagiza shehena nje ili kuziuza Congo na pia kusafirisha bidhaa zake kwenda nje na hilo ni suala la msingi kwa uchumi wa Congo.

Aidha, pamoja na usafirishaji wa bandari ya Dar -es- Salaam na kutumia bandari kavu, suala la kuimarisha miundombinu ya mawasiliano inayofanikisha biashara na uwekezaji wa taifa hilo nalo halikwepeki.

**AMANI /USALAMA**

Tanzania imekuwa mshirika wa Congo hata kabla ya ujio wa Rais Felix Tshisekedi madarakani na imekuwa na msaada mkubwa kwenye ulinzi wa amani nchini humo.

Hilo linaweza kuonekana kama DRC haiwezi kuiacha Tanzania pembeni ni jirani wa muhimu zaidi ambaye licha ya kupata msiba kufuatia kushambuliwa wanajeshi wake waliokuwa wanalinda amani nchini DRC haikuwaondoa wanajeshi hao.

Kwa kuthamini uwepo wa amani Tanzania iliahidi kusaidia juhudi za kulinda amani tena ikiahidi kuwa itawaondoa mara tu amani ya kudumu itakapopatikana nchini humo, kauli na msimamo huo ukitolewa na Rais wa wakati huo John Magufuli.

Wakati wa awamu ya tano ya John Magufuli, walinda amani 30 waliokuwa DRC chini ya Mpango wa Umoja wa Mataifa 'MONUSCO,' walishambuliwa na kuuliwa, lakini bado iliendelea na ushiriki wa kutafuta amani .

Tanzania imeendelea kuunga mkono juhudi za kuleta amani kwa sababu siyo tu kwamba nchi hiyo inahitaji uhakika wa amani na utulivu lakini inaamini kuwa amani ni muhimu na kitu cha lazima kinachochochea maendeleo ya kiuchumi kati ya nchi za Maziwa Makuu , ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na Ukanda wa Kusini mwa Afrika (SADC) ambako mataifa hayo yanakutana.

Ndiyo maana hata katika ziara ya hivi karibuni Rais wa Congo, amesisitiza kuwa suala la usalama limejitokeza pia kwenye mkutano wa viongozi Rais Samia Suluhu na mwenzake wa DRC .

Wanasema kuna umuhimu wa pande zote mbili kuendelea kuimarisha amani Rais Tshisekedi akisisitiza kuwa kunapokosekana amani la usalama fursa nyingine za maendeleo nazo zinatoweka.

**MIRADI KIMKAKATI**

Ujio wa Rais Félix Tshisekedi, wa hivi karibuni, unalenga pia kujadili miradi mikubwa ya miundombinu kama vile reli ya standard gauge (SGR) na ujenzi wa barabara kuu inayoiunganisha Tanzania na DRC.

Masuala hayo ya kiuchumi yanachukua nafasi kubwa wakati Rais Samia Suluhu Hassan, anapomkaribisha mwenzake wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo jijini Dar- es- Salaam.

Ujenzi wa reli ya kisasa inayojengwa kuanzia Kigoma, kupita Burundi na hatimaye Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo ni suala la kipaumbele mbali na kuboresha miundombinu, Rais Samia Suluhu Hassan, anasema wanazingatia pia eneo la ukuzaji biashara pamoja na teknolojia kwenye ushirikiano wa sasa.

Ujenzi na maendeleo ya bandari ya Kibirizi katika Ziwa Tanganyika na miradi mingine kadhaa kama hatua zaidi za kukuza biashara kati ya Tanzania na DRC ni mambo ya kipaumbele wakati wa ziara za kiongozi huyo ambaye anaiona Tanzania kama lango kuu la kibiashara, kiuchumi, uwekezaji , mshirika wa kupata amani Congo na pia mdau wanayezungumza lugha moja kwenye masuala ya mshikamano na maendeleo.

Wakati wa ziara ya hivi karibuni zipo taarifa kuwa kumekuwa na kudorora kwa biashara kati ya nchi hizo mbili kwa miaka 10 iliyopita na lengo la sasa ni kubadili hali hiyo.

Rais Samia anasema, wako tayari kupokea wanachama wa jumuiya ya wafanyabiashara kutoka Congo na tayari wapo wengine kutoka Tanzania ambao kwa sasa wanafanya biashara huko, ikiwa ni pamoja na kwenye miradi mikubwa ya kilimo.

Rais wa Congo anaamini kuwa Afrika inaweza kuzibaini shida na changamoto zake na kuzitafutia suluhisho la kusaidia nchi hizo na bara kwa nguvu ya amani, ushirikiano na uhusiano mwema baina ya mataifa ili kusonga mbele na amekuwa na uhusiano mwema na majirani hasa Tanzania.

> Tanzania imekuwa mshirika wa Congo hata kabla ya ujio wa Rais Felix Tshisekedi madarakani na imekuwa na msaada mkubwa kwenye ulinzi wa amani nchini humo.

DRC inaitazama Tanzania kama 'kaka mkubwa' mshirika 'namba wani' kwenye jukumu la kufanikisha ujenzi wa miundombinu ya kimkakati kama uwekezaji mkubwa katika kuboresha Bandari ya Dar- es- Salaam, SGR, lakini pia kujenga bandari za Kigoma, Kibirizi na Karema katika Ziwa Tanganyika, ambazo ni njia muhimu za usafirishaji na kuimarisha biashara baina ya nchi hizo.

Ujenzi wa bandari hizo ni muhimu kwa kuwa ndiyo ufunguo wa biashara za mipakani kwenye eneo lote la Maziwa Makuu, ndiyo maana linapewa kipaumbele ili kuongeza ushiriki wa sekta binafsi na wafanyabiashara wa soko kubwa la Afrika Mashariki ambalo Congo ina sehemu kubwa kwenye kufanikisha.

Idadi ya sasa ya watu wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo ni 95,832,889 (milioni 96) kwa mujibu wa makisio ya mtandao wa 'Worldometer ' hivyo taifa hilo lenye takribani watu milioni 100 ni muhimu kwenye maendeleo ya Afrika Mashariki na Ukanda wa SADC.

# Bilionea Rishi Sunak anapoahidi uadilifu mkubwa kwa Waingereza

**• Ni mdogo kuliko mawaziri wakuu waliotawala miaka 200 iliyopita**

**Na Mwandishi Wetu**

RISHI Sunak ameahidi kuitumikia Uingereza kwa "uadilifu na unyenyekevu" mkubwa, ahadi anayoitoa muda mfupi baada ya kushinda kinyang'anyiro cha uongozi wa Chama cha Conservative na kuwa Waziri Mkuu wa Uingereza mtarajiwa, mwanzoni mwa wiki hii.

Akiwa na umri wa miaka 42, anakuwa Waziri Mkuu mwenye umri mdogo kuliko wote anayeliongoza taifa hilo katika zaidi ya miaka 200 iliyopita , akichukua nafasi ya Liz Truss, ambaye alijiuzulu wiki iliyopita.

Mwanasiasa Sunak sasa ndiye kiongozi wa Conservative na atakuwa Waziri Mkuu baada ya Liss kujiuzulu akiongoza kwa siku 44 na kuandika historia.

Sunak anakuwa mshindi baada ya mshindani wake Penny Mordaunt kujitoa katika dakika za mwisho baada ya kukosa kura 100 zinazomuunga mkono.

Rishi Sunak ambaye ni mmoja wa wanasiasa matajiri zaidi nchini Uingereza, na ambaye atakuwa kiongozi wa kwanza wa taifa hilo asiye Mzungu akiwa na asili ya India, anatajwa kuwa ni muumini wa dini ya Kihindu, ambaye sasa anasubiriwa kuunda serikali na kuanza mchakato wa kuinusuru Uingereza yenye mdororo mkali wa karibu kila kitu.

Wakati wa uongozi wa Boris Johnson, ambaye alijiondoa kwenye kinyang'anyiro cha uwaziri mkuu wa Uingereza, Sunak alikuwa Waziri wa Fedha.

**AHADI KWA WAINGEREZA**

"Ningependa kutoa pongezi kwa Liz Truss kwa utumishi wake wa umma wa kujitolea kwa nchi. Ameongoza kwa heshima na weledi kwa wakati wa mabadiliko makubwa na ndani ya hali ngumu ya kipekee, ndani na nje ya nchi.

"Ninanyenyekea na kuheshimu kupata uungwaji mkono wa wabunge wenzangu na kuchaguliwa kuwa kiongozi wa Chama cha Conservative na Unionist. Kwangu ni bahati kubwa maishani mwangu kuweza kutumikia chama ninachokipenda na kurudisha heshima na kwa taifa linalonidai."

Waziri Mkuu wa zamani Boris, aliyekuwa amejiondoa kwenye kinyang'anyiro cha uwaziri mkuu, alikuja kwa gia kubwa kutaka kurejea tena lakini mambo yakawa magumu na akaamua kujiweka pembeni na kumpaisha waziri wake wa fedha.

Baadhi ya wadadisi walieleza kuwa aliondoka kwa vile wengi hawakumuunga mkono na inawezekana kilichomuondoa madarakani miezi miwili iliyopita ambacho ni kuwa mdanganyifu kwa bunge na serikali kilibakiza doa lisilofutika kiasi kwamba hakuna uwezekano wa kiongozi ambaye hakuwa mwaminifu kuanza kuaminika na kuaminiwa tena.

Itakumbukwa kuwa miezi miwili iliyopita Sunak alishindwa katika harakati zake za kukiongoza chama cha Conservative lakini sasa hali imebadilika kwa kutangazwa kuwa mkuu wa chama hicho baada ya Boris aliyetizamwa kuwa mshindani wake mkuu kutangaza kujiondoa kwenye kinyang'anyiro hicho usiku wa kuamkia Jumapili.



Boris Johnson Waziri Mkuu wa zamani, alitamani tena jukumu hilo wiki iliyopita lakini akajiondoa kwenye mchakato na sasa anabakia kuwa mstaafu.

> Wakati wa uongozi wa Boris Johnson, ambaye alijiondoa kwenye kinyang'anyiro cha uwaziri mkuu wa Uingereza, Sunak alikuwa Waziri wa Fedha.



Waziri Mkuu mpya wa Uingereza Rishi Sunak kwa ujasiri akijiandaa kuelekea ofisi yake iliyoko 10 Downing Street jijini London kuanza kazi. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

Kazi ya kusaka Waziri Mkuu mpya ilitokana na Liz Truss kujiuzulu Alhamisi wiki iliyopita na kusababisha tena chama chake kuingia kazini kusaka kiongozi na kwa mujibu wa katiba yao , mshindi anatakiwa kuungwa mkono na wabunge wasiopungua 100 wa chama cha Conservative kwa njia ya kura na sasa mikoba ya Lizz amepewa Sunak.

Katika harakati za kuwania uongozi mpinzani mwingine wa Sunak alikuwa Penny Modaunt ambaye alijiengua na kueleza kuwa ushindi wa Sunak ni kama uamuzi wa kihistoria, ambao kwa mara nyingine umeonyesha kipaji kilichoko ndani ya chama chao na kuongeza kuwa anamuunga mkono Rish kikamilifu.

Kwa mujibu wa Idhaa ya Kiswahili ya DW, Mwenyekiti wa chama cha Conservative Jake Berry, anatoa wito kwa 'chama chote' kuungana na kuwa nyuma ya Sunak, wakati akijiandaa kuanza kazi ya kukabiliana na changamoto zilizo mbele yao kama taifa la Uingereza.

Wito wa kumuunga mkono Sunak, Berry anautaja akisema wakati wa mijadala ya ndani umeisha na kwamba anajua chini ya uongozi wa Rish Sunak, wanaweza kutekeleza mambo ya kipaumbele kwa watu wa Uingereza.

Sunak aliyezaliwa mwaka 1980 na mwenye miaka 42 na waziri wa zamani wa fedha, anakuwa waziri mkuu wa tatu wa Uingereza katika kipindi cha chini ya miezi miwili, akikabiliwa na jukumu la kurejesha utulivu katika taifa linalopambana na machafuko ya kisiasa na kiuchumi kwa miaka kadhaa.

Mambo mengine yakitokana na uamuzi wa kujiondoa kwenye uanachama wa Umoja wa Ulaya (EU) kupitia mchakato wa British Exit, maarufu Brexit.

DW, inakumbusha kuwa mtangulizi wa Sunak, Lizz aliangushwa na mpango wake wa kiuchumi uliosababisha mtikisiko katika masoko ya kifedha, kupandisha gharama za maisha kwa wapigakura na kuwakasirisha wengi ndani ya chama chake.

Mwanamama huyo mtaalamu wa fani ya uchumi na filosofia, alitumia mbinu kadhaa zikiwamo kupunguza nguvu ya sarafu ya Pauni ya Uingereza ili kuwezesha kufanyika biashara zaidi, lakini juhudi hizo ziliambulia patupu akaachia ngazi.

Hata hivyo chini ya mfumo wa bunge wa Uingereza pamoja na mawaziri wakuu kadhaa kuachia ngazi taifa hilo halihitaji kufanya uchaguzi mkuu mpya hadi mwishoni mwa 2024 na chama tawala ndicho kitakachoendelea kuubeba msalaba huo , aidha Sunak amesema hana mpango wa kuitisha uchaguzi mpya. Lakini ikielezwa na wachambuzi kuwa endapo angeuitisha huenda chama cha upinzani cha Labour kingeiangusha Conservative.

**ALIKOTOKA**

Ni mzaliwa wa Southampton Uingereza wazazi wake ni Wahindu waliozaliwa Afrika mama Tanzania na Baba Kenya, Sunak ni mmoja wa wanasiasa matajiri zaidi wa Uingereza. Kabla ya kuingia bungeni kwa mara ya kwanza mwaka wa 2015, Sunak alifanya kazi kwa bilionea, Goldman Sachs, aidha alifanyia kazi benki ya uwekezaji na kampuni kubwa ya fedha.

Mkewe, Akshata Murty, ambaye alikutana naye alipokuwa akisoma katika Chuo Kikuu cha Stanford, ni binti wa mmoja wa wajasiriamali mabilionea akiwekeza kwenye Teknolojia ya Habari na Mawasiliano -TEHEMA nchini India.

Ni msomi wa filosofia (falsafa) na uchumi akijifunza katika Chuo Kikuu cha Oxford . Mwaka 2009 alifunga ndoa na mwanamitindo Akshata Murty, binti wa bilionea Narayan Murty wa India.

Tangu 2015 amekuwa mbunge wa Chama cha Conservative na ilipofika 2020 alikuwa Waziri wa Fedha, lakini 2022 alijiengua akitaja sababu kuwa ni kutokuelewana baina yake na bosi wake Waziri Mkuu Boris Johnson. **MITANDAO**

JUKWAA LA VIONGOZI

TOM JOSEPH MBOYA

# Shujaa wa uhuru, maendeleo ya Kenya aliyezawadiwa kifo

• Alichangia kusoma Hussein Obama, Maathai

**NA MWANDISHI WETU**

THOMAS Joseph Mboya, maarufu Tom Mboya alizaliwa Agosti 1930 na kuuawa Julai 1969, alikuwa mmoja wa wanaharakati wa kupambana kutafuta uhuru wa Kenya.

Aliongoza majadiliano ya kufikia muafaka wa Kenya kujipatia uhuru katika ukumbi wa "Lancaster House" nchini Uingereza na alishiriki kikamilifu kukiimarisha chama cha KANU, kilicholikomboa taifa hilo kutoka kwenye ukoloni wa Waingereza.

Busara za Mboya, pamoja na jitihada za uongozi wake, zilimfanya akubalike na viongozi wengi duniani. Alitoa hotuba na kuhudhuria katika midahalo mbalimbali pamoja na kushiriki katika mahojiano kadhaa katika nchi mbalimbali kwa ajili ya kupambania Kenya ili ipate uhuru.

Mwaka 1958, akiwa na umri wa miaka 28, Mboya alichaguliwa Mwenyekiti wa mkutano wa wajumbe wawakilishi kutoka nchi mbalimbali barani Afrika ulioandaliwa na Kwame Nkrumah wa Ghana.

Alisaidia kuimarisha harakati ya vyama vya ushirika nchini Kenya, Uganda na Tanzania na pia katika mataifa mengine ya Afrika, alipata nguvu hizo za kimadaraka kutokana na kuwa mwakilishi wa Ushirika wa Umoja wa Kimataifa wa Biashara Huria.

Ilipofika mwaka 1959, Mboya aliitisha mkutano huko Lagos -Nigeria ambako walianzisha chama cha wafanyakazi wa Afrika kilichojulikana kama "All-Africa ICFTU".

Mboya aliwahi kufanya kazi pamoja na John F. Kennedy na Martin Luther King Jr.ambapo walifanikiwa kuzalisha fursa za elimu kwa wanafunzi wa Afrika, jitihada hizo zilifungua milango kwa Kennedy katika kipindi cha miaka ya 1960 ya kutoa nafasi kwa vijana wa Afrika kwenda kusoma katika vyuo vikuu vya Marekani. Walionufaika na fursa hiyo ni pamoja na Wangari Maathai na Hussein Obama baba mzazi wa Barack Obama aliyekuwa Rais wa Marekani.

**ELIMU YAKE**

Mboya alipata elimu kupitia shule mbalimbali za madhehebu ya Kikatoliki na mwaka 1942, alijiunga sekondari akisoma zaidi Lugha ya Kiingereza na Historia. 1946, aliendelea na kidato cha tano na sita ambako ufaulu wake ulimwezesha kusajiliwa katika mitihani mingine ya Cambridge.

Ilipofika mwaka 1948, alijiunga na chuo cha "Royal Sanitary Institute's Medical Training School" akifanyakazi ya bwana afya jijini Nairobi, alihitimu mafunzo hayo mwaka 1950. Alipata fursa nyingine ya masomo Afrika Kusini ambako alisomea masuala ya uchumi mwaka 1955, alijiongeza na kupata nafasi ya masomo zaidi nchini Uingereza katika teknolojia ya kuendesha viwanda.



Tom Mboya mwanasiasa aliyefanikisha kwa asilimia 100 uhuru wa Kenya. Aliuawa kabla ya kufurahia matunda ya uhuru. **PICHA: MTANDAO**

**KUJIUNGA NA SIASA**

Maisha ya kisiasa yalianza mara baada ya kuajiriwa na halmashauri ya jiji la Nairobi mwaka 1950 akiwa bwana afya wa jiji, alipochaguliwa kuwa rais wa umoja wa Waafrika ambao muda si mrefu umoja ulianzisha chama cha 'Kenya Local Government Workers' Union.'

Aliacha kazi ya ubwana afya na kuendelea na shughuli za chama cha wafanyakazi wa Kenya akiwa Katibu Mkuu, kabla ya kwenda tena Uingereza masomoni.

Mwaka 1953, wakati wa vita vya kutafuta uhuru vilivyoongozwa na Mau Mau ya Jomo Kenyatta pamoja na viongozi waandamizi wengine wa Kenya walikamatwa na kuwekwa ndani.

Mboya aliombwa kuiongoza KAU (iliyokuwepo kabla ya KANU) na akashauriwa kuendeleza jitihada za kutafuta uhuru. Hata hivyo serikali ya mkoloni ikakipiga marufuku chama hicho, lakini Tom akatumia chama cha wafanyakazi kupigania uhuru.

Alichaguliwa tena kuwa katibu mkuu wa chama hicho cha KFL na kutokana na nafasi hiyo, alihutubia mikutano mbalimbali nchini Uingereza pamoja na mingine iliyofanyika New York, Marekani na kuanzisha maandamano na migomo mbalimbali nchini Kenya kudai maslahi bora kwa wafanyakazi.

Mwaka 1956, baada ya Mboya kurejea kutoka nchi za Ulaya, serikali ya kikoloni ilitoa kibali cha Mwafrika yeyote kuteuliwa na kufanya kazi katika Baraza la Kutunga Sheria.

Alichaguliwa kutoka Kenya na akawa Katibu Mkuu wa jopo la "African Elected Members Organization" - AEMO, na akaendeleza juhudi zake za kutafuta Uhuru wa Kenya, wakati huo huo alikuwa akipata ushauri kutoka kwa Mzee Jomo Kenyatta pamoja na wanasiasa wengine waliokuwa gerezani.

Aliunda chama cha Nairobi Peoples Convention wakati huo, akiwa na mahusiano ya karibu na Kwame Nkrumah wa Ghana ambaye kama alivyokuwa Mboya, alikuwa mpambanaji.

Mwaka 1958, wakati wa mkutano wa viongozi wa vyama mbalimbali vya ukombozi Afrika uliofanyika nchini Ghana, na ambao uliitishwa na Kwame Nkrumah, Mboya alichaguliwa kuwa mwenyekiti wa mkutano huo.

Mwaka 1960, utaratibu wa kuwafadhili wanafunzi wa Afrika kwenda kusoma Marekani uliongezeka kupitia jitihada za Kennedy Foundation baada ya Mboya kuwasiliana naye alipoomba msaada, kutoka hatua hiyo, nafasi zaidi zikatokea kwa wanafunzi kutoka Uganda, Tanganyika na Zanzibar, Zambia, Zimbabwe na Malawi.

> Mwaka 1953, wakati wa vita vya kutafuta uhuru vilivyoongozwa na Mau Mau ya Jomo Kenyatta pamoja na viongozi waandamizi wengine wa Kenya walikamatwa na kuwekwa ndani.

Ilipofika 1961, Jomo Kenyatta na Oginga Odinga waliachiliwa huru kutoka gerezani, ndipo chama chake kikajiunga na vyama vya Kenya African Union na Kenya Independence Movement na wakaviunganisha na kuanzisha chama kimoja cha Kenya African National Union (KANU), hatua hiyo ililenga kuwa na chama ambacho hakitakuwa na mwelekeo wa ukabila na pia viongozi wake walikuwa wakijiandaa kushiriki katika mkutano mkubwa wa Lancaster jijini London kujadili ujio wa uhuru wa Kenya.

Akiwa Katibu Mkuu wa KANU, Mboya aliongoza ujumbe wa Kenya katika mkutano huo wa Lancaster, na akapendekeza bendera ya taifa jipya la Kenya.

**BAADA YA UHURU**

Uhuru ulipopatikana aliteuliwa kuwa Waziri wa Kazi wa Kenya tangu 1962, aliteuliwa pia kuwa mbunge wa jimbo la Nairobi, ambalo sasa linafahamika kama jimbo la Kamukunji na akateuliwa kuwa Waziri wa Katiba na Sheria kuanzia Juni 1963, hadi Desemba 1964.

Alianzisha mfuko wa hifadhi ya jamii (NSSF), taasisi ya kijamii inayoshughuulikia matatizo ya kijamii mahala pa kazi, mahakama ya kazi ambayo ilijihusisha na matatizo yanayotokea maeneo ya viwandani.

Wakati Kenya ilipokuwa Jamhuri, Desemba 1964, Rais Kenyatta alimteua Tom Mboya kuwa Waziri wa Maendeleo na Mipango na akahamishia shughuli zote zilizokuwa zikifanyika Wizara ya Sheria kwenda Ofisi ya Mwanasheria Mkuu Charles Njonjo.

Ilipofika 1966,Tom Mboya alihamishwa kutoka Wizara aliyokuwa akiiongoza wakati huo huo Kibaki kwa mara ya kwanza aliteuliwa kuwa Waziri wa Biashara na Viwanda.

Matokeo ya mipango ya Wizara aliyoiongoza Mboya, yalikuwa chanya ya uchumi wa Kenya kuongezeka kwa asilimia saba katika kipindi cha uongozi wake.

**KUUAWA MBOYA**

Akiwa na miaka 38, na Waziri wa Uchumi, Mipango na Maendeleo, alipigwa risasi Julai 5, 1969 akiwa kwenye barabara ya Government Road sasa Moi Avenue, jijini Nairobi, wakati anatoka kutembelea duka la dawa.

Nahashon Njoroge alituhumiwa kwa mauaji na baada ya kukamatwa alifikishwa mahakamani na akakutwa na hatia na baadaye alinyongwa hadi kufa.

Matokeo ya mauaji ya Mboya yalisababisha maandamano katika miji ya Kenya na wakati wa mazishi yake Rais Kenyatta, alisema "uhuru wa Kenya ungepitia changamoto nyingi kama isingelikuwa jitihada nyingi na kujitoa kwa uimara kwa Tom Mboya." Sanamu ya Mboya iliwekwa katika mtaa wa Moi Avenue, sehemu alipouliwa, na mtaa wa karibu yake wa 'Victoria Street' ulipewa jina lake kwa kumbukumbu ya heshima yake.

# Ni kuchunguza watuhumiwa wanapoelekezwa si 'kulianzisha'

INATOKA UK. 13

hizo iwe ni kwa kungoja hadi taarifa za kiserikali zitolewe halafu wachukue hatua, kwa upande wa TAKUKURU au hadi waelekezwe kuchukua hatua, wanavyofanya ZAECA.

Licha ya kuwapo tofauti kati ya maelekeo hayo, kimsingi inafuatana na utamaduni wa kisiasa pande zote mbili ambako kwanza unaweka uzio wa kuchukua hatua kwa kusikiliza tuhuma za wapita njia au 'whistle blowers,' au wapiga filimbi kuashiria hali ya hatari.

Watoa taarifa wanaweza kutoka popote siyo lazima wawe ni wa serikalini. Inabidi tuhuma ziwe za kitaasisi, yaani serikali ikiri kuwa kuna tatizo kwenye eneo fulani.

### KENGELE KWA PAKA

Kwa vile mweleko huo umekuwepo muda wote, ina maana kuwa taasisi hizo zina kazi ya kuchunguza rushwa pale taasisi nyingine ya kiserikali au kiongozi wa ngazi ya juu akitoa maelekezo kufanya hivyo.

Ni wazi kuwa taasisi hizo kwa njia moja au nyingine zinakwepa 'kumfunga paka kengele' kwani wanaotuhumiwa wakati mwingine ni watu walioteuliwa na wanaoaminiwa na wakuu serikalini na wale wanaowaongoza katika taasisi hizo.

Kiutamaduni inabidi hatua ya kutaka ofisa fulani wa serikali achunguzwe kwanza maelekezo yatoke ngazi za juu, na siyo jitihada ya kipolisi kutoka TAKUKURU au ZAECA kumchunguza mteule.

Kimsingi ni wazi kuwa sheria inatakiwa kutazama mbali zaidi, kwa vile inaweza kuwa vigumu kusema fulani ana mwelekeo wa kula fedha za umma au anamiliki mali nyingi ambazo zinatia wasiwasi, kufanya hivyo kunaweza kutengeneza mazingira ya kiuhasama baina ya viongozi hao na TAKUKURU au ZAECA.

Ni kanuni ambayo haijaandikwa kokote pale ila ni sehemu ya jadi, kuwa kutwaa jukumu la kumtuhumu mtu akiwamo mteule ni kumtangazia vita, jambo ambalo linaibua maswali mengi.

Mara nyingi Jeshi la Polisi limekuwa na mwelekeo kama huo kutaka watu watoe taarifa za wale wanaopanga uhalifu huku au kule, lakini pia kuna hofu unaweza kuripoti taarifa za uhalifu na wahusika wakafahamu kuwa wewe ndiye chanzo, ndiyo maana wengi wanaogopa.

Maelezo na hatua zilizochukuliwa kwa mfano kuhusu kutoridhika kwa wazi kwa Rais Samia kuhusu inachofanya TAKUKURU ni kielelezo kuwa mtindo wa kuacha rushwa iendelee halafu kuzinduka kwa amri ya wakuu serikalini kuchunguza, inatakiwa kufanyiwa kazi.

Endapo serikali inataka taasisi ya kupambana na rushwa ifanye kazi kikamilifu kuna haja ya kuziangalia upya sheria na kuweka muundo wa kipolisi, yaani CID (upelelezi) halafu mkurugenzi wa mashtaka jinai (DPP) .

Ni kuondoa kinga ya kitaasisi, kufuta mshikamano wa taasisi za serikali, ili iwe ni taarifa mojawapo ya mtiririko wa kipolisi, kwa amri ya mkuu wa wilaya, waziri au ngazi nyingine kulingana na nini kimegunduliwa na katika mazingira gani.

Walio na kumbukumbu ya kuundwa kwa TAKUKURU awali ikiitwa TAKURU, wanafahamu kuwa serikali ya awamu ya tatu iliiboresha na kuipa jukumu zito kwa kuunda taasisi ya kuzuia na kupambana na rushwa itakayokuwa na ofisi wilaya zote nchini na juhudi zikafanikiwa.

Miaka takriban 20 baadaye hitaji la ufanisi katika kuzuia rushwa linarudisha swali hilo la awali, ni vipi serikali itaweza kuzuia rushwa ndiyo Rais Samia amegundua kuna walakini?

### KUBADILISHA UELEKEO

Kwa upande mmoja kuna suala la kuondoa mfumo wa idara maalum ya serikali ya kuwaumbua wenzao serikalini na kurudisha mfumo wa kipolisi ambao hasa ni kutoa mamlaka ya uchunguzi wa tuhuma kwa CID.

Njia anyingine ni kutoa hisa za mashirika yote 253 yanayotakiwa kutoa gawio serikalini kuwa na wanahisa tofauti, sekta binafsi ishike hatamu kuzuia upotevu wa fedha na kuhakikisha faida inapatikana.

Kadhailika walipe kodi stahili kwa masuala mengine yaliyobaki idara ya upelelezi (CID) iamue inaowataka kutoka taasisi hizo za kipelelezi, wafanye kazi ya kupambana na rushwa wakiwa na kinga ya kipolisi na kisheria na wafuatilie kila mahali kwa uchunguzi wa kina, kuwa na uthibitisho na kutenda haki na ufanisi ili kukabiliana na rushwa kwa utaratibu wa kisheria.




Rais Samia Suluhu Hassan akipokea Taarifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali kwa mwaka 2020/2021 kutoka kwa Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali (CAG) Charles Kichere, Ikulu Chamwino Jijini Dodoma. **PICHA: MTANDAO**

Dondoo: Kulia
1. Taifa lenye ushawishi duniani
6. fikira inayoeleza jambo fulani
8. mfuasi wa chama cha siasa
9. (,) 11.magonjwa
12.wafanyakazi wageni katika mashamba makubwa
16.hutagwa na ndege
17.ndege mla mizoga 18.uchokozi
20.hali ya kustarehe 21.dhamira
22.patia mtu msaada

Chini:
1. ajenda
2. ala ya ngozi ya kuwekea mishale
3. mwisho wa dunia
4. Itikadi
5. nuru
7. Oslo ni mji Mkuu
10.fanya mtu awe na nidhamu
11.mtu anayetabiri mambo kwa kutumia elimu ya nyota
13.filimbi 14.mapambo ya boma
15.chombo cha chuma cha kukaangia vitu 19.kaka wa Mama

## CHEMSHABONGO NA -00 17 00-


Na Felix Magezi
felixmagezi@gmail.com



Kamilisha jedwali kwa kujaza maneno yafuatayo:

NYAMAZA
THAMANI
NYUMBUKA
MAJIRA
MANATI
SAMADI
NIKAHA
SAHIHI
JUANA
MIMBA
RIAKA
ZANA
ADHA
AMAA

MBU
DIA
IDI
HAI
SOKA




Majibu toleo lililopita



| | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | M | | I | | B | | |
| | | | | G | E | N | D | E | R | I |
| | | | | A | | A | I | N | A | |
| | | | | H | A | M | A | K | I | |
| M | A | D | H | A | R | A | | I | S | I |
| | C | H | A | W | A | | | | | D |
| S | H | A | B | A | K | I | | B | | H |
| H | A | H | A | | A | S | M | A | R | A |
| A | M | A | | M | | I | T | A | | A |
| T | A | B | E | N | A | K | U | L | O | |
| I | | U | | O | | E | | I | | |

| | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| G | H | A | L | A | | B | | M |
| U | A | S | I | | K | A | D | A |
| M | I | M | B | A | | N | | U |
| U | B | A | Y | A | | D | U | A |
| | A | R | A | L | I | A | | J |
| K | | A | | I | | M | T | I |
| A | | | M | | R | A | I | |
| B | A | R | A | F | U | | M | |
| L | | | D | | D | | U | |
| A | N | G | A | L | I | W | A | |



# Uboreshaji wa masoko waanza

**Na Grace Mwakalinga, MBEYA**

UBORESHAJI wa miundombinu ya masoko ya mboga na matunda katika Jiji la Mbeya, umeanza kufanyika kama njia ya kulinda usalama wa chakula na afya za walaji.

Miundombinu hiyo ni pamoja na ujenzi wa vizimba bora vya kuuzia mboga na matunda ili kuhakikisha chakula kinachoingizwa na kuliwa jijini Mbeya kinakuwa safi na salama.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya jana, Juma Homera, alisema jana kuwa vizimba 270 vinatarajiwa kujengwa kwenye masoko hayo ambayo ni ya kimkakati kama vile Soweto, Uhindini, Igawilo na Uyole.

"Uboreshaji wa miundombinu hiyo utasaidia kuongeza thamani ya mboga na matunda ili kukidhi vigezo vya walaji wa ndani na nje ya nchi, licha ya kuongeza thamani ya bidhaa hizo lakini itasaidia kulinda usalama wa watumiaji kwa sababu itatolewa kwenye mazingira salama," alisema Homera.

Mmoja wa wafanyabiashara hao, Agness Isambi, alisema uboreshaji wa miundombinu ya soko hilo utapandisha hadi soko hilo na kuonekana la kimataifa hali itakayochangia kupata wateja kutoka maeneo mbalimbali ndani na nje nchi.

Alisema miundombinu hiyo itasaidia kukabiliana na majanga ya moto pindi yanapotokea.

Mwenyekiti wa Soko la Soweto, Shadhil Bashiru, aliomba serikali kwa kushirikiana na Shirika la Ricolto, kujenga vizimba vya bidhaa nyingine sokoni hapo na sio tu mboga na matunda kama ilivyofanyika kwa sasa.

Alisema miundombinu ya vizimba kwa wafanya biashara sokoni hapo ikiboreshwa itachangia kuongeza pato kwa Halmashauri ya Jiji la Mbeya pamoja na wajasiriamali kujikwamua kiuchumi.

Mratibu wa Mradi wa AGRI CONNECT kupitia Shirika la RICOLTO, Shukuru Tweve, alisema ni mradi wa mboga na matunda unaotekelezwa katika mikoa mitano ya nyanda za juu kusini kama vile Mbeya na Iringa.

Alisema vizimba vya mbao ambavyo vilikuwa vikitumika awali vilikuwa kikwazo katika kupata mikopo kwenye taasisi za kifedha na kwamba vizimba hivyo vipya ambavyo vimejengwa kisasa vitasaidia kupata mikopo.

Mradi huo wa ujenzi wa vizimba vya kisasa vya mboga na matunda unasimamiwa na Shirika la Rikolto kwa kushirikiana na Chemba ya Wafanyabiashara, wenye Viwanda na Kilimo (TCCIA) na Jiji la Mbeya kwa ufadhili wa Umoja wa Ulaya.

# Chanzo ongezeko ukatili wanaume chatajwa

**Na Grace Mwakalinga, MBEYA**

KUKOSEKANA kwa chombo cha kutetea haki za wanaume, kumechangia ongezeko la vitendo vya ukatili wa kijinsia dhidi yao, imeelezwa.

Hali hiyo imeelezwa kusababisha baadhi yao kuchukua sheria mkononi na kufanya matukio ya kutisha yakiwamo kuua au kujiua.

Baadhi ya wadau wa haki za binadamu mkoani Mbeya wamesema kama kungekuwapo chombo cha kutetea haki za wanaume, ingesaidia kundi hilo kupaza sauti zao na kuripoti vitendo mbalimbali vya ukatili wanavyofanyiwa kwenye jamii inayowazunguka.

Mratibu wa Kanda wa Chama cha Wanasheria Wanawake Tanzania (TWLA), Wakili Latifa Ayoub, alisema jana kuwa amekuwa akipokea malalamiko mengi kutoka kwa wanaume wakidai kunyanyaswa na wake zao kwenye ndoa lakini linapokuja suala la kufanyiwa uamuzi, huogopa na kutoa ushirikiano.

Alisema aibu na woga kwa wanaume huchangia kwa kiasi kikubwa kushindwa kuchukua hatua kutokana na vitendo vya ukatili wanavyofanyiwa na wake zao na kusababisha kuchukua maamuzi magumu.

Kongamano la wanaume wa mkoa wa Mbeya limeandaliwa mahususi kwa ajili ya kutoa nafasi kuzungumza kwa pamoja masuala mbalimbali yanayowakabili na namna ya kuyatatua.

Mjumbe wa Bodi kutoka Taasisi ya Empower Youth Prosperity, Joseph Mbilinyi, maarufu kama Sugu, alisema kinachosababisha wanaume wengi kufa mapema ni msongo wa mawazo ambao huchangiwa na kukaa na vitu moyoni muda mrefu.

Alisema kongamano hilo limebeba maudhui mbalimbali ikiwamo kutoa fursa kwa wanaume kupaza sauti zao kuhusu vitendo vya ukatili elimu ya afya ya akili, fursa za kiuchumi na burudani.

"Tunahitaji na sisi wanaume tuwe na sehemu yetu ya kusemea mambo tunayofanyiwa ya ukatili wa kijinsia, elimu juu ya afya ya akili nayo ni muhimu sana kwa sababu tunakaa na vitu moyoni kwa muda mrefu baadae kusababisha maamuzi magumu ambayo yanagharimu maisha yetu, utofauti wetu na wanawake ni kwamba wenyewe hawakai na vitu moyoni, wana vyombo vya kuripoti," alisema Sugu. Mkurugenzi wa Empower Youth Prosperity (EYP), Ipyana Mwakyusa, alisema kongamano la wanaume jijini Mbeya ambalo litafanyika Novemba 20, mwaka huu, litatoa nafasi kujadili kwa pamoja masuala mbalimbali yanayowahusu kama vile kujikwamua kiuchumi, burudani na elimu ya afya ya akili.

Alisema kwa miaka mitano sasa taasisi hiyo imekuwa ikiandaa makongamano mbalimbali kwa ajili ya kuwakutanisha wanaume wa mkoa wa Mbeya na maeneo mengine kujadili kwa pamoja masuala mbalimbali yanayowahusu.

"EPY kwa kushirikiana na wadau mbalimbali watazungumza na wanaume wa jijini Mbeya kuwajengea uwezo wa kukabiliana na vikwazo kama vile afya ya akili na vitendo vya ukatili msimu huu kongamano letu limebeba ujumbe usemao "BRO FUNGUKA" na sema bila woga kauli hii inalenga kumtoa mwanaume katika kifungo cha ukimya na imani ya kuficha magumu anayokumbana nayo," alisema Mwakyusa.



Aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Mbeya Mjini, Joseph Mbilinyi 'Sugu' (katikati), akisalimiana na wananchi wakati akipita eneo la Igawilo, jijini Mbeya juzi. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Wahadhiri wapeana mbinu kusaidia wanafunzi

**Na Grace Mwakalinga, MBEYA**

WANATAALUMA wa Chuo Kikuu Kishiriki cha Katoliki Mbeya (CUCoM), wamekutana kwa lengo la kujifunza mbinu mbalimbali za kuwasaidia wanafunzi wa chuo hicho kupata ujuzi na maarifa ya namna ya kukabiliana na soko la ajira la ndani na nje ya nchi.

Mafunzo hayo yalikuwa na lengo mahusussi la kuwajengea uwezo wa namna ya kuwafundisha wahadhiri kinadharia na vitendo ili baada ya kuhitimu waweze kukidhi mahitaji ya ajira.

Profesa Kalafunja Useki wa Chuo Kikuu cha Mtakatifu Augustino ni miongoni mwa watoa mada kwa walimu hao ambaye alisema wamefanya hivyo baada ya kubaini asilimia kubwa ya vijana wanaomaliza elimu ya juu hawana ujuzi na maarifa ya kujiajiri au kumudu ushindani wa soko la ajira ndani na nje ya nchi.

Kutokana na kukosekana kwa ujuzi na maarifa vijana wengine wamebakia kuilalamikia serikali kwamba haitoi ajira jambo ambalo sio lengo la elimu ya vyuo vikuu.

Aliongeza kuwa walimu hao pia wamejengewa uwezo wa namna ya kufundisha kidigitali na kwamba mabadiliko ya sayansi na teknolojia yamesaidia kurahisisha utoaji wa elimu, hivyo ili kuendana na kasi watajitahidi kuzingatia suala hilo kwa madai ya kupunguza mzigo wa upatikanaji wa vitu vya kujisomea wanafunzi kupitia mitandao.

Chuo chetu kimejipanga kuwafundisha wanafunzi wetu kigitali na kuwaongezea ujuzi na maarifa ambao utawasaidia kuwa wabobezi na mahiri wa masomo wanayotaka, jukumu letu ni kuwatengenezea mazingira rafiki ili watimize ndoto zao alisema Prof. Kalafunja Usaki.

Profesa Euleria Temba, Naibu Mkuu wa CUCoM (Taaluma), alisema mbali na kuwaandaa vijana kwa kuwapatia ujuzi na maarifa, pia wanawafundisha tabia njema kama vile utii, uaminifu, upendo na uzalendo.

Alisema wanafanya hivyo ili kuwasaidia vijana hao kuepukana na tabia mbaya ambazo zinaweza kuharibu ndoto za maisha yao kama vile, uvutaji bangi, umalaya, unywaji wa pombe na wizi.

Mdhibiti Ubora wa Chuo hicho, Elisha Kwiga, alisema wamejiandaa vyema kuwapokea wanafunzi wapya ambao wanatarajia kuanza masomo Oktoba 28, mwaka huu.

Alisema ni utaratibu wa chuo hicho kuwajengea uwezo wanataaluma namna bora ya kuwafundisha wanafunzi na kwamba wanafanya hivyo ili kuwasaidia kutimiza majukumu yao ipasavyo ya kuhakikisha wanafunzi wanaandaliwa kushindana kwenye soko la ajira.





# CBT: Mabilioni ya Rais Samia Suluhu yamesaidia mzunguko wa biashara

**Na Paul Mabeja, DODOMA**

BODI ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko (CBT), imesema Sh. bilioni 150 zilizotolewa na Rais Samia Suluhu Hassan zimesaidia kuongeza mzunguko wa biashara kutoka Sh. bilioni 15 kwa mwaka 2021 hadi Sh. bilioni 52 mwaka 2022.

Mkurugenzi wa CPB, Dk. Anselm Moshi, alibainisha hayo juzi wakati akizungumza na waandishi wa habari juu ya vipaumbele vya taasisi hiyo kwa mwaka huu wa fedha.

"Katika kipindi hiki ambacho Rais Samia amekuwa madarakani CPB imepata mafanikio makubwa ikiwamo kutoa kibali cha kukopa fedha kutoka katika Benki ya Biashara ya CRDB kama mtaji ili tuweze kuendesha shughuli zetu na kuhakikisha wakulima wanapata masoko ya uhakikika wa mazao yao.

"Haya ni mafanikio makubwa na yakujivunia, kupitia fedha tulizonazo tumefanya uwekezaji wa kujenga kiwanda kikubwa cha kukoboa mpunga jijini Mwanza. Hadi sasa kinafanya kazi na wakulima wa kanda ya ziwa wamepata soko la uhakika," alisema.

Aidha, Dk. Moshi alisema katika kuhakikisha wakulima wanakuwa na masoko ya uhakika CPB imejipanga kuongeza uwezo wa kuhifadhi mazao kutoka tani 122,800 inayohifadhi hadi tani 600,000 ifikapo mwaka 2025.

Alisema, kutokana na ongezeko la uhifadhi kutaiwezesha CPB kuongeza uwezo wa kununua na wakulima watapata masoko ya uhakika ya mazao.

"Mkakati mwingine ni kuhakikisha wakulima wanalima kwa tija ili wapate mazao mengi ya matumizi ya nyumbani na kwa ajili ya biashara na sasa tumeanza kuajiri maofisa ugani ili wawasimamie wakulima waweze kutumia mbinu za kisasa katika shughuli zao lengo ni kuongeza uzalishaji,"alisema.

Kuhusu ngano alifafanua kuwa CPB imesaidia wakulima kuzalisha ngano kwa tija kupitia mpango wa kilimo mkataba katika mikoa ya Manyara, Kilimanjaro na Arusha.

Alisema CPB imejenga kiwanda cha ngano Arusha ambacho kwa mwaka kinasaga tani 36,000.




Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko (CPB), Dk. Anselm Moshi, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dodoma jana, kuhusu utekelezaji wa shughuli mbalimbali za bodi hiyo na mwelekeo wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2022/2023. **PICHA: PAUL MABEJA**

## Simbachawene awaita wawekezaji kuwekeza Dodoma

**Na Paul Mabeja,DODOMA**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu, George Simbachawene ametoa wito kwa jamii kuwekeza mkoani Dodoma kwa kuzingatia fursa zilizopo.

Alitoa wito huo juzi jijini hapa wakati wa ziara ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria ilipotembelea maendeleo ya ujenzi wa Mji wa Serikali Mtumba Jijini Dodoma.

Akieleza majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu Waziri Simbachawene alisema ofisi yake inajukumu la kuratibu na kusimamia mradi wa ujenzi wa majengo ya wizara na taasisi zake, hivyo atahakikisha unasimamiwa kwa weledi na kukamilika kwa wakati.

"Hadi sasa ujenzi umefika asilimia 50 hadi 80 kwa baadhi ya majengo na kwa upande wa miundombinu ya barabara, nishati, maji na mawasiliano ipo vizuri hivyo nitoe rai kwa wananchi kutumia fursa zilizopo ili kuwekeza Dodoma," alisema Simbachawene.

Aliongezea kuwa uwapo wa mji wa serikali itasaidia kurahisisha utoaji wa huduma kwa wananchi kwa wepesi zaidi.

"Mji huu ndiyo utafanikisha na kurahisisha shughuli za serikali kwa urahisi kwani kila wizara itakuwa hapa na itafikika kwa wepesi na niwakaribishe wananchi kuja kupata huduma mahali hapa," alisema

Mwenyekiti wa Kamati hiyo Dk. Joseph Mhagama, aliipongeza serikali kwa namna inavyowezesha ujenzi wa Mji huo kwenda kwa kasi.

"Ninampongeza Rais Samia Suluhu Hassan, amekuwa mstari wa mbele katika kuendeleza Mji wa Dodoma na Kamati imeridhishwa na maendeleo ya ujenzi hivyo ninawapongeza Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kufanya kazi kwa weledi,"alisema Dk. Mhagama.

Mjumbe wa kamati hiyo Asha Abdallah alitoa pongezi kwa kazi kubwa inayofanywa na serikali. huku akiwaasa Watanzania kutumia mji huo katika kupata huduma kwakuwa unafikika kwa wepesi.

# Serikali kuwapiga msasa watoa huduma Afya 3,000

**Na Ibrahim Joseph, DODOMA**

SERIKALI inatarajia kutoa mafunzo kwa watoa huduma wa afya msingi 3,000 ili waweze kuzuia magonjwa yasiyoambukiza kwenye maeneo yao.

Mkurungenzi wa Huduma za Tiba kutoka Wizara ya Afya, Prof. Paschal Ruggajo, alisema hayo juzi wakati akitoa hotuba ya kufungua mafunzo ya kuzuia na kudhibiti magonjwa yasiyoambukizia awamu ya nne kwa watoa huduma wa mikoa minne yaliyofanyika jijini hapa jana.

Prof. Ruggajo alisema katika kukabiliana na magonjwa yasiyoambukiza serikali inakusudia kutoa mafunzo kwa watoa huduma wa afya msingi wapatao 3,000 ili kuboresha kiwango cha huduma hizo hapa nchini.

"Moja kati ya mipango mikakati iliyopo ni kuimarisha huduma za msingi kwa kuvijengea uwezo vituo vya afya 600 kwa kuwapa mafunzo watoa huduma za afya msingi 3,000 kutoka mikoa 26 ifikapo Desemba 2023,"alisema.

Alibainisha kuwa tayari watoa huduma 577 wameshajengewa uwezo kutoka vituo vya afya 138 katika mikoa mitano kwa awamu ya kwanza, pili na ya tatu.

Kadhalika alisema, mafunzo hayo yanategemea kuwafika watoa huduma afya ili kuboresha kiwango cha huduma za kinga, tiba na huduma utengamao za magonjwa hayo kuanzia ngazi ya jamii hadi taifa.

Alisema, mafunzo hayo pia yataongeza ufanisi katika kutoa elimu kwa wananchi wanaokwenda kwenye vituo vya kutolea huduma za afya ili wachukue tahadhari ya kuepuka vichocheo vya magonjwa hayo yasiyoambukiza

Meneja Mpango wa Taifa wa Kuzuia na Kuthibiti Magonjwa Yasiyoambukiza, Afya ya Akili na Ajali, Valeria Millinga alisema mkakati huo unatekelezwa kwa kuzingatia vipaumbele vya mpango mkakati wa mwaka 2012 mpaka 2026.

Millinga alisema mafunzo hayo katika awamu ya kwanza na pili yalifanyika Desemba 2021 na jumla ya watoa huduma 33 kutoka Mkoa wa Dar es Salaam na Pwani walijengewa uwezo kwa watoa huduma 150 wa vituo vya afya 43.

Alisema, awamu ya tatu wakufunzi 53 kutoka mikoa saba ambayo ni Kilimanjaro, Arusha, Songwe, Dodoma, Singida, Kigoma na Lindi na wataalamu kutoka ngazi za hospitali za wilaya na mikoa waliwezeshwa mafunzo na wizara ya afya.

Aliongeza kuwa awamu ya nne ambayo mafunzo yake yalifunguliwa juzi jijini hapa yanashirikisha watoa huduma 400 kutoka katika vituo vya afya 94 vya mikoa minne.

Aliitaja mikoa hiyo kuwa ni Lindi, Kigoma, Dodoma na Songwe ambayo wanajengewa uwezo wa elimu hiyo ya kudhibiti magonjwa hayo yasiyoambukiza.

Pia alisema, wanakusudia kuwajengea uwezo wakufunzi 68 ngazi ya mkoa kutoka mikoa 17 ambayo ni Geita, Mwanza, Simiyu, shinyanga, Kagera, Manyara, Tabora, Iringa, Mbeya, Njombe, Rukwa, Katavi, Ruvuma, Mtwara, Morogoro na Tanga.

Mkurugenzi Msaidizi Huduma za Magonjwa Yasiyoambukiza Afya ya Akili na Ajali, Dk. James Kiologwe alisema pamoja na mafunzo hayo lakini watu wanatakiwa kujenga tabia ya kufanya mazoezi na kula vyakula visivyo na mafuta mengi ili kuepuka magonjwa yasiyo ya kuambukiza.



## Jaji Mkuu ataka kasi ya kusikiliza kesi iongezwe

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

JAJI Mkuu wa Zanzibar, Khamis Ramadhan Abdalla, amezitaka mahakama kuongeza kasi ya kusikiliza mashauri mbalimbali yanayowasilishwa na wananchi ili haki itendeka na hukumu kutolewa kwa wakati.

Jaji Ramadhan alisema hayo jana alipokuwa Mkoa wa Kaskazini Unguja katika ziara ya kuangalia watendaji wa mahakama na shughuli zao.

Alisema, kwa upande wa Mahakama ya Ardhi, serikali imeongeza nguvu kwa kuteua watendaji wa mahakama hiyo baada ya kujitokeza kwa malalamiko mengi ya kurundikana kwa kesi za migogoro ya ardhi.

Alisema mahakama ni sehemu ya kimbilio la wananchi kuona matatizo yao yanapatiwa ufumbuzi ikiwamo kusikilizwa mashauri yao kwa wakati.

"Tulikuwa tunakabiliwa na changamoto kubwa katika mahakama ya ardhi ambayo hivi karibuni imepata watendaji wake na kuongezewa mahakimu ambapo matarajio yetu changamoto zilizopo zitafanyiwa kazi haraka," alisema.

Naye Mrajisi wa Mahakama Kuu ya Zanzibar, Valantina Andrew Katema, alisema wameongeza kasi ya kushughulikia mashauri mbalimbali ikiwamo yaliyokwama na kuchukua muda mrefu bila ya kusikilizwa.

Alisema kupitia maboresho yanayoendelea kutekelezwa na Mahakama Kuu ya Zanzibar, matarajio yao makubwa ni kuona kwamba kasi ya kusikilizwa kwa kesi ni kukamilika kwa uchunguzi.

Ahiyo kuipongeza serikali ya Zanzibar, kutekeleza ahadi zake kwa kutoa gari kwa ajili ya kurahisisha shughuli za usafiri kwa watendaji wa mahakama ikiwamo katika mahakama zilizopo mikoani.

# Jamii kuelimishwa kuhusu matumizi mazuri ya kimtandao

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

KATIKA kuadhimisha mwezi wa uelimishaji wa usalama mtandao, Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari Tanzania kwa kushirikiana na wadau wengine imeanza kutoa elimu kwa jamii hasa vijana kuhusu matumizi mazuri ya kimtandao.

Akizungumza jana baada ya utoaji wa elimu hiyo katika chuo cha Institute of Continuing and Professional (ICPS), Mkurugenzi Msaidizi sehemu ya usalama wa mtandao kutoka wizara hiyo, Injinia Steven Wangwe, alisema elimu hiyo imelenga kwa wanafunzi kwa sababu ndio watumiaji wakubwa wa mitandao bila ya kujua madhara yake.

Alisema, wanafunzi wamezungukwa na jamii na kwamba watakua mabalozi kufikisha elimu hiyo kwa watu wengine ili kuepuka matumizi mabaya ya mtandao.

"Leo tumekuja hapa kwa sababu tunalenga wanafunzi na wao ndio watumiaji wakubwa, lakini pale ambapo wanafunzi hawa wanatumia bila ya kufahamu mambo yatakayowasababisha madhara," alisema.

Alisema kuna matukio mengi ya udhalilishaji mtandaoni, kwa watu wenyewe kujirusha mitandaoni kwa kutoa taarifa zao za siri au wanaofanya hivyo kwa kukusudia na kurushwa katika mitandao.

Alisema kuna changamoto kubwa ya uhalifu wa kimtandao ikiwamo uporaji wa akaunti na wahalifu hutumia mwanya huo kwa matumizi mabaya ya kimtandao.

Aliwataka wananchi kutokutoa taarifa zao za siri katika mitandao ili kuepuka uhalifu wa kimtandao ambao utasababisha madhara kwao.

Alisema, katika kusaidiana kupunguza uhalifu wa kimtandao hasa wa kitapeli, ni vyema kupiga simu namba 15040 na kutoa taarifa sahihi ili hatua stahiki zichukuliwe.

Alisema, katika kuadhimisha mwezi wa uelimishaji wa kimtandao kutakuwa na kongamano la kitaifa la Tehama litakalofanyika leo visiwani Zanzibar ambalo litawakutanisha wataalamu wa Tehama na kutoa elimu ya usalama wa mtandao kongamano ambalo litafunguliwa na Rais wa Zanzibar, Dk. Ali Hussein Mwinyi.

Naye, mtaalamu wa masuala ya usalama kimtandao na uchunguzi, Yussuf Kileo, aliwataka vijana kuepukana na uhalifu wa kimtandao.

"Mitandao ina tabia ya kuhifadhi kumbukumbu hivyo kuhakikisha wanachokiandika au kukituma mitandaoni kiwe ni kizuri kisochokuwa na madhara ili kuwa na kumbukumbu nzuri," alisema.

Aliwataka vijana kuwa makini na utapeli mtandaoni na kila muathirika wa uhalifu wa mtandao kutoa taarifa kituo cha polisi kilicho karibu naye ili hatua stahiki zichukuliwe.

Kwa upande wao wanafunzi wa chuo hicho wamepongeza elimu waliyopatiwa ambayo itawasadia katika matumizi sahihi na mazuri ya kimtandao.

Ibrahim Fadhil, mmoja wa wanafunzi hao alisema changamoto kubwa anayokabiliana nayo ni utapeli wa kimtandao wa kutumiwa ujumbe mara kwa mara kupitia simu yake ya mkononi kutakiwa atume fedha (tuma fedha kwa namba hii) bila ya kufahamu mtumaji wa ujumbe huo.

Kaulimbiu ya mwezi wa uelimishaji wa usalama mtandaoni ni "Usalama wa kimtandao unaanza kwa mtu binafsi".




Mkurugenzi Msaidizi Idara ya Usalama wa Mtandao kutoka Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mhandisi Steven Wangwe, akizungumza na waandishi habari baada ya kutoa elimu ya usalama wa kimtandao kwa wanafunzi wa Chuo cha Elimu Endelevu na Mafunzo ya Kitaaluma (ICPS), Chukwani Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Thamani usafirishaji bidhaa nje yapungua

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

BIDHAA zilizosafirishwa nje ya nchi kwa mwezi Septemba mwaka huu zilikuwa na thamani ya Sh. bilioni 27.6 na kupungua kwa asilimia 50.8 ikilinganishwa na mwezi Agosti, mwaka huu.

Hayo yalielezwa jana na Sharih Khatib Faki, kutoka Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali kitengo cha biashara na kodi, Idara ya Takwimu za kiuchumi wakati akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake Mazizini nje ya mji wa Zanzibar.

Alisema kundi la vyakula na wanyama hai linaongoza kwa kuchangia asilimia 96.1 ya thamani yote ya usafirishaji wa bidhaa hizo.

Alisema, usafirishaji huo kwa nchi tano zilizoongoza kwa mwezi wa Septemba umefikia asilimia 95.1 ya thamani ya bidhaa zote zilizosafirishwa.

Alizitaja nchi hizo kuwa ni Singapore inayo ongoza kwa bidhaa zenye thamani ya Sh. milioni 15,949.4 ikifuatiwa na Indonesia, Vietnam, Denmark na Falme za Kiarabu.

Alisema, thamani ya bidhaa zilizoagizwa nje ya nchi imeongezeka kwa asilimia 26.1 ikilinganishwa na mwezi wa Septemba mwaka 2021 ambayo imepunguwa kwa asilimia 9.9 ikilinganishwa na mwezi wa Agosti mwaka huu.

Alisema, bidhaa zilizoagizwa kwa mwezi wa Septemba mwaka huu zina thamani ya Sh. bilioni 111.3 na kundi la madini ya mafuta na vilainishi limechangia asilimia 39.6 ya bidhaa zote zilizoagizwa.

Alisema, nchi za Umoja wa Falme za Kiarabu zimeongoza kwa bidhaa zenye thamani ya Sh. bilioni 52.5 sawa na asilimia 47.2.

Naye Dk Ulrick Mumburi kutoka Benki Kuu ya Tanzania, alisema kuwa benki hiyo inahakikisha inaweka fedha za kigeni za kutosha kwa ajili ya kuagiza bidhaa kutoka nje ya Tanzania.





## ‘Vituo vya mafuta 12 Kanda ya Ziwa havina bima ya majanga’

**Na Vitus Audax, MWANZA**

VITUO 12 kati ya 121 vya kuuza mafuta ya petroli na dizeli vilivyokaguliwa Kanda ya Ziwa vimebainika vinajiendesha bila kuwa na bima ya majanga kama sheria za nchi zinavyotaka.

Ukaguzi wa vituo hivyo ulifanywa hivi karibuni na Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati na Maji (EWURA) kwa kushirikiana na Mamlaka ya Usimamizi wa Sekta ya Bima Nchini (TIRA).

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Mwanza baada ya kufunguliwa mafunzo kwa wadau wa sekta ya bima Kanda ya Ziwa, Meneja wa TIRA Kanda ya Ziwa, Richard Toyota, alisema ukaguzi huo ulilenga kujua hali ya halisi ya namba ya vituo hivyo, ikiwamo kukidhi kigezo cha kukata bima ya majanga.

Alisema ni kosa kisheria vituo hivyo kujiendesha bila ya kuwa na bima na kwamba kazi ya TIRA ni kuhakikisha inasimamia sheria ya bima.

Aliongeza kuwa baada ya kazi hiyo kufanyika, EWURA ndiyo wenye jukumu la kuvichukulia hatua vituo hivyo ambavyo vimebainika kuwa kasoro hizo.

Akizungumzia sekta ya bima kwa kanda ya ziwa, Toyota alisema bado inahitaji msukomo wa elimu ili jamii ijue umuhimu wake.

Aidha, alisema lengo la sekta hiyo ni kuhakikisha inachangia pato la taifa kwa asilimia tano kutoka asilimia 1.68 ya sasa.

Toyota alisema bado jamii haijapata elimu ya kutosha ili kujua umuhimu wa kukata bima hususani bima ya maisha.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Usimamizi wa TIRA, Aboubakary Ndwata, alisema sekta ya bima ni muhimu kwa taifa na wananchi wake na kwamba jamii nzima inahusika

Aidha, alizitaka kampuni za bima kulipa kamisheni mawakala wao ambao wanaendesha shughuli hizo kwa asilimia 80 ili kuhakikisha sekta ya bima inasonga mbele.

“Kampuni nyingi hazilipi kamisheni kwa mawakala wao, hatua hii ni mbaya kwa sababu inaturudisha nyuma badala ya kusonga mbele,” alisema.

Mafunzo hayo yalihusisha viongozi wa kampuni za bima, mawakala, TIRA pamoja na benki mbalimbali.

# Wanafunzi msingi wadaiwa kunajisiwa wakienda chooni

**Na Marco Maduhu, SHINYANGA**

WANAFUNZI wa kike katika Shule ya Msingi Town Manispaa ya Shinyanga, wamedaiwa kuviziwa na kunajisiwa na baadhi ya vijana wanapokwenda kujisaidia nyakati za usiku kutokana na shule hiyo kutokuwa na uzio.

Mwalimu Mkuu wa shule hiyo, Meshaki Helmani aliyasema hayo juzi wakati wa mahafali ya darasa la saba.

Alisema kuwa vitendo hivyo vinasababishwa na shule hiyo kukosa uzio ikiwa ipo maeneo ya mjini. Helmani alisema pia hali hiyo inasababishwa na shule hiyo kuwa na mwingiliano mkubwa wa watu ambao ni pamoja na wajasiriamali ambao hutumia vyoo vya wanafunzi kujisaidia na kutumia nafasi hiyo kuwavizia wanafunzi hao.

“Shule hii ipo katikati ya mji na haina uzio hali ambayo imekuwa ikisababisha wanafunzi wetu hasa wa kike wanapokwenda kujisaidia hukutana na vijana chooni na kufanyiwa vitendo vichafu vya kiukatili,” alisema Helmani.

Hivyo aliiomba serikali pamoja na wadau wengine wa maendeleo kusaidia tatizo hilo la ujenzi wa uzio ili wanafunzi wawe salama.

Alisema katika shule hiyo wanafunzi 147 wamehitimu elimu yao ya msingi, wasichana wakiwa 79 na wavulana 68.

Meneja wa Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) mkoani Shinyanga Mhandisi Mibara Ndilimbi, ambaye alikuwa mgeni rasmi katika mahafali hayo aliahidi kuanza ujenzi wa uzio katika shule hiyo, huku akitoa wito kwa wadau wa maendeleo kumuunga mkono, ili kuweka mazingira salama ya wanafunzi kusoma na kutimiza ndoto zao.




Meneja wa Ofisi, Mazingira, Jamii na Utawala wa Orca Energy Group, Rebecca Framp (kushoto), akiwa na watoto wa Shule ya Awali ya Songo Songo, iliyojengwa na Kampuni ya PanAfrican Energy (PAET), baada ya kukagua miradi mbalimbali ya maendeleo inayogharamiwa na kampuni hiyo, ili kusaidia jamii ya wananchi wanaoishi katika kisiwa hicho mkoani Lindi hivi karibuni. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# NMB yatenga bil. 5.9/- kukopesha wakulima wa tumbaku

**Na Neema Sawaka KAHAMA**

BENKI ya NMB Tawi la Kahama mkoani Shinyanga imetenga Sh. bilioni 5.9 kwa ajili ya kuwakopesha wakulima wa tumbaku kwa kupitia vyama vya msingi kwa msimu wa mwaka 2022/2023.

Akizungumza na Nipashe katika mahojiano maalum, Meneja wa NMB Tawi la Kahama, Gadiel Sawe, alisema malengo yao ni kuvifikia vyama 25.

Sawe alisema mpaka sasa NMB imeshawakopesha wakulima kupitia vyama vya msingi 15 vya wakulima wa zao la tumbaku.

“Wakulima wa zao la tumbaku wanakopeshwa kutokana na matatizo wanayopitia ya uandaaji wa kuni, bani za kuchomea na kuweka mbolea katika shamba, shughuli zote zinahitaji kuwa na fedha,” alisema Sawe.

Sawe alisema msimu wa mwaka 2021/2022 walikopesha vyama vya msingi 22 kwa kutoa mkopo wa Sh. bilioni 4.5 kwa wakulima wa zao la tumbaku katika halmashauri hiyo.

Alieleza kuwa wakulima wamekuwa wakiwafuata maeneo walipo na kuwapatia elimu ya mkopo na namna gani watakavyorudisha baada ya mavuno na kuuza.

Akizungumza na Nipashe Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Festo Kiswaga, alisema wakulima wa tumbaku watagawiwa bure mbegu za zao hilo kwa lengo la kuinua zao hilo wilayani humo.

# Rishi Sunak akutana na Mfalme Charles III

**LONDON, Uingereza**

Rishi Sunak amekuwa waziri mkuu wa 57 wa Uingereza baada ya kualikwa na Mfalme Charles kwa ajili ya kuunda serikali.

Atakuwa waziri mkuu wa tatu mwaka huu kujiuzulu na ataingia Downing Street kama Waziri Mkuu mdogo zaidi katika karne mbili nchini humo.

Katika hotuba yake ya kwanza kama waziri mkuu, Sunak alisema daima atamshukuru Boris Johnson kwa mafanikio yake ya ajabu kama waziri mkuu.

Sunak alisema serikali yake itakuwa na uadilifu, weledi na uwajibikaji katika kila ngazi. "Uaminifu hupatikana pale nitapata chako," alisema.

Aidha, mkutano wa Mfalme Charles na waziri mkuu mpya, Rishi Sunak, unaashiria makabidhiano ya mfano ya mamlaka, katika mchanganyiko wa sherehe na myumbisho wa kisiasa.

Rishi Sunak amekuwa Waziri mkuu mpya wa Uingereza, akichukua wadhifa huo kutoka kwa Truss. Anarithi changamoto kadhaa kutoka kwa mtangulizi wake.

Mhariri wa BBC wa masuala ya uchumi Faisal Islam, alisema Sunak aliingia katika ofisi namba 10 , baada ya kutoa ahadi mbali mbali, lakini pia alionywa kuhusu kupanda haraka kwa bei za bidhaa .

Changamoto kuu kwake itakuwa ni kutafuta hakikisho la bei ya nishati, mfumo wa ruzuku kusaidia nyumba na biashara kukabiliana na gharama za umeme na gesi.

Aidha, Nick Triggle, alisema huku idadi kubwa ya watu wakisubiri kupata matibabu ya hospitalini na tisho la migomo kuhusu malipo na kipindi cha msimu wa baridi ukikikaribia, Sunak atalazimika kukabiliana na moto kuanzia siku ya kwanza ofisini.

***BBC***



Mfalme Charles wa Uingereza akimkaribisha Waziri Mkuu mpya, Rishi Sunak, jana katika makazi yake ya kifalme kwa ajili ya kujitambulisha. **PICHA: REUTERS.**

## Watu 11 wauawa baada bweni kuungua moto

**KAMPALA, Uganda**

Polisi nchini Uganda imesema watu 11, miongoni mwao wakiwa ni wanafunzi, wamefariki na wengine sita wakiwa katika hali mahututi baada ya bweni kuungua moto.

Tukio hilo lilitokea juzi katika shule ya watoto wasioona iliyopo Mukono, mashariki mwa mji mkuu wa nchi hiyo Kampala.

Majeruhi wanatibiwa katika hospitali ya Herona, polisi ilisema.

Uchunguzi umeanza kubaini chanzo cha moto huo uliotokea katika shule ya wasioona ya Salaam ambao unasemekana uliibuka mapema asubuhi Jumanne.

Visa vya mioto inayoibuka shuleni ni ya kawaida nchini Uganda, wakati mwingine chanzo chake huwa ni mishumaa inayowaka katika mabweni baada ya kuzimwa kwa taa za shule.

Juhudi za kudhibiti moto mara kwa mara hukwamishwa na wingi wa watoto kupindukia katika mabweni ya kulala.

***BBC***

## Israel yaua Wapalestina sita

**JERUSALEM, Palestina**

WIZARA ya Afya ya Mamlaka ya Palestina, imesema watu sita wameuawa na wengine karibu 20 wamejeruhiwa jana kufuatia oparesheni ya jeshi la Israel katika ukingo wa Magharibi.

Kulingana na wizara hiyo, awali iliripoti vifo vya watu watatu na majeruhi 19, watatu kati yao wakiwa na hali mbaya baada ya kupigwa risasi na wanajeshi wa Israel.

Waziri Mkuu wa Israel Yair Lapid, alisema kuwa Wadih Al Houh, kiongozi wa kundi la wanamgambo wa Kipalestina lililopewa jina la "Pango la Simba" alikuwa miongoni mwa waliouawa katika mji wa Nablus kaskazini mwa ukingo wa Magharibi.

Jeshi la Israel lilisema limefanya oparesheni iliyojumuisha polisi na maofisa wa ujasusi wakilenga eneo linalotumiwa na viongozi waandamizi wa kundi la "Pango la Simba.

***DW***

**Kulingana na wizara hiyo, awali iliripoti vifo vya watu watatu na majeruhi 19, watatu kati yao wakiwa na hali mbaya baada ya kupigwa risasi na wanajeshi wa Israel.**

## Kimbunga chaua 16 Bangladesh

**DHAKA, Bangladesh**

WATU 16 wamekufa baada ya kimbunga Sitrang kupiga Bangladesh na kulazimisha watu wapatao milioni moja kuhama makazi yao.

Maofisa walisema watu milioni 10 hawakuwa na umeme katika wilaya 15 za pwani, huku shule zikifungwa katika mikoa ya kusini na kusini magharibi.

Jebun Nahar, ofisa wa serikali ameliambia shirika la habari la AFP kuwa watu 14 wamepoteza maisha, wengi wao walikufa baada ya kuangukiwa na miti, wakati wawili walikufa baada ya mashua yao kuzama katika mto Jamuna ulioko sehemu ya kaskazini.

Mvua kubwa ilinyesha katika sehemu kubwa ya taifa hilo na kusababisha mafuriko katika miji ya Dhaka, Khula na Barisal ambayo imeshuhudia mvua kubwa tangu juzi.

***DW***

## Wabunge Korea Kusini wasusa

**SEOUL, Korea Kusini**

WABUNGE wa upinzani nchini Korea Kusini, wamesusia hotuba ya kwanza ya bajeti ya Rais Yoon Suk-yeol katika bunge.

Hatua ya wabunge hao ni kuonyesha kupinga uchunguzi wa kihalifu dhidi ya kiongozi wa upinzani.

Yoon alielezea pendekezo la bajeti yake ya dola za Kimarekani bilioni 445 katika bunge lililokuwa nusu tupu. Wabunge wa chama cha Democratic na ambacho kina wingi wa wabunge katika bunge lenye viti 300 walisusia hotuba hiyo.

Serikali ya kihafidhina ya Yoon itahitaji uungwaji mkono wa chama cha Democratic ili kufadhili mipango ya serikali ya kuufufua uchumi ulioporomoka kutokana na janga la Corona na kujibu vitisho vya nyuklia vya Korea Kaskazini. Muda wa mwisho wa kupitisha bajeti hiyo ni Desemba 2. Upinzani ulikasirishwa na hatua ya waendesha mashtaka waliovamia makao makuu yake mjini Seoul kama sehemu ya uchunguzi wa muda mrefu kwa sakata la ufisadi

***DW***

## Rais wa Ujerumani awasili Ukraine

**KYIV, Ukraine**

WAKATI mashambuzi ya Russia yanazidi kuisambaratisha Ukraine, Rais wa Ujerumani, Frank Walter Steinmeier amewasili nchini humo kama ishara ya kuiunga mkono.

Rais Steinmeier aliwasili jana katika mji mkuu wa Ukraine wa Kyiv, Shirika la habari la Reuters limeripoti.

Ziara yake haikutangazwa kabla jambo ambalo ni la kawaida kwa maofisa wa Magharibi wanapokwenda katika mji mkuu huo wa Ukraine tangu vita vilipoanza.

Steinmeier ana uhusiano mgumu na Rais Volodymyr Zelensky, ambapo wengi nchini Ukraine wanamchukulia kama mwanasiasa anayeunga mkono Russia, na miezi michache iliyopita alifahamishwa kuwa Waukraine hawataki kumuona mjini Kyiv.

Kulingana na kituo cha televisheni cha NTV ya Ujerumani , mkutano baina ya Steinmeier na Zelensky ulifanyika jana.

Shirika la habari la Ufaransa AFP, baadaye liliripoti kuwa msemaji wa Steinmeier alithibitisha kuwasili kwake mjini Kyiv na nia yake ya kukutana na Rais Zelensky.

***BBC***

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**SHABANI MAGANGA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha sita chenye index namba S1375-0663 kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia NEW ERA HIGH SCHOOL mwaka 2017. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **DAR/CHU/RB/415862/2022**

## KUPOTEA KWA CHETI



**GRACE GOODLUCK URASSA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba S.018/011 kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **KISARAWE LUTHERAN JUNIOR SEMINARY** mwaka 2019. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **DAR/MAG/RB/16642/2022**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA NGARA, KAGERA**

**MAOMBI NA.03/2022**

**VAILETH PASCHAL DOMISIAN……………….MWOMBAJI**

**DHIDI YA**

**PASCHAL DOMISIAN**
**BARAKA WILFRED……………………….WAJIBU MAOMBI**

**KWA; PASCHAL DOMISIAN NA BARAKA WILFRED**

Mnaarifiwa kuwa kesi Na.03/2022 imepangwa kutajwa tarehe 25.11.2022 mbele ya Mwenyekiti wa Baraza, P.J. Makwandi saa 2.00 asubuhi, mahala-Ngara.

Hivyo, Mnaamuriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa.Msipohudhuria Baraza litasikiliza shauri upande mmoja dhidi yenu.

AMRI hii imetolewa kwa mkono wangu na MUHURI wa Baraza hii leo tarehe 25.10.2022

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA
NGARA

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**TAARIFA YA KUSIKILIZWA RUFAA MAHAKAMA ZA WILAYA YA TANGA**

**SHAURI LA RUFAA YA NDOA NA… 12… LA… 2022…**

**ZERA WILLIAM OWINO……….MUOMBA RUFAA**

**DHIDI YA**

**MORIS ODONGO OMINGO………….MJIBU RUFAA**

**Kwa ………MORIS ODONGO OMINGO**

Fahamu kwamba tarehe 2/11/2022 saa 2:30 asubuhi ndiyo siku ya kusikilizwa kwa rufaa iliyotajwa hapo juu. Siku hiyo ikiwa ni lazima ulete hati zote zinazohusu shauri hilo kwa ajili ya kujitetea katika shauri hilo. Naambatanisha nakala ya sababu za rufaa alizoleta muomba rufaa. Tarehe 13 mwezi **OKTOBA 2022**

HAKIMU MKAZI MFAWIDHI
WILAYA YA TANGA.
RESIDENT MAGISTRATE
TANGA
…. nimepokea nakala ya taarifa

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya TEMEKE**
**Kituo cha JUMUISHI Mkoa DAR ES SALAAM**
**Usimamizi wa Mirathi Na. 2050/2022**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU MLEKWA MUSSA SALUM**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA SHAMSA ABDALLAH OMARY**

**TANGAZO**
**(Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 29 Mwezi wa 11 Mwaka 2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;** Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.

**Imetolewa leo tarehe 24 Mwezi wa 10 Mwaka 2022.**

HAKIMU

**FORM NO. 58**
**IN THE COURT OF DISTRIC T DELEGATE OF MOROGORO**
**DISTRICT AT MOROGORO**
**PROBATE AND ADMINISTRATION**
**CAUSE NO 115 OF 2022**

**In Matter of the Estate of the Late RICHARD SAMSON SEKWAO**

**By 1. NICKSON RICHARD SEKWAO**
**2. ………………………………**

All Person claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or latter of administration) is made to the above - named petitioner.

Objection to the grand should be field on or before the 14 day of November / 2022.

Dated at Morogoro, this 25th day of OCTOBER 2022

RESIDENT MAGISTRATE

**FOMU YA MIRATHI-2**
**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO KIHONDA**
**WILAYA YA MOROGORO**
**MKOA MOROGORO**

**Usimamizi wa Mirathi Na. 57/2022**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHENU HAMISI ABED SAID WA MADUKA KUMI KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOTOLEWA NA THERESIA LUWEBE LIAGANE**

**TANGAZO**
(Kanunu ya 5 (2) kanuni za usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 31 / Mwezi 10 Mwaka 2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Zingatia;

Endapo kuna yeyeto mwenye Wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.

* Wosia wa Marehemu huyu upo Mahakamani na waweza kukaguliwa
* Marehemu hakuacha wosia
* Futa isiyohusika

**Imetolewa leo tarehe 24 mwezi 10 mwaka 2022**

HAKIMU

Kwa Habari Motomoto Usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku

Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676

OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.




# YOUNG HANA TABU NA TUNDA

**Na Mwandishi Wetu**

MSANII wa Bongo Fleva, Young Dee, amesema kwamba anakuwa na amani kubwa kuona mpenzi wake wa zamani akiwa na furaha.

Young Dee, amesema hayo katika mahojinao na EATV akimzungumzia mpenzi wake ambaye ni nyota wa muziki huo.

Young alikuwa katika mahusiano na Cappuccino Tunda ambaye kwa sasa yupo kwenye mapenzi na msanii wa singeli, Meja Kunta na amesema anapenda kumuona akiwa na furaha.

Amesema, yeye ni muumini wa kupenda kuona mtu aliyeachana naye ana furaha bila kuangalia yupo na nani.

"Mimi ni mtu ambaye napenda kukuona unakula hata kama hatuli wote. Wewe kula huko kivyako mimi sina tatizo," alisema Young.

## NAY WA MITEGO AMKATAA GIGY MONEY

**Na Mwandishi Wetu**



RAIS wa Kitaa, Nay Wa Mitego, amekana kuwahi kutoka kimapenzi na msanii, Gigy Money, akisema huenda watu wanahisi hivyo kutokana na uropokaji wa kauli zake.

Nay Wa Mitego amesema ukaribu wake na Gigy Money umesababishwa baada ya kumtumia kama 'Video Vixen' wa ngoma yake ya Akadumba wakati anasoma sekondari.

"Nakumbuka Gigy Money alicheza kwenye video yangu ya Akadumba na naweza kusema ndiyo iliyomtambulisha kwenye tasnia hiyo, wakati huo alikuwa anasoma sekondari kule Jitegemee kama sikosei alikuwa kidato cha pili au tatu," alisema Nay katika mahojiano na kipindi cha Friday Night Live cha EATV.

"Labda ananitaka, lakini mimi sijawahi kuwa kwenye mahusiano naye, halafu si unajua Gigy anaropoka sana."

## ABDUL KIBA AKOSHWA NA HARMONIZE

**Na Mwandishi Wetu**

MSANII Abdul Kiba amemmwagia sifa msanii mwenzake wa Bongo Fleva, Harmonize baada ya kutumbuiza kwenye shoo mkoani Mtwara.

Mtwara ndio nyumbani kwao Harmonize na Abdul Kiba, ambaye ni mdogo wa Ali Kiba kutoka Lebo ya Kings Music, alikuwa na shoo katika mji huo.

Alifurahia mapokezi ya mashabiki ambao walimkaribisha jukwaani kwa mbwembwe na kuimba pamoja naye nyimbo zake alipokuwa anatumbuiza.

Kikubwa kilichowateka watu ni pale alipoamua kuimba wimbo wa Harmonize 'Amelowa' jukwaani na umati wa watu ukamshangilia kwa nguvu.

Baadaye alipomaliza kutumbuiza alifanya mahojiano na waandishi na kuzungumzia kitendo chake cha kuimba wimbo wa Harmonize, ambapo aliweka wazi kwamba anamkubali sana msanii huyo bosi wa Konde Music na kukiri kuwa ana kipaji kikubwa sana kinacholenga kuipeleka nchi mbali kimuziki.

"Harmonize ni mtu ambaye wakati mwingi ninasikiliza nyimbo zake, hususan wimbo ambao nimeuimba pale juu (Amelowa) ni wimbo ambao umeniteka.

"Halafu pia niko kwao na sikuona vibaya kuonyesha upendo kwamba ingawa hayupo bado tunaweza kuonyesha heshima kwa mfalme wao," alisema Abdul Kiba.

"Naweza nikasema kwamba ninakubali kazi zake ambazo anafanya, zinaonekana, anajituma na kupambana na pia anaonyesha anataka kuipeleka nchi sehemu gani kwenye muziki.



# MIAKA MIWILI YA DK. MWINYI KUADHIMISHWA KWA RIADHA

**Na Mwandishi Wetu**

KATIKA kuadhimisha miaka miwili ya uongozi wa Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, Kamati ya Zanzibar Blue Economy Athletics Club Championship 2022, imeandaa mashindano ya kugombea Ubingwa wa Riadha yatakayofanyika Novemba 4-6, mwaka huu, katika Uwanja wa Amaan mjini Zanzibar.

Mwenyekiti wa maandalizi ya klabu hiyo, Idrissa Majura, amesema licha ya mashindano hayo kuwa miongoni mwa shamrashamra za kuadhimisha miaka miwili ya Rais Mwinyi, pia ni kutekeleza ilani ya Chama Cha Mapinduzi ya kuutangaza uchumi wa buluu pia kukuza michezo visiwani humo.

Hata hivyo, Mwenyekiti huyo amesikitishwa na Taasisi za Zanzibar kutokuwa na mwamko wa kuchangia kwani ni ZECO pekee iliyowachangia kati ya sita zilizopelekewa maombi.

''Mwaka jana tulipeleka maombi PBZ tu na walituchangia Sh. milioni 10, mwaka huu tumeongeza wigo wa maombi bado sehemu nyingi tumetoka mikono mitupu," alisema.

Pia amevishukuru vyombo vya Habari vya ZBC, Chanel Ten, Azam Media na AM24 FM 98.5 Zanzibar ambavyo vitawatangazia matangazo ya kuhamasisha mashindano hayo ili wananchi wajitokeze kwa wingi Uwanja wa Amaan kushuhudia patashika hiyo.

"Hadi tulipofikia uamuzi wa kuandaa Zanzibar Blue Economy Club Championship 2022, tulikuwa tumekusanya Sh. milioni 6.6 tu kati ya bajeti ya Sh. milioni 77 ambapo Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) walikuwa wametuchangia milioni tano, Jitegemee Holdings Company Ltd walikuwa wametuchangia shilingi milioni moja huku Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF) wakilituchangia Sh.600,000,"alisema Majura.

Aidha, alisema mshindi wa jumla katika mashindano hayo atapata zawadi ya Sh. 1,000,000, kombe na medali, mshindi wa pili Sh. 800,000, kombe na medali huku wa tatu akibeba Sh. 500,000/- kombe na medali.

**DALUGA...**



Beki wa Yanga, Kibwana Shomari, akiruka daluga la mshambuliaji wa Simba, Pape Sakho kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara, iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam mwishoni mwa wiki na kumalizika kwa sare ya bao 1-1, shukrani kwa Agustine Okrah na Stephane Aziz Ki, waliozifungia timu zao. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Simba Queens yapaa Morocco michuano CAF

**Adam Fungamwango na Saada Akida**

KIKOSI cha wachezaji 25 na benchi la ufundi pamoja na baadhi ya viongozi wa timu ya wanawake ya Simba Queens, kimeondoka leo alfajiri kuelekea nchini Morocco, tayari kwa fainali za Ligi ya Mabingwa Afrika zinazotarajiwa kuanza kutimua vumbi Oktoba 30, mwaka huu.

Meneja Habari na Mawasiliano wa klabu hiyo, Ahmed Ally amesema kikosi hicho kilitarajiwa kuondoka leo alfajiri na ndege ya Shirikila la Ndege la Uturuki ambapo kwanza itafika kwenye nchi hiyo iliyo barani Ulaya kabla ya kubadilisha ndege nyingine kuelekea Morocco ambako michuano hiyo itachezwa.

Akizungumza jana kabla ya kuondoka, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Charles Lukula, amesema kikosi kinaondoka kikiwa hakina majeruhi hata mmoja na kiko katika hali nzuri ya ushindani.

"Hatuna majeruhi hata mmoja, tunaenda Morocco tukiwa na kikosi kamili. Tumecheza mechi za kirafiki na timu ipo kwenye hali nzuri ya ushindani," alisema kocha huyo.

Lukulu alisema wamejiandaa kwenda kushindana na kufikia malengo yanayotarajiwa na Wanasimba na Watanzania kwa ujumla.

Alisema amewafuatilia wapinzani wao hao kwa kuona ubora wao, hivyo akafanyia kazi mapungufu ya kikosi chake ili kwenda kufanya vizuri katika mchezo wa kwanza katika kundi lao.

"Tumefanya maandalizi mazuri tumecheza mechi za kirafiki za kutosha, vijana wangu wako vizuri na tunaimani ya kupambana kupata matokeo mazuri," alisema kocha huyo.

Alisema anatambua michuano hiyo haitakuwa rahisi kwa sababu Simba Queens ni mara ya kwanza kushiriki na kuna baadhi ya timu zoefu.

Nahodha wa timu hiyo, Opa Clement, aliwashukuru viongozi wa klabu ya Simba kwa sapoti kubwa ambayo wamepata, ikiwa ni pamoja na maandalizi, hivyo kuwahakikishia kufanya vema kwenye michuano hiyo.

"Tunawashukuru viongozi wetu kwa sapoti kubwa wanayotupa, wamekuwa wakiweka mazingira yetu ya kazi kuwa rahisi, kikubwa tunawaomba mashabiki waendelee kutuombea, ingawa hawatakuwapo uwanjani. Tunafahamu michuano itakuwa migumu, lakini lengo letu ni kuhakikisha tunafika hatua ya nusu fainali," alisema nahodha huyo ambaye anacheza nafasi ya ushambuliaji.

Kwa mujibu wa ratiba iliyotolewa, Simba Queens itafungua dimba Oktoba 30, kwa kucheza dhidi ya wenyeji Asfar FC ya nchini humo, kabla ya kukutana na Determine Girls ya Liberia Novemba 2, na kumalizia mechi yao ya Kundi A Novemba 5, mwaka huu dhidi ya Green Buffaloes ya Zambia.

Simba Queen ilipata nafasi hiyo baada ya kuibuka kuwa Mabingwa wa Afrika Mashariki na Kati, hivyo kuwa wawakilishi michuano hiyo kwenye Ukanda wa CECAFA.

## Baseball Z'bar yaenda Japan

**Na Shufaa Lyimo**

TIMU ya wachezaji 13 na viongozi watatu wa mchezo wa Baseball Visiwani Zanzibar, jana mchana imekwea 'pipa' kuelekea Japan kushiriki mashindano ya ndani ya vijana yatakayofanyika Oktoba 27, mwaka huu, nchini humo.

Akizungumza na gazeti hili jana kutoka visiwani humo, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Mohamed Rajabu, alisema ana imani na wachezaji wake kufanya vizuri katika mashindano hayo kutokana na mazoezi ya muda mrefu waliyoyafanya.

"Sina wasiwasi na wachezaji wangu, nimewapa mazoezi ya kutosha, naamini tutarudi na kombe la ushindi," alisema Rajabu.

Kwa upande wa nahodha wa timu hiyo, Abdulmounim Othman, alisema wamejipanga vizuri kuhakikisha wanakwenda kuitangaza Tanzania kupitia mashindano hayo.

"Mipango yetu ni kwenda kuwaonyesha kuwa Tanzania tunaufahamu mchezo huu, tunaahidi kurudi nyumbani na kombe, alisema Othman.

## Kocha Singida aianika Ihefu

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kupata ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Ihefu FC juzi, Kocha Msaidizi wa Singida Big Stars, Mathias Lule, amesema walistahili kupata ushindi huo kutokana na kuwasoma vizuri wapinzani wao hao na kugundua kuwa mabeki wake ni imara lakini si wanyumbulifu, hivyo wakawawekea straika Dario da Silva kwa ajili ya kuwafungua ili kupatikana nafasi za kufunga kirahisi.

Akizungumza baada ya mechi hiyo iliyochezwa Uwanja wa Liti mkoani Singida, Lule alisema kutokana na aina yao ya uchezaji, walijua wacheze vipi ili kupata mkwaju wa penalti na kweli ilipatikana, lakini ikakoswa na straika wa zamani wa Simba, Meddie Kagere ambaye sasa anakipiga na kikosi hicho.

"Kabla ya kwenda kucheza nao tulikuwa tunajua tunakwenda kucheza na timu ya aina gani, tuliisoma na kugundua kuwa ina mabeki wazuri, lakini si wanyumbulifu, kutokana na hilo sisi tukaamua kuwaweka Dario pale kwa sababu yeye ni mnyumbulifu ili awafungue na kweli tulifanikiwa.

"Na kwa aina hiyo ya uchezaji wao ilikuwa ni rahisi sisi kupata penalti. Tulijua kuwa tunapata kama si mbili basi moja na kweli tulifanikiwa, lakini kwa bahati mbaya tukakosa na tuliambizana na wachezaji wetu tujitahidi sana tupate mabao ya mapema, ikawa kama tulivyotarajia, ingawa kwenye mechi hii tumepata bao moja," alisema.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### KANE KUSAINI TENA SPURS

KLABU ya Tottenham Hotspur inataka kukubaliana kuhusu mkataba mpya na mshambuliaji wa England, Harry Kane mapema mwaka ujao na wana uhakika mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29, ataweka mustakabali wake wa muda mrefu katika klabu hiyo. ***(90Min)***

### BAYERN HAITAINGIA SOKONI

MKURUGENZI wa michezo wa Bayern Munich, Hasan Salihamidzic, amesema klabu hiyo ya Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga, ambayo imekuwa ikihusishwa na kutaka kumnunua Harry Kane, haitaingia sokoni katika dirisha la uhamisho la Januari. ***(Bild, via Christian Falk)***

### NYOTA WA3 KUMRITHI RONALDO

MSHAMBULIAJI wa Bayer Leverkusen raia wa Jamhuri ya Czech, Patrik Schick mwenye umri wa miaka 26, nyota wa Lille na Canada, Jonathan David (22), na Mfaransa wa Lyon, Moussa Dembele (26), ndio chaguo linalopendekezwa na Erik Ten Hag kuchukua nafasi ya Cristiano Ronaldo. ***(Mirror)***

### LEAO KIPAUMBELE CHELSEA

KLABU ya Chelsea itaweka kipaumbele kwa kumnunua mshambuliaji wa AC Milan na Ureno, Rafael Leao mwenye umri wa miaka 23, badala ya kumnunua Ronaldo. ***(CBS, Mirror)***

### PSG SHAKA KWA MBAPPE

KLABU ya Paris St-Germain ina shaka juu ya uwezo wao wa kuendelea kulipa mkataba wa mshambuliaji wa Ufaransa, Kylian Mbappe. Mkataba wa sasa wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23, una thamani ya pauni milioni 549 kwa miaka mitatu - robo ya jumla ya bajeti ya timu. ***(Sport)***

### SLONINA KWA MKOPO

CHELSEA wanafikiria chaguo la kumtoa kwa mkopo mlinda mlango Mmarekani mwenye umri wa miaka 18, Gabriel Slonina, ambaye walimsajili kwa pauni milioni 12 msimu wa majira ya joto. ***(Evening Standard)***

### NAPOLI YAMMULIKA RONALDO

CRISTIANO Ronaldo yuko tayari kurejea Italia, huku Napoli wakiwa bado na nia ya kukamilisha mpango huo waliokuwa nao tangu msimu wa majira ya joto. ***(Sun)***

### ZAKHARYAN AWINDWA DARAJANI

KLABU ya Chelsea bado ina nia ya kumsajili kiungo wa kati wa Urusi, Arsen Zakharyan mwenye umri wa miaka 19, kutoka Dynamo Moscow. ***(Sport Express, Metro)***

### CONTE AHITAJI USAJILI

KOCHA Antonio Conte anaamini atahitaji madirisha matatu zaidi ya uhamisho ili kuboresha upana wa kikosi cha Tottenham Hotspur. ***(Times)***

### ASENSIO MKATABA MPYA

KLABU ya Real Madrid inajiandaa kumpa mkataba ulioboreshwa miaka mitatu mshambuliaji wa Hispania, Marco Asensio mwenye umri wa miaka 26, ambaye alihusishwa na kuhamia Arsenal, Liverpool na Tottenham baada ya kukataa ofa ya awali. ***(Ser Deportivos)***

### POSTECOGLOU AIKATAA EPL

KOCHA wa Celtic, Ange Postecoglou, amepuuzilia mbali uvumi wa kutaka kuhamia Ligi kuu England, huku kukiwa na ripoti zinazomhusisha na kazi katika klabu za Brighton na Leicester City. ***(Mail)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# UNITED, RONALDO RASMI WAJIANDAA KUACHANA

●●●Pande zote mbili ziko tayari kusubiri wiki tatu zilizobaki za soka la nyumbani kabla ya...

**MANCHESTER, England**

MANCHESTER United na Cristiano Ronaldo wako tayari kuachana baada ya mzozo wa hivi majuzi kati ya mchezaji huyo na kocha, Erik ten Hag, ingawa namna ya kuondoka kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 37, pale Old Trafford bado iko hewani.

Kwa mujibu wa 90min, kuondoka kwa Ronaldo kwenye benchi la wachezaji wa akiba kabla ya filimbi ya mwisho wakati wa ushindi wa United dhidi ya Tottenham wiki iliyopita, ndio haswa kulikoibua mzozo huo.

Na sasa Ronaldo hayupo kwenye kikosi cha kwanza cha Man United na hajajumuishwa katika mechi za mwishoni mwa wiki.

Pande zote mbili ziko tayari kusubiri wiki tatu zilizobaki za soka la nyumbani kabla ya Kombe la Dunia ili kufanya maamuzi.

United watacheza mechi mbili za Ligi ya Europa dhidi ya Sheriff na Real Sociedad, mechi tatu za Ligi Kuu dhidi ya West Ham, Aston Villa na Fulham na mechi ya Kombe la Ligi - pia dhidi ya Villa - kabla ya Ronaldo kusafiri kwenda Qatar na timu ya Taifa ya Ureno katikati ya Novemba.

United ina wachezaji wengine wa kikosi cha kwanza ambao wanatarajiwa kushiriki katika michuano hiyo.

Inatarajiwa kwamba Ronaldo, atarejea United - ikiwa atakubaliwa na Ten Hag baada ya mzozo huo na wanatarajiwa kukutana kule Carrington ili kufanya mazungumzo yao ya mwisho.

Ronaldo ndiye mchezaji anayelipwa fedha nyingi zaidi pale United, lakini mkataba unamalizika mwishoni mwa msimu huu, na kuna uhakika kwamba ataondoka katika klabu hiyo mwanzoni mwa 2023.

United ilifikiria kumwachia mchezaji huyo kwa uhamisho wa bure kabla ya dirisha la Januari, lakini hii haionekani kama chaguo bora, kwani inaonekana inaweza kuwa na gharama kubwa.

Ikiwa Ronaldo ataondoka inaeleweka kuwa Ten Hag atahitaji fowadi mwingine kwenye kikosi chake. Cody Gakpo wa PSV, ambaye anawakilishwa na mawakala wa Ten Hag, anachukuliwa kuwa chaguo sahihi kwake.

Gakpo amefurahia msimu mzuri wa PSV hadi sasa, akiwa na mabao tisa na asisti tisa katika michezo 11 ya Eredivisie hadi sasa.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,044,3

MECHI KALI
BARCELONA
VERSUS
BAYERN MUNCHEN
1 | 2.33
X | 3.66
2 | 2.65

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa vodacom m-pesa airtel money
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 18+ HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# ZIDANE AGUSIA KURUDI KWENYE UKOCHA



**MADRID, Hispania**

ZINEDINE Zidane ametania kuwa atarejea kufundisha "hivi karibuni", huku kukiwa na uvumi kwamba atakuwa mrithi wa Didier Deschamps katika Timu ya Taifa ya Ufaransa.

Kocha huyo aliyeshinda taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya mara tatu, amekuwa nje ya dimba tangu aondoke Real Madrid mwaka 2021, lakini amekuwa akihusishwa na kazi nyingi za juu barani Ulaya.

Klabu za Juventus na Paris Saint-Germain zimekuwa zikihusishwa naye, ingawa kuchukua mikoba ya kuinoa 'Les Bleus' baada ya Kombe la Dunia nchini Qatar, inaendelea kuonekana kuwa na nafasi kubwa zaidi kwake.

Zidane akizungumzia uvumi huo alitania kwa kusema: "Je, ninakosa suti ya kufundishia? Hapana, siko mbali. Tusubiri, tusubiri kidogo. Hivi karibuni, karibuni sana," alinukuliwa na RMC Sport.

Zidane pia alizungumzia kuhusu Kombe la Dunia nchini Qatar, ambako Ufaransa itatetea taji waliloshinda nchini Urusi miaka minne iliyopita, akisema kwa sasa haifai kuzungumza lolote kuhusu ukosoaji.

"Nadhani tunapaswa kuacha mabishano kando na kuacha nafasi ya mchezo na mahali pa Kombe la Dunia," aliongeza.

"Hata hivyo, tutakachosema kuhusu jambo lolote, kamwe hakitakuwa sawa, kamwe si kweli na haitakuwa sahihi. Kwa hiyo tunapaswa kuacha nafasi ya soka na ushindani ili mashabiki wote wawe na wakati mzuri."

Ufaransa wataanza kutetea taji lao Novemba 22 dhidi ya Australia, kisha kucheza na Denmark na baadaye Tunisia katika Kundi D.

# Emery amrithi Gerrard Villa

**LONDON, England**

KLABU ya Aston Villa imemteua Unai Emery kuwa kocha wao mkuu mpya.

Villa walikuwa wakimtaka bosi wa Sporting CP, Ruben Amorim kama mrithi wa Steven Gerrard, lakini walifahamu Jumatatu kwamba Mreno huyo hakuwa na nia ya kuchukua mikoba hapo Villa Park licha ya mazungumzo ya awali kuwa mazuri.

Kwa mujibu wa 90min, kocha mkuu wa zamani wa Arsenal, Emery, lilikuwa jina lingine linalozingatiwa na uongozi wa Villa na Mhispania huyo, ameamua kuondoka Villarreal ili kurejea Ligi Kuu England- chini ya miaka mitatu baada ya kupoteza kazi yake katika Uwanja wa Emirates.

Villa haijathibitisha urefu wa mkataba wa Emery, lakini vyanzo vimedokeza kuwa karibu pauni milioni sita zilihitajika kumnunua kocha huyo mwenye umri wa miaka 50, kutoka kwenye mkataba wake na Villarreal.

Ataanza kazi yake mpya Novemba Mosi, mwaka huu baada ya taratibu za kibali cha kazi kukamilika.

Emery ameonja mafanikio katika Ligi ya Europa akiweka rekodi ya kulitwaa taji hilo mara nne - mara tatu akiwa na Sevilla na mara moja akiwa na Villarreal na alinyanyua mataji sita katika kipindi kifupi kama kocha mkuu wa Paris Saint-Germain.

Anarithi timu ya Villa iliyochochewa na kipigo chao cha 4-0 dhidi ya Brentford siku ya Jumapili, ingawa matokeo kabla ya hapo yalikuwa ya kusikitisha.

Kocha wa zamani wa Rangers, Gerrard alifukuzwa kazi baada ya miezi 11 tu katika kibarua hicho baada ya mwendo mbaya wa matokeo uliozaa pointi tisa pekee katika mechi 11 za Ligi Kuu hadi sasa.



# HABARI MICHEZO

303,118/-

SUPA JACKPOT
MECHI WIKI HII
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 29/10/22 | 17:00 | Hull City vs Blackburn | 2.59 | 3.19 | 2.74 |
| 02. 29/10/22 | 17:00 | Wigan vs Watford | 2.93 | 3.28 | 2.39 |
| 03. 29/10/22 | 17:00 | Preston vs Middlesbrough | 2.68 | 3.13 | 2.68 |
| 04. 29/10/22 | 17:00 | Huddersfield vs Millwall | 2.99 | 3.24 | 2.37 |
| 05. 29/10/22 | 17:00 | Brighton vs Chelsea | 2.94 | 3.29 | 2.38 |
| 06. 29/10/22 | 19:30 | Fulham vs Everton | 2.29 | 3.42 | 2.97 |
| 07. 29/10/22 | 19:30 | Eintracht Frankfurt vs Borussia Dortmund | 2.93 | 3.52 | 2.25 |
| 08. 29/10/22 | 21:30 | St. Pauli vs SV Darmstadt | 2.53 | 3.53 | 2.58 |
| 09. 30/10/22 | 15:00 | AJ Auxerre vs AC Ajaccio | 2.45 | 3.07 | 2.97 |
| 10. 30/10/22 | 15:30 | Hannover vs Karlsruher SC | 2.41 | 3.43 | 2.79 |
| 11. 30/10/22 | 15:30 | Sandhausen vs Eintracht Braunschweig | 2.63 | 3.22 | 2.68 |
| 12. 30/10/22 | 15:30 | Paderborn vs Hamburger SV | 2.28 | 3.73 | 2.79 |
| 13. 30/10/22 | 16:15 | FC Sion vs FC Zurich | 2.39 | 3.48 | 2.79 |
| 14. 30/10/22 | 17:00 | Brest vs Reims | 2.40 | 3.33 | 2.83 |
| 15. 30/10/22 | 18:30 | Boavista vs Vizela | 2.50 | 3.25 | 2.80 |
| 16. 30/10/22 | 19:00 | Sandefjord vs Ham-Kam | 2.58 | 3.37 | 2.63 |
| 17. 30/10/22 | 19:05 | Lorient vs Nice | 2.57 | 3.26 | 2.67 |

MECHI ZA USHINDI
"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMATANO - 26/10/2022

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 09:30 | 5976 | Hainan Star vs Qingdao Red Lions | 1.66 | 3.84 | 4.18 |
| 10:00 | 2133 | Hebei Kungfu vs Nantong Zhiyun | 3.54 | 3.25 | 1.96 |
| 10:00 | 5549 | Sichuan Jiuniu vs Beijing BG | 1.39 | 4.08 | 7.39 |
| 12:00 | 1317 | Zlin U19 vs Slovacko U19 | 1.64 | 4.08 | 4.08 |
| 13:30 | 1824 | Anyang vs Suwon Samsung | 2.49 | 3.13 | 2.64 |
| 13:30 | 5571 | Daejeon Citizen vs Sangju Sangmu | 2.27 | 3.16 | 2.92 |
| 15:00 | 2269 | TSV St. Johann vs SK Bischofshofen | 5.25 | 4.47 | 1.46 |
| 15:00 | 3226 | Pobeda Junior vs FC Struga Trim Lum | 14.62 | 5.07 | 1.20 |
| 15:00 | 4221 | Rabotnicki Sk vs Sileks | 2.73 | 2.78 | 2.68 |
| 15:00 | 4936 | Shkupi Skopje vs FK Tikves Kavadarci | 1.35 | 4.70 | 8.40 |
| 15:00 | 5424 | FK Skopje vs Shkendija | 9.80 | 4.80 | 1.32 |
| 15:30 | 2503 | SKF Sered vs Spartak Trnava | 15.59 | 9.74 | 1.07 |
| 15:30 | 4845 | MFK Dolny Kubin vs FC Petrzalka 1898 | 2.58 | 3.50 | 2.34 |
| 16:00 | 3139 | Ruvu Shooting vs Geita Gold FC | 2.83 | 2.78 | 2.59 |
| 16:00 | 3468 | Ararat Armenia vs Alashkert Martuni | 2.48 | 2.97 | 2.77 |
| 16:00 | 3489 | Uganda Revenue Authority FC vs Bright Stars | 1.35 | 3.75 | 10.70 |
| 16:30 | 1408 | Kokand 1912 vs Sogdiyona Jizzax | 3.30 | 3.25 | 2.04 |
| 16:30 | 1942 | US Ben Guerdane vs ES Metlaoui | 2.48 | 2.77 | 2.97 |
| 16:30 | 2455 | JDR Stars vs Venda Football Academy | 2.05 | 2.82 | 3.89 |
| 16:30 | 4988 | Otmk Olmaliq vs Dinamo Samarqand | 1.27 | 4.86 | 9.14 |
| 17:00 | 1348 | Rapid Vienna vs TSV Hartberg | 1.51 | 4.17 | 5.04 |
| 17:30 | 2197 | Hajduk Split vs HNK Gorica | 1.34 | 4.57 | 7.39 |
| 17:55 | 2498 | Alshoulla vs Al Qadisiyah | 2.10 | 2.83 | 3.71 |
| 18:00 | 2344 | GKS Jastrzebie Zdroj vs PKS Olimpia Elblag | 1.81 | 3.30 | 4.07 |
| 18:00 | 2512 | VPS Vaasa vs Haka | 2.48 | 3.25 | 2.57 |
| 18:00 | 3900 | Zrinjski Mostar vs FK Sloga Simin Han | 1.43 | 4.18 | 6.22 |
| 18:00 | 5904 | Farco FC vs Haras EL Hodood | 2.48 | 2.79 | 3.19 |
| 18:05 | 3566 | AL Arabi (SA) vs Najran SC | 2.12 | 3.02 | 3.36 |
| 19:00 | 1047 | Young Africans vs KMC | 1.30 | 4.48 | 9.54 |
| 19:00 | 2811 | Krsko Posavje vs NK Dob | 2.48 | 3.40 | 2.48 |
| 19:45 | 1902 | Inter vs Viktoria Plzen | 1.11 | 7.91 | 19.78 |
| 19:45 | 3464 | Brugge vs Porto | 3.17 | 3.37 | 2.14 |
| 19:50 | 5436 | Al Jabalain vs AL Khlood | 2.05 | 2.93 | 3.71 |
| 20:30 | 3966 | Marumo Gallants FC vs Amazulu | 2.67 | 2.86 | 2.81 |
| 20:30 | 5162 | FC Altona 93 vs TuS Dassendorf | 5.80 | 4.80 | 1.44 |
| 21:00 | 3442 | Deportivo Iztapa vs Club Xelaju | 1.97 | 3.06 | 3.74 |
| 21:00 | 4441 | Cronenberger SC vs 1 FC Kleve | 3.78 | 4.46 | 1.64 |
| 21:30 | 1923 | Swindon Supermarine vs Hanwell Town | 2.16 | 3.89 | 2.63 |
| 21:45 | 2530 | Gosport Borough vs Harrow Borough | 1.64 | 3.99 | 4.19 |
| 21:45 | 3079 | Plymouth Parkway vs Tiverton Town | 2.14 | 3.60 | 2.82 |
| 21:45 | 5013 | Havant and Waterlooville vs Bath City | 1.72 | 3.65 | 4.08 |
| 22:00 | 1587 | Barcelona vs Bayern Munchen | 2.33 | 3.66 | 2.65 |
| 22:00 | 2605 | Atletico Madrid vs Bayer Leverkusen | 1.70 | 3.72 | 4.46 |
| 22:00 | 3496 | Ajax vs Liverpool | 3.62 | 3.92 | 1.82 |
| 22:00 | 3821 | Napoli vs Rangers | 1.21 | 6.15 | 10.92 |
| 22:00 | 3876 | Sheffield Wed vs Bristol Rovers | 1.48 | 4.26 | 5.95 |
| 22:00 | 4614 | Tottenham vs Sporting Lisbon | 1.43 | 4.55 | 6.13 |
| 22:00 | 4848 | Eintracht Frankfurt vs Marseille | 2.25 | 3.28 | 3.03 |
| 23:00 | 2549 | M. Zacatecas vs CF Atlante | 2.66 | 3.05 | 2.52 |
| 23:30 | 3595 | 12 de Octubre de Itaugua vs Sportivo Ameliano | 2.82 | 3.21 | 2.30 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# VIZIWI KAMBINI KUWANIA TAJI LA UREMBO LA DUNIA JUMAMOSI

**Na Shufaa Lyimo**

WASHIRIKI mbalimbali wa Shindano la Dunia la Urembo, Utanashati na Mitindo kwa viziwi, litakalofanyika nchini Jumamosi wiki hii, wametembelea maeneo mbalimbali ya Jiji la Dar es Salaam jana ikiwamo Ukumbi wa Mwalimu Julius Nyerere, sehemu ambayo litafanyika.

Washiriki hao pia walitembelea Fukwe za Coco pamoja na kupata nafasi ya kupiga picha kwenye daraja la Tanzanite.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, Mkurugenzi wa Idara ya Maendeleo na Sanaa, Emanuel Ishengoma, alisema lengo la kuwatembeza kwenye maeneo hayo ni kulitangaza taifa letu ili kukuza utalii wa ndani.

"Tumefanya hivi kwa lengo la kumuunga mkono Rais wetu Samia Suluhu Hassan, kutangaza utalii kupitia filamu ya Royal Tour," alisema Shengoma.

Mkurugenzi huyo alisema baada ya shindano hilo washiriki hao watapelekwa kufanya utalii wa ndani kwenye Mbuga ya Wanyama ya Serengeti na visiwani Zanzibar.

Alisema washiriki wote ambao walithibitisha kushiriki wamewasili na kwamba mchujo utafanyika Ijumaa wiki hii ili wapatikane vinara watakaoshindanishwa siku hiyo ya shindano.

Naye Rais wa shindano hilo Afrika, Habibu Mrope, alisema mshindi atapatikana kutokana na vigezo vyake na kwamba hakutakuwa na upendeleo wowote.

Alisema baada ya washiriki wa mataifa hayo kuwasili wameweka kambi ya kimataifa iliyohusisha wote kwa ujumla.

## UMETUHESHIMISHA...




Mwakilishi wa Valor Tv, akimkabidhi Kaimu Kocha Mkuu wa Simba Tuzo na Hati ya Pongezi kwa kufanikiwa kuifikisha timu hiyo hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika. Kocha Msaidizi wa Simba, Selemani Matola naye alikabidhiwa tuzo na hati hiyo ya pongezi katika hafla fupi iliyofanyika jijini Dar es Salaam jana. **MPIGAPICHA WETU**

# Azam yaongeza dozi

INATOKA UK. 32

kujiweka sawa na kujituma zaidi ili kufanya vizuri," amesema Kali.

Azam inakwenda kucheza mechi hiyo kwa mara ya kwanza baada ya kumtimua Lavagne, kutokana na kuondolewa kwenye Kombe la Shirikisho Afrika na kisha kuchapwa mabao 2-1 dhidi ya KMC kwenye mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara.

Kuhusu kuhamishia mechi yao ya nyumbani Uwanja wa Benjamin Mkapa badala ya kupigwa Azam Complex, Chamazi, Kaimu Ofisa Habari wa klabu hiyo, Hasheem Ibwe, alisema hayo ni matakwa binafsi ya klabu na ni sehemu ya kanuni ambazo wamezitumia kwamba mwenyeji anaweza kuamua baadhi ya mechi zake zipigwe mbali na uwanja halisi wa nyumbani.

# Kocha Nabi njiapanda

INATOKA UK. 32

dimbani kwa tahadhari kubwa ili kuendelea na malengo yao.

Alisema haitakuwa mechi rahisi kutokana na ubora wa wapinzani wao ikiwamo uimara wa benchi la ufundi la timu hiyo huku wachezaji wakionyesha kujitoa wakati wote uwanjani.

"Haitakuwa mechi rahisi, nimewaona mechi mbili tunahitaji kucheza kwa tahadhari kubwa kuhakikisha tunapata matokeo, baada ya mechi ya Simba tumerejea mazoezini kwa kufanyia kazi mapungufu na ubora wetu kusaka pointi tatu," alisema Nabi.

Kocha Msaidizi wa KMC FC, Ahmad Ally, yeye alisema wanaenda kucheza mechi ngumu na timu bora na kwamba utakuwa mchezo utakaotawaliwa na ufundi na mbinu nyingi.

Alisema wachezaji wako tayari na wameona ubora na madhaifu ya Yanga kwa kuwaangalia mechi iliyopita, hivyo tutatumia mapungufu yao kutafuta pointi muhimu.

"Mechi itakuwa ya kiufundi kwa asilimia kubwa na nidhamu kwa sababu Yanga wanashambulia wote na kukaba hivyo hivyo, pia tumeona safu yao ya mawinga nayo pia tumeangalia hilo na tunaenda kusahau matokeo chanya tuliyopata dhidi ya Azam," alisema Ahmad.

Michezo
Jumatano Oktoba 26, 2022
Nipashe



UKURASA 29

## United, Ronaldo rasmi wajiandaa kuachana

# KOCHA NABI NJIAPANDA YANGA SC IKIIVAA KMC

## Hofu yatanda kila kona kuhusu kibarua chake, Mkwasa atajwa…

**Na Saada Akida**

HUKU sintofahamu ikiendelea kutanda kuhusu hatima ya kibarua cha Kocha Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi, ndani ya klabu hiyo, leo ataendelea kukiongoza kikosi hicho kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara dhidi ya KMC FC baada ya jana kuzungumza na vyombo vya habari kuelekea mchezo huo.

Kumekuwa na tetesi nyingi za Nabi kukalia kuti kavu tangu Yanga ifurushwe nje ya michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika na Al Hilal ya Sudan kwa jumla ya mabao 2-1, baada ya sare ya 1-1 Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam na kwenda kuangukia pua ugenini kwa kuchapwa 1-0.

Hata hivyo, hakuna kiongozi yeyote wa Yanga amekuwa tayari kujitokeza hadharani kutoa ufafanuzi wa kukubali ama kukanusha kuhusu tetesi hizo, zaidi ni vyanzo vya ndani vya klabu hiyo vimekuwa vikieleza lakini kwa sharti la kutotajwa majina.

Chanzo kimoja ndani ya klabu hiyo kimedai kwamba mazungumzo yanaendelea na Kocha Mkuu wa Ruvu Shooting, Charles Boniface Mkwasa, kuja kukaimu nafasi hiyo, wakati huu taratibu za kuvunja mkataba na kocha huyo zikiendelea.

“Huenda tukaachana naye tutakapokwenda Tunisia kucheza mechi ya marudiano ya kuwania kufuzu Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya Club Africain na nafasi yake atakaimu kwa muda Mkwasa kama atakubali,” kilieleza chanzo chetu.

Chanzo hicho kiliendelea kufafanua kuwa Kocha Msaidizi, Cedric Kaze, yeye atahamishiwa nafasi ya Mkurugenzi wa Ufundi iliyokuwa ikishikiliwa na Mwinyi Zahera, ambaye kwa sasa amemaliza mkataba wake.

Hata hivyo, wakati hayo yakiendelea Nabi ameendelea kutekeleza majukumu yake kama kawaida na jana akizungumzia mchezo wa leo dhidi ya KMC, alisema ameiona timu hiyo katika michezo miwili msimu huu, ilipocheza na Simba na Azam na kuona ubora kwa wapinzani wao hao, jambo ambalo wanapaswa kushuka

INAENDELEA UK. 31



Nabi

## Azam yaongeza dozi pointi Simba

**Na Hadija Mngwai**

KAIMU Kocha Mkuu wa Azam FC, Kali Ongala, amesema kutokana na mchezo unaowakabili mbele yao dhidi ya Simba, amelazimika kuongeza dozi ya mazoezi ili kuweza kuibuka na pointi tatu kesho.

Azam inatarajia kuikaribisha Simba katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam kesho kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara itakayopigwa majira ya saa moja usiku.

Kali amekabidhiwa mikoba ya kukiongoza kikosi cha Azam FC kutoka kwa aliyekuwa Kocha Mkuu, Mfaransa Denis Lavagne ambaye alidumu na klabu hiyo kwa kipindi cha mwezi mmoja tu kabla ya kufurushwa wiki iliyopita.

Akizungumza na Nipashe jana, Kali alisema ana kibarua kigumu kuikabili Simba kutokana na uwezo waliokuwa nao wapinzani wao hao kwa sasa na hasa ikizingatiwa ni timu kubwa kuliko wao.

“Mchezo wetu na Simba utakuwa mgumu hii ni dabi nyingine, timu zote kubwa, ila ukiangalia wapinzani wetu wapo kwenye fomu, lakini sisi bado hatupo vizuri hivyo mchezo utakuwa na ushindani.

“Tunahitaji kupambana ili tuweze kuwa vizuri ambapo tunahitaji kuendelea na mazoezi kwa kiwango kikubwa ili tuwe vizuri na kuweza kuibuka na pointi tatu katika mchezo huo.

“Huu ni wakati mwingine, hivyo tunahitaji kupambana, unajua anapobadilisha kocha, kocha mwingine unakuwa na wakati mgumu, lakini tunahitaji

INAENDELEA UK. 31

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >